Msimulizi, 1889[1]

Edited and corrected by
Arvi Hurskainen
Department of World Cultures, Box 59
FIN-00014 University of Helsinki, Finland
arvi.hurskainen@helsinki.fi

Abstract

This is a corrected version of Msimulizi, the first periodical written and printed in Swahili language. The periodical was established to be an information channel between scattered mission station of the Universities' Mission to Central Africa, and also between the supporters of the mission work in Great Britain. The perodical was originally scanned and made available by SOAS (School of Oriental and African Studies, London). Obvious scanning errors were corrected. Also, clear errors in original print text were corrected. However, nonstandard spelling was not corrected, if it was possible to assume that the writer intended to write in the way it was done.

The file follows the original pagination. A page in the original publication is a page in this file. Page numbering is continuous from year to year, and it is printed at the top of the page.

This file contains the text of year 1889.

MSIMULIZI. February, 1889. III.
Imepigwa chapa Kiungani, Zanzibar,
katika "Universities' Mission to Central Africa,"

HABARI ZA VITA YA PWANI.

Uthia huu unazidi sana. Watu wa Mlima wanazidi kukasirikia Wadoicha. Kwani wamepiga mizinga mji wa Dares-salaam, imeharibika pia. Walikaa kule Waalimu Wadoicha waliowatunza

[1] The text is issued under licence CC BY-NC

wahuru wao waliowakamata mateka siku hizi baharini, bassi walitokea Waarabu wakawanyang'anya wote wapata 200 wakawachukua utumwani tena. Wale Waalimu walijiponya kwa shidda tu mtumbwini. Marra wale Waarabu wakaenda safari ya saa tatu hatta mji mwingine walipofanya Wadoicha 'Mission' wakamua bibi mmoja na waume wawili Wadoicha, na wangine wakachukua wawatakie ukombozi.

Tena Mwingreza mmoja Mwalimu wa Chama cha L.M.S. jina lake Mr Brooks ameuawa na watu wa pwani alipokaribia Saadani. Tena mizigo yetu sisi yaliyopelekwa Magila imezuiwa Pangani, hapana ruhusa kuipeleka juu. Tena Mr Key alijaribu kutokea Tanga lakini alikatazwa.

Lakini kule kwenyi Mvita katika enzi ya Waingreza tunasikia amani nyingi kuliko pande hizo za chini wanazozitaka Wadoicha. Bassi mwisho wa uthia huu hautambulikani kabisa bado.

UGANDA, FITINA NA MAFUKUZO.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Habari kubwa sana zimetoka katika Uganda siku hizi, na hakika yao haswa ni hii. Yule Mwanga aliyetawala huko alifanya shauri ya kuwaua kikosi chote wanaoitwa Walinzi wake, sijui kwa kosa gani. Bassi alinia kuwachukua naye na kuwashusha penyi kisiwa kimoja kidogo na kuwaacha wafe kwa njaa. Lakini alipowaleta pwani akasema Ingieni mashuani, walikataa wote kwani wameambiwa shauri lake baya la siri. Marra akafahamu fitina, naye Mwanga akarudi upesi mjini katika mashua, nao wakarudi kwa miguu

MSIMULIZI. 31

kwani mbali kidogo. Bassi Walinzi wakafika kwanza wakatangaza shauri la mfalme alivyotaka kuwaua burre. Bassi walipatana kumweka mgine mfalme mahali pa Mwanga, Kwanza Walinzi wengi walio Wamasihiya walitaka mtu wao lakini waliozidi kuwa wengi wakamtaka Miwewa, ndiye ndugu mkubwa wake Mwanga, bassi walio Wamasihiya waliacha kumpendelea mtu wao aliyekuwa ndugu mgine wa Mwanga, wakapatana kusayidia kumtawalisha Miwewa. Bassi mji ule mkuu wao Waganda mkubwa sana, watu wakigawanyika, lakini wengi kwa Miwewa, wachache kwa Mwanga, bassi walipigana kidogo akafukuzwa Mwanga akakimbia pwani ukaingia na watu wake, haswa waanawake na watoto, katika mitumbwi mitano tu, lakini mitumbwi ya huko mikubwa sana, bassi akakimbia katika ziwa Nyanza lililo kama bahari kubwa. Marra akaona ameachwa kabisa na mtumbwi mmoja tu, minne wamemkimbia. Bassi akashika njia akafika mahali kwenyi kusini kabisa ya Nyanza panaitwa Magu, naye kama fukara, hana watu, hana fetha; akafungwa na Mwarabu mmoja anakaa kule, akamwandikia yule Padre Bwana Mackay wa C.M.S. aliyefundisha mjini mwake miaka mingi lakini ametoka sasa anafundisha karibu na Magu, akasema Njoo niokoe katika mafungo, sina rafiki yo yote illa wewe.

Bassi nyumaye kule Uganda wakadiriki kumtawalisha Miwewa, naye kesho akafanya baraza akanena Namruhusu killa mtu katika ufalme wangu kushika dini yo yote anayoipenda; akaanza kuwapendelea Wamasihiya na kuwafanya wangine maamiri, hatta katikiro mwenyewe (ndiye wa pili wake katika ufalme) akamfanya Mmasihiya. Wakakaa muda wa juma tatu, bassi Waarabu wa huko wakaanza kuonea uwivu sana mambo hayo hatta siku moja wakaenda barazani na bunduki zao tayari, na watu wanapokiondoka barazani waliwapiga risasi Wamasihiya, na katikiro

MSIMULIZI. 32

wakamua. Mfalme mwenyewe ukanyamaza tu, akaona nikiwakataza wataniua mimi pia. Bassi marra uthia mtupu na machafuko. Waenda kwa nyumba za Mapadre, Waingreza na Wafransa, wakawakamata wakawatia mahali pabaya wakawatendea jeuri wakawachukua mmoja mmoja kuwafungulisha makasha na mali ya mle nyumbani mwao, kiisha huwarudisha pale pabaya. Hayo ya juma moja; kiisha, waliwachukua wakawashuhudisha wakiharibu pia killa kilichomo nyumbani mwao na mwisho wakazitia moto nyumba zenyewe zikateketea.

Kiisha wakawapeleka pwani wakawatia wote na watoto wao katika mtumbwi mmoja wakawashutumu sana, na padre mmoja wakamvulia karibu nguo zake zote. Nao wakapata taabu sana kwani mtumbwi ule ukapinduka na watoto wanne wa Wafransa wakuzama majini, bassi mwisho wakafika kwa shidda sana kwa Bwana Mackay, kama Nov. 10, Naye ndiye aliyeandika habari hii yote kwa Balyozi hapa Unguja. Lakini anaona kama Miwewa hatapata kutawala sana, kwani desturi za Kiganda zamkataza ndugu mkubwa wa mfalme asitawale.

Tena kwa nyuma ameandika habari zayidi tena, kama Waarabu wale walitaka kumwingiza Miwewa katika desturi zote pia za Kiislamu, naye hakutaka, bassi akajaribu kuwatia sumu wasimwuthi, lakini mmoja tu aliyepata kufa. Bassi siku moja akamwita katikiro yake ndio Mwarabu mmoja, na wawili walio wakuu baada yake kama kusemezana pao kwa shauri la siri, marra kwa amri yake watu wakawarukia wale watatu wakawakamata. Miwewa akawaua wale wawili kwa mkuki wake, lakini mtoto wa katikiro akimwona bwanawe anauawa alimpigia mfalme bunduki asimpate, lakini mfalme akakimbia marra na katikiro akafunguliwa akamtia ndugu mwingine wa Mwanga kutawala, anakwitwa Kilema, akaita Waarabu wengi akaenda kumtafuta Miwewa. Naye amekimbia hatta kaburi la

MSIMULIZI. 33

Mtesa babaye, lakini akafukuzwa, na sasa yuko mbali akikusanya watu na majumbe wanaompendelea, na haswa majumbe Wamasihiya, aende kupigana na Waarabu hao waliomtawalisha Kilema. Waarabu wale wawili aliowaua kwa mkuki wake, mmoja ndiye haswa aliyewathuru Wazungu safari hii na kuwaharibia nyumba zao, na wa pili amekuwa yuleyule aliyewafukuza sana Wamasihiya mwaka ule akawachoma ndugu zetu kule wasiokania dini yao. Bassi Uganda sasa vita tupu wala mwisho hautambulikani bado. P.L.J-B.

KURUDI BWANA ASKOFU UNGUJA.

Kwanza alithani Bwana Askofu kupita kwa njia ya kwa Mfalme Kimweri kufika hatta Mvita illi tupate meli tuingie tukaje zetu Unguja.

Bassi tukatoka Magila January 3 na wapagazi wanane kwenda Vuga, tukaenda mwendo wa siku tatu, kwanza siku ya pili tukafika mto Lwengela ndio mto wenyi mamba wengi na wakali pia, siku ile ya tatu tukafika mji wa kwa Sigi, kama saa a pili assubui tukakuta watu wa Pangani wanachunga punda zao na kungoja msafara wao waende Masai, wakajaribu kutufanyia uthia na kututisha, halafu walipoona kama Bwana Askofu haogopi, wakaanza kututia hofu sisi, wakasema tumeamriwa mtu yoyote afuatanaye na Mzungu tumwue illa Mzungu mwenyewe tumwache, hatukuona neno kwani hawana kitu, na sisi tuna bunduki tungeweza kuwapiga, nao watatu tu. Bassi tukaendelea siku hiyohiyo tukafika mji wa Makuyuni kwa jioni ndio ulio karibu Vuga kwa Kimweri, wenyewe wakasema kwanza, Ginsi gani kuja Mzungu huku? sisi tukimwona Mzungu ni nyama tu, twamwua, lakini wao ni rayiya zake Kimweri, tukawaambia kama tumeitwa na Mfalme wenu, hatta mtu mmoja, jina lake akida Huyo, akaleta ushahidi kama kweli ameitwa. Tukakaribishwa mjini tukalala.

MSIMULIZI. 34

Usiku wakaja watu wa Pangani wangine waliotoka kwa Semboja Baba yake Kimweri kutwaa vitu vya Mdoicha alivyonyang'anywa. Nasi tangu hapo tumeambiwa kama Kimweri hayuko kwake amekwenda kupigana vita ya Pare, na Mfalme wao ndiye Kihungwi shemeji yake Kimweri kwani ameoa binti ya Semboja. Wale watu wakatuambia tumetumwa pia kumrudisha huyu Mzungu tukawaambia hatta hamngekuja tungerudi kwa sababu Kimweri hayuko. Hatta assubui siku ya nne na Juma a pili ya Wonyesho tukarudi nao, kwanza wakasema tutawapeleka hatta Magila kwani hatari njiani isiwapate, tukaja nao hatta siku ya tano tukafika mahali pa kugawanyika njia ya Pwani na ya Bonde, hawakukubali kwenda Bonde. Bwana Askofu akataka kawapa zawadi wakakataa kama kidogo wakataka R 150 hakuwapa hatta robo pesa, hapo nikaogopa sana kama watamwua Bwana, kwani nalikuwa peke yangu na mpagazi mmoja, wangine wako mbali kidogo, nao wakasema vikali kwanza, tukatoka tukarudi siku ya sita tukafika Magila. Bwana Askofu akawa hawezi homa.

January 12 tukatoka Misozwe illi kuja Mvita turudi Unguja. Tukapita inchi ya Wadigo, nao walikuwa wangwana sana wakatukaribisha vizuri sana pasipo uthia, tulipofika Vanga tukasikia kama pia twaweza kupita pasipo uthia, tukaingia mjini tukapata chombo kwa R 50 tukaingia, watu wa Vanga walikuwa wema pia. Marra mbili Wadoicha wakatukamata baharini kwa sababu tulikuwa na bunduki. Bassi siku ya sita kutoka Misozwe twalifika Unguja. P.L.

CHUAKA.

Alhamisi baada ya Uzaliwa sisi Waalimu wa Kiungani tulifunga safari na Wazungu kwenda Chuaka na kurudi Juma a mosi, na Chuaka ni kwa pwani ya mashariki ya Unguja kutoka hapa yapata mayili 21. Bassi tulitoka na mapema, tukachukua killa mtu mzigo wake, kwani tulikuwa

MSIMULIZI. 35

sisi watoto kumi na moja na wapagazi wawili na Wazungu watatu. Tulipotoka hapa tukaenda hatta tukafika Mwera baada ya saa ya kwanza tukapumzika katika daraja linalopita kati ya mto Mwera.

Tukashika njia katika mashamba ya mikarafuu mitupu. Tukaanza kuingia katika uwanda wa mawe uliolekea Dunga, tukatoka hapo tukafika njia kuu ya Dunga tukaingia katika nyumba hiyo ya Dunga, tukakaa katika baraza. Na wazee wa hapo wakaleta viti viwili na maji na madafu. Na tena tukawapikia Wazungu chayi nasi pia tukala mikate yetu tuliyochukua. Na tukakaa sana pale kuwangoja wenzetu watatu waliotufuata nyuma wakatufikia baada ya saa sita. Marra pale tukapata habari kama Mr. Geldart anarudi kwenda tena Kiungani tukasikitika sana. Na hawa wenzetu watatu walipokwisha kula tukaondoka pale Dunga. Lakini tulipata habari pale Dunga, kama hamwezi kulala hapa kwani hamkuleta barua, illa kupumzika pumzikeni. Tukatoka pale wote illa Mr. Geldart tukamwacha pale peke yake, hana chakula wala rafiki.

Nasi tukaendelea na kutoka Dunga, tukaanza kuyaona mawe ya ajabu yaliyotuumiza sana, wala punda hakuweza kwenda, kwa ginsi mawe yalivyo mengi. Na halafu yake tukaendelea hatta tukaachana wangine wakapita njia ingine, nasi watu watatu tukaongoza njia yetu na Martin Furahani, na watu wengi tukawakuta wamechukua samaki watokao huko Chuaka, nao wakatuambia kama tutaona kisima mbele yetu na tutaendelea katika mashamba yaliyolimwa katika mawe na tutatelemkia mjini. Nayo ni kweli, tukaenda tukafika kisimani tukanywa maji, na baadaye tukaendelea tukayaona hayo mashamba yaliyolimwa kama mwambani, na vyakula vinaota sana katika hayo mawe tukastaajabu sana, na katika hayo mashamba yamepandwa mahindi na pilipili tele na mapapai na ufuta. Na halafu tukaingia mjini, na minazi mingi ipo, na hori yake pia na mji wenyewe

MSIMULIZI. 36

kama mji wa Lindi. Na watu wake halisi wote kazi zao ni kufanya majuya ya samaki. Bassi tukamwendea Jumbe atupe maliali pa kulala. Akakataa, akisema, wapi barua ya Sayidi, kwani tumeambiwa naye kama killa Mzungu ajaye kuko msimkaribishe, billa kwa barua yangu. Nasi tukamwambia Hawa ni Waingereza wala si Wadoicha. Akasema, Sayidi amesema kama Mzungu aliye yote asikaribishwe. Hatuwezi kuwapa mahali pa kulala, illa nendeni mkalale huko pwani mchangani; na tuliomwendea huyo Jumbe ni mimi, Herbert Martin Feruzi na Cyprian Lizani. Bassi tukaenda tukawaambia Wazungu, nao wakasikitika sana, bassi tukalala mchangani tukapika chakula chetu, na kitoweo ndio ndege sita aliowapiga Mr. Travers. Watu wote wa mjini wala hawaji kuongea nasi illa mtu mmoja tu aliyetuazima chungu kupikia huyo tu bassi. Na assubui tukapika chakula chetu na cha Wazungu pia nao. Walipokwisha kula wakatangulia kurudi nasi tukangoja chakula chetu kiwive, na baada ya kutoka hawa Mr. Geldart tuliyemwacha Dunga akaja na mtoto wa Dunga jina lake Kilima. Na Martin Furahuni akatwaa bunduki ya Mr. Travers akaenda kupika ndege, (kwani ndege wengi wako huko) lakini hakumpata hatta mmoja. Na tulipokwisha kula tukatoka tukasumbuka sana vilevile kwa mawe. Hatta tukafika Dunga, napo pia tukafukuzwa, na Mr. Geldart akawaambia, kama, Mkitufukuza saa hizi za jioni tutakwenda mwambia Balyozi yakafike hatta kwa Sayidi, Nao wakamwendea bibi yao kumwambia, hakukubali, ya pili pia, na ya tatu pia, hatta halafu tukaambiwa Haya laleni. Lakini manokoa wangine wakasema, Hapana, hamtalala hapa, kwani hamkuleta barua ya Sayidi, hatta ukawa ugomvi wao kwa wao, kwani mmoja akatuambia kama laleni, naye ndiye aliyetukaribisha, lakini manokoa wangine wakaona uwivu, (kwani walisikia kama tumempa zawadi) hatta wakawa tayari kupigana, halafu yakatulia,

MSIMULIZI. 37

tukalala. Na assubui tukatoka hatta tukafika Mwera tukapika tukala, na halafu yake Wazungu wakatangulia wakatuacha tunakula, naswi tukafuata nyuma, hatta kufika hapa petu Kiinua Miguu. Bassi baada ya siku Balyozi akamwambia Sayidi walivyotutendea, akamwita Jumbe wa Chuaka na wazee wangine wakaja hatta Kiungani kutuungamia kama walitushutumu, bassi tulifanya baraza Wazungu na sisi Waalimu, na wakiisha kuungama walivyotutendea vibaya na kututupa pwani, tuliwakaribisha kwa heshima wakanywa sherbeti na biskwiti tukawaonyesha nyumba yetu yote tukawaaga kwa amani. Hivi tukawatendea mema kwa mabaya yao. Y.B.A.

HABARI ZA MASASI.

Lile kanisa letu lililoungua moto limejengwa tena sasa na limekuwa zuri kuliko kwanza na kupita si zayidi kamwe, waina kuingia tunangojea Uzaliwa.

Bassi jana walikwenda kwenyi 'kisango kulondola,' ndio kupiga bao. Bassi watu wote wa mfalme Kumbemba, na wenyi kisango chao wakasema, sharti nyumba zilizojengwa wakati ilipokunya mvua ya kwanza zibomolewe zote.

Illakini sharti tena kanisa na nyumba kubwa za mwaka huu za petu nazo zibomolewe pia udongo wote, ao mvua itakunya siku moja, itaacha tu isinye tena.

Bassi nalisikitika kwa hayo, illakini inakunya sasa hiyo mvua, na watu wanapiga vigelegele.

Habari za Machemba na Nahua (Satia). Mzee Matola na Barnaba Nakaam wanajaribu kuwapatanisha, illa Nahua anasema kukataa sikatai illa mnipe kwanza mwanangu aliyechukuliwa katika vita ya kwanza yao. Bassi wao wanamjibu Nahua, Kama wewe wataka mwanao, je, mwenzio Machemba akinena Nawe nipe waliouawa na Magwangwara, je, nawe utalipa? Bassi usihitajie malipo, lakini mpatane

tu, lakini bado hawajapatana.

Na habari za Machemba, yeye mwenyewe mwema, illakini watu wake naona kama chui aliyenyang'anywa waanawe. Siku zote tayari kwenda inchi ya mbali kuiba watu, na kuwanyang'anya mali yao, hatta safari hii iliyorudi pwani kama mwezi wa Nov. 1888 wamewaona na watu wetu wa hapa Masasi akina Machemba wanaingiza mateka waliokwenda kuwaiba inchi ingine. P.K.

HABARI ZA MISOZWE.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Misozwe sasa iko katika kujengwa, yajengwa nyumba ya Padre Mr Woodward nayo ya matofali, watu wengi wafanyao matofali. Sasa yeye na Mr Wride wanarudi hapa Misozwe wametoka Magila.

Decembcr 4 twalikwenda kwa Jumbe mmoja aliye karibu yetu hapa aitwa Makange; tulienda kumsalimia kwani hatujaonana naye kwa siku nyingi tangu kuondoka kwake kwenda juu Mgambo kumsayidia nduguye Kibanga katika vita ya Kimweri ya mwaka wa jana. Ajabu moja tulisikia kule ndio, Mpale mmoja ana mbuzi wake, na mbuzi huyo hali majani, illa nyama ya kuku, mbuzi, na ng'ombe, achinjiwa kuku, apewa, ndicho chakula chake. Huyo Mpale yupo hapa karibu na Misozwe lakini hatukumwona jana alimwacha mjini anakokaa mwenyewe si mbali, karibu na mji uitwao Kumba, nasi tunatumaini kwenda siku nyingine kumtazama tuone hakika yake, na huyo mtu jina lake Magili. H.N.

HABARI ZA SHAMBA LA MBWENI.

Siku kuu za Uzaliwa tunaona hapana pahali palipostawi kupita huku Mbweni. Kwa ngoma, kwani Bwana Mr Wallis aliwapa watu wa shamba ruhusa ya kucheza ngoma muda wa siku tatu, illa jambo moja alikataza ndiyo kucheza

MSIMULIZI. 39
usiku. Tena katika siku hizo tatu walipewa mapesa yao kama walivyokuwa wakipewa Walipokuwa wakifanya kazi. Watu tangu waume hatta waanawake wa shamba walikula tende hatta iliwashinda. Mashindano ya kuvutana kamba waanaume upande na wake upande, kushindana kwa kukimbia kwa visibao; ah, mchezo mwingi uliokuwapo siku hiyo. Hatta watu wa shamba wananena tangu kutekwa kwao hawajapata siku kuu ya Kuzaliwa Bwana wetu kama hii.

Pana tena habari inayompasa kwa mtu wa zamani aliyekuwa akikaa Kiungani, ndugu yetu Hallal Chosi. Amefariki. Tazameni Mwenyiezi Muungu hakupenda afie inchi za makafiri. Kama mjuavyo alikuwa Pangani, na hapo Pangani karibu angalikufa, illa Muungu amependa aje azikwe hapa Mbweni. Tena pana mtu mmoja aliyekuwa Kiungani zamani sana Ali Katio, naye amekufa hapa.

Na habari kidogo ni hii, mkewe Henry Nasibu ana mtoto naye amebatizwa jina lake Edward Steere, na Kathleen ana mtoto mwanamke, naye amebatizwa jina lake Faith Difflis. G.K.

HABARI ZA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. January 3 lilikuwapo duka la watu weusi, lakini Wazungu waliuza ghali vitu vingine, viliuzwa kwa rupia nyingi, walikuja watoto wa Kiungani na Mkunazini. Siku ya Kuzaliwa Bwana wetu ilistawi sana, tuliamka saa kumi na moja za Assubuhi tukaanza kuimba 'Christmas Carols,' Siku ya Stefano, tulikwenda Mbuyuni kushinda sisi 83 pamoja na Wazungu 16 jumla tulikuwa 99. Alhamisi tulikwenda kucheza njia kuu, yalikuwapo mashindano, walioshinda walikuwa watu saba ao wanane, na katika waanawake tano ao sita. Kurudi kwake Miss Thackeray na Faith, wamefika

MSIMULIZI. 40

Zanzibar January 20 kwanza walifikia Mkunazini, watoto 32 walikwenda kumtwaa pamoja na Bibi Miss Bennett, chumba chake kilipambwa vizuri sana, alipofika hapa killa mtoto alifurahi sana, hatta Miss Berkeley alifurahi mno, hatta akacheza pamoja na watoto.

Lilikuwa kusanyiko la Chama ya Mchunga Mwema, Feb. 1, tulikuwa watu 16.

Meli hii Baba yetu mpendwa ametuletea barua sisi watoto wake pamoja na Wazungu wote waliopo hapa, ametuambia alifika Yerusalemi na habari zake zote ametueleza. M.M,

HABARI ZA NEWALA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Habari za Newala siku hizi ni njema.

Siku kuu ya Kuzaliwa tulipata furaha tele, kwanza jioni Juma ya tatu wakabatizwa watoto hawa wa nyumbani, Tomaso Juma, Harun Bukin, Yona Selenje, Chembini Masaninga, Benito Nyalila, Siluano Malinjila, Habil Malaya. Juma a nne wafalme kumi na wawili na watu walikusanyika, yakawa mashindano ya kupiga bunduki kwa shabaa, halafu tulikwenda mpilani kwa mashindano ya watoto, kukimbia, kuruka, kutupa risasi, na kuvuta kamba; tulipewa vitambaa vizuri vya Ulaya sisi tulioshinda. Jioni zilikuwa sanamu za faa, watu, wengi wakaja kuzitazama na wasafiri wa Mtonya wakastaajabu mno. Watoto wa Chitangali wakaja na watoto wa nje, watoto wa nje wakalala nyumbani siku ile wote pamoja, labuda sabwini ama themanini.

Siku hizi Mwalimu Joseph hawezi. Hakuingia chuoni kwa siku nyingi wala kutembea. Mwaka huu mvua tele, tumepanda miembe mingi na mbegu zingine. Juzi Bwana Porter alichukua sanamu za taa Makonde kuwaonyesha watu huko. C.M.

MSIMULIZI. 41

YERUSALEMI YA LEO.

Siku hizi Archdeacon Hodgson amekwenda Uingreza, lakini njiani amekwenda Yerusalemi, akaandika habari yake yote hiviâ Siku kuu ya Uzaliwa, 1888.

Leo nikiwapo mwilini baharini karibu na Smurna, rohoni nipo nanyi Mbweni; hivi nimeona sina buddi nianze leo barua ya kuwaeleza wote habari za safari zangu, na kuwapelekea salamu zangu za siku kuu. Nalikumbuka sana assubuhi leo nyimbo zote za Uzaliwa mnazoimba leo Mbweni, na marra nyingi nimetamani kuwapo tena kati ya watoto wangu wote.

Bassi safari yangu, nimesafiri sana wakati huu. Tangu nilipotoka merikebu ya Kifransa huko Port Said, kwanza naliogopa safari yangu ingaliharibika kwa kukawia mno huko. Nalifika Dec 7, nikapata habari njema za bibi yangu na Richardi, lakini Jumaa, ina Juma a mosi, Juma a pili, Juma a tatu, hapana merikebu ya kwenda Yaffa mpaka Juma a 'nne tu nikapata kutweka. Wala Port Said si mahali pazuri pa kukawilia hatta kidogo. Bassi Juma a tano assubuhi tukafika Yaffa, nikapata furaha ya kuona milima ya Inchi Takatifu ya Uyahudi. Kwanza tukaona hofu tusiweze kushuka Yaffa, kwani mawimbi huko hufanya uthia sana wala bandari si nzuri. Tukajaliwa lakini tukashuka kwa shidda kidogo na kwa makelele mengi. Ee furaha gani niliyokuwa nayo kuingia inchi ya Bwana yetu; na mji huu wa Yaffa, mtakumbuka, ulikuwa alikotoka nabii Yunas, safari ile ya kuasi, tena alikofanya mtume Petro mwujiza wa kumfufusha Tabitha wakati ule ule alipopewa matokeo yake ya ajabu ya kumwonyesha asiogope kuwahubiria mataifa Anjili. Hatta sasa huonyesha

MSIMULIZI. 42

hapa nyumba ya Siman mfua ngozi alipokaa Petro siku zile.

Bassi nikiisha kushuka nalikwenda kwa Mr Hale Kasisi mmoja wa C.M.S., nipate kufanya mashauri, na kuacha masanduku yangu kwake. Tena akaniambia, Yuko hapa umbu wa Sayidi wa Unguja anajitafutia nyumba, nalistaajabu, lakini sikupata kumwona. Sikukawia Yaffa, saa mbili tu nikaingia garini nipate kufika Yerusalemi siku ile ile. Kwenda kwake mayili 38, lakini njia, isipokuwa marra kwa marra, njema sana. Nikasafiri pamoja na mwalimu mmoja anayefundisha Wayahudi huko Yerusalemi, gari moja. Tukaenda tukaenda mchana wote. Kwanza kupita inchi sawa ya Sharon halafu kupanda milima ya Uyahudi, tukapita Ludda, kwenyi Petro alipomponya Ainea, na Boonde la Ayalon, Isa wa Nun aliposimamisha jua, na Ela, kwenyi mapigano ya Golia, tukakiona kijito Daud alikookota mawe matano. Marra kwa marra tukashuka garini tukaenda kwa miguu, frasi wetu watatu, lakini milima mirefu sana jua likachwa ikawa giza. Yerusalemi bado mbali. Mbele ya mlima wa mwisho ikiwa bado safari ya zayidi ya saa uzima Wazungu wawili waliopanda punda wakaja kumlaki mwenzangu nikakaribishwa kupanda punda nikatangulia pamoja na mmoja wao, hivi tukafika mapema kama saa pili ao saa tatu ya usiku. Nalikaribishwa na Kasisi mwingine rafiki ya Mr Hale, anayo nyumba nje ya Yerusalemi karibu na mlango wa njia ya Yaffa, jina lake, Mr Zellen, nikakaa nyumbani kwake siku zote nilipokuwako Yerusalemi ndio Juma a tano usiku hatta Juma a mosi assubuhi.

Nalifika usiku, bassi keshoye tu nikaanza kutazama. Wakati wa baridi lakini si mno, na siku nzuri, bassi kwanza kutembea kwangu nikaenda kwa miguu hatta Betlehemu, kutoka Yerusalemi mpaka Betlehemu sawa na kutoka mjini mpaka Chukwani. Mji wa Yerusalemi ukaonekana mzuri

sana nilipokuwa nikipanda milima ya njia ile. Njia yenyewe nzuri lakini pande zote za huko milima mitupu, mawe mengi, hapana miti hatta kidogo na majani haba. Kwa saa mbili nikafika Betlehemu. Kwanza naliona boonde alipookota Ruth nafaka yake Boaz zamani, na milima Daud alipowatunza kondoo za baba ya Yesse, hatta walipowatunza kondoo zao wachungaji wangineo usiku ule alipozaliwa Mwana wa Daudi aliye Masiya mkuu. Halafu nikapita kaburi lake Rahel mkewe mpenzi Yakob: hatimaye nikapanda mwingine nikafika Betlehemu. Bado ni kijiji kidogo tu illa watu wake wengi. Liko kanisa kubwa la zamani, husema Helena mkewe Konstantino aliyelijenga kanisa hili la anasa, tena chini ya mathbahu limeshuka paangoni, huonyesha mahali alipozaliwa Isa Masiya na malisho alimotiwa na mamaye Maryamu. Bassi nikaenda kutazama nikazunguka mji, nikarudi, nikafika Yerusalemi tena saa saba.

Nussu iliyosalia ya barua hii itatiwa katika Msimulizi ijayo. Mwezi huu hatuna nafasi. Mtg.

HABARI ZA MAGILA.

Tumesikia kama watu 70 walifanywa waanafunzi katika Juma a pili ya tatu baada ya Wonyesho, waume 45, waanawake 25. Lakini Mletaji hakutuletea habari ngine safari hii.

HABARI ZA NYASSA.

Anaandika Augustin Ambali, kwenyi Dec. 9, anasema kama William na Denys wanafundisha sana pale mtoni Shire ilipokwama "Charles Jansen." Yeye Augustin anatwaa mashua ndogo huenda mtoni kijiji kwa kijiji killa pahali mpaka Matope na kurudi. Tena mkewe ana watoto Waanawake yapata 26 chuoni. Na Aruffo yuko Matope bado akifundisha, na mkewe ana watoto waanawake yapata 22 chuoni. Na kule kwenyi "Charles Jansen" wanapofundisha Denys na William watoto wengi sana

MSIMULIZI. 44

wanakuja kufundishwa, na Mfalme wa huko amekubali wajenge nyumba ya chuoni, kwani alikataa kwanza akiwashuku. Na mabibi wawili wamefika Lukoma, ndugu ya Mr. Woodward na bibi mgeni daktari.

HABARI ZA MKUNAZINI.

Siku kuu ya Kuzaliwa hapa petu tukacheza, hatukuenda kazini mpaka Juma a tano, tukafanyiwa karamu na Miss Mills na Miss Shaw, sharbati, akatoa mali mengi sana, tukapika tukala athuuri tukamwita yeye aje atutazame, Alhamisi tukaitwa Mbweni peke yetu na Miss Woodward, tukafanyiwa karamu tukala.

Tena sisi huku mjini tumefiwa na Mzungu mmoja jina lake Mr Coombe, alikuwa hawezi homa, ilimwanza siku ya Juma a mosi jioni tuliporudi mpilani. Na Mr Bishop amerudi sasa Mkunazini, na Luke W. Kumi amerudi tena hapa.

HABARI ZA KIUNGANI.

January 1888 palikuwa kutazamiwa darasa nne 'Eiamination,' na waliotazamia ni Mr Geldart na Mr Travers darasa ya kwanza na ya pili, na Mr Jones-Bateman ametazamia darasa ya tatu na ya nne, walitazamiwa muda wa siku tatu.

Na walioshinda katika darasa ya kwanza ni 1. John B. Mdoe, 2, Yohana B. Abudallah, 3. Hugh Mhina 4. Martin Furahani, na katika darasa ya pili 1. Constantine Mgoma, 2. Arthur Mvenya, 3. Edward Nyongo. Na darasa ya tatu 1. A. Semmanyi, na 2. Y. Mgonea, na katika ya nne walioshinda ndio 1. M. Meweawa, 2. Y. Sonjo. Tena Hugh S. Mtoka hakuwamo katika 'Examination' hii, sababu alikuwa hawezi. Tena pana Padre mmoja aliyekaa hapa zamani halafu akaenda zake Ulaya kwa ugonjwa, na baada ya miaka minne ameturudia tena hapa nasi tumefurahi mno kumwona amerejea tena,

MSIMULIZI. 45

naye jina lake Mr Travers, hatta baada ya siku chache akawa hawezi tena, bassi na iliyokuwa imebaki ni kurudi tena Ulaya, bassi meli hii ya juzi amerejea kwao. Dec. 1888 Mr Jones Bateman alikwenda Mbweni pamoja na Martin Furahani na Yohana B. Abdallah, kuwafanyia watoto wa Mbweni 'Examination' na Martin na Yohana waliwatazamia darasa ya tatu na 'Half Timers.' Kanisa letu juma hii litaisha kabisa kujengwa, nje ndio linapakwa chokaa, naswi tunafurahiwa sababu sasa tunalitumia na lina nafasi nyingi kuliko la zamani. Mwezi huu Gray Feruzi, Martin Zanga na Mattayo Lamilako wametiwa katika kazi ya kupiga chapa. Tena Gilbert Matengwe ameingizwa katika kazi ya upishi; na Nicholas Kusi kwanza alikuwa akipiga chapa, lakini sasa anatumaini i kazi ya kufundisha, bassi sasa amerudia chuoni tena. Katika juma hii watoto kumi na mbili watatiwa mikono, Gray Feruzi, Julius Mkwaya, Mackenzie Meweawa, Barnaba Mtaula, Andrea Andani, Martin Zanga, Selwyn Ukolo, Tomaso Asuadi, Nutter Kiwazi, Henry Msopola, Yohana Sonjo na Billy Swedi.

Tena katika safari ya Bwana Askofu akienda inchi ya Bonde pamoja na Mr Geldart, atawachukua waalimu wawili pamoja naye, Philip Yahom, Herbert M. Feruzi, na Philip ataenda kukaa Misozwe kumsayidia Henry Nasibu kuundisha, na Herbert ataenenda kukaa Magila kufundisha mahali pa Manfred Manyula kwani Manfred sasa anarejea Kiungani kusoma tena.

Katika mwezi wa December 1888, Mr Muxworthy aliwakarimia sana watoto wa Kiungani aliwaita katika shamba lake kubwa sana lenyi matunda mengi na miwa mingi sana, akawaambia waile wawezavyo, bassi marra moja miwa ililala chini thoruba moja kama mbele ya upepo, wakaila hatta ikawashinda.

Tunataka sana majina ya Waletaji habari na watakao Msimulizi wa Magila, Umba, Mkuzi, na Nyassa. Mtg.

MSIMULIZI. April, 1889. IV.
Imepigwa chapa Kiungani, Zanzibar,
katika "Universities' Mission to Central Africa."

HABARI ZA MADACHI.

Hakika uthia sana pwani ya Mlima, tena itazidi, kwani Madachi wanaleta karibu askari, watu weusi, nao ndio Wasudani wa Misri, kuwapigania juu ya Waarabu walio katika miji ya pwani. Itakuwa vita kali sana, lakini Madachi watashinda hawana buddi, kwani hodari mno kwa vita, na wenyi bunduki zenyi risasi nyingi nyingi, na mizinga ya nguvu, watakaa katika miji ile ya pwani ya Mlima, hawaondoki tena. Waarabu watakasirika sana, uthia utaenea barani.

Na mimi naona shaka kwa mambo haya, yafaa sana Waarabu waondolewe kwa maana biashara ya utumwa ikome pia. Hatta makabila yote ya barra wangetaka kuwaondolea mbali hao Waarabu kama wakijua ndio waharibuo inchi, na watu pia. Lakini nathani Madachi hawawezi kuwaondoa Waarabu wote pia, illa labda pwani tu, kwani watawakasiri sana. Ndio mashaka na hatari nyingi kwa ndugu zetu pote bara.

Lakini mambo mawili nayajua mimi, ndio haya, la kwanza, Yote haya yatatokea vema kwao wampendao Muungu; la pili, Sisi Wamasihiya kazi yetu tupendane na wote, hatta na Waarabu na Madachi.

Lakini angalia, hali ya Madachi sasa pande hizi za Unguja imegeuka sasa. Kwani walikuwa, wale wa kwanza watu wa biashara tu wakafanya ujinga wao na fithuli kamwe hatta wakaambiwa na waziri mkuu Bismark, "Ndinyi wajinga." Bassi sasa mtu anakuja, ametoka kwa Kaisari wao, ameamriwa na kabila lote la Madachi aje awapige Waarabu na awatawale Madachi wale wa biashara nao. Naona hawataachiwa tena kufanya ugomvi na fitina kama kwanza. Vita hii haina fayida kwa Madachi; hawapati hatta robo pesa, mpaka watu wote watulie, wakatake biashara. Bassi afathali vita ifanyike upesi, iishe upesi. A.C.M.

MSIMULIZI. 47

Imepita juma mbili Madachi walitaka kuwarudi watu wa Saadani kwa kuwapiga na bunduki, bassi wakarudi wakaupigia mji wa Saadani mizinga elfu na mia 'nne, kumbe walipohesabu jumla yao waliouawa wakakuta hapana, watu wamehama na mapema, na waliopata kumwua ni mbwa mmoja tu!

Huyu mkuu wa vita ya Madachi amefika, jina lake Captain Weismann, lakini hapigani kwanza, anayangojea masika yaishe.

HABARI ZAO WALIOKAMATWA KIPUMBWI.

Misozwe, March 21, 1889

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi Salaamu. Siku ya l0 ya March Juma a pili assubuhi chombo kikawa tayari, tukaenda na vitu nussu pwani, tulipofika tukaipakia mizigo yetu katika mashua, tukaambiwa tupitie njia ya juu, kwani sasa ni kaskazi tutabisha sana, bassi mkewe mwalimu Henry, na mke wa James Mwaimu na yeye mwenyewe, na Maryamu Swedi, na Augustine Amani na mkewe, na John B. Mdoe na wangine, wakapita njia ya juu, illa mimi Philip E. Yahom nikaingia chomboni kuangalia vitu, haya tukatweka, na jahazi hilo linakwenda sana, tukashika njia ya Bawe, tukaona mashua mbili za matanga za Mwingereza, ikaja moja tukasikia, Tua, tukatua, akaingia mkalimani, akaulizauliza akaisha, akaandika katika kikaratasi kidogo maneno ya kumwonyesha Dachi akija, Tukachapa wee, hatta athuuri matlai ilivuma vibaya, bahari ikaanza kuchafuka sana, hatta chombo chetu kikatupwa huku na huku na jua kali sana hatta alasiri tukaingia katika bandari ya Mwanda, tukatia nanga, na wenzangu bado kufika, wakafika Mwanda saa pili ya usiku, wakalala bandani pwani, napo pana vidudu vidogodogo, vinauma sana vikawauthi sana; Juma a tatu March 11. assubuhi nami pia nikashuka pwani, hatta saa sita tukaingia chomboni wote, watu wengi,

MSIMULIZI. 48

Wanaake wakaingia chini, ndani mlikuwa na jamvi limetandikwa, juu yake umetiwa mchanga vizuri, ndipo walipolala wanaake, sisi tukakaa juu ya kibanda. Nahotha akasema Tusiende mpaka Pangani illa tufike Kipumbwi ndipo pazuri, baharia wakamwambia Siyo, yafaa tuende Pangani kwani hakuna hatari, nahotha hakuwasikia, tukaenda huko Kipumbwi, tukafika jioni kama saa moja kassi robo, kufika tu wakatokea watu wakasema, Kwanini kushukia hapo, sisi hatutaki watu washukie hapa, bassi leo msishuke, wakasema, Nahotha wa Kigunya ruhusa ashuke pamoja na kizee kimoja cha hapo, wakashuka, yule kizee akawaambia mle mna abiria waendao Bonde, watu wakawauliza, Mna wanaake? wakajibu Wamo, wale watu wa pwani wakasema na washuke baharia watatu waje kulala huku, na wakatua tanga wakalishusha illi tusipate kutoka kwenda Pangani, mkubwa wao akasema, Nipeni rupia mbili kesho maneno haya nitayatengeneza nitauisha pia na uthia huu, zikatolewa rupia mbili, kama saa sita ya usiku akaja baharia chomboni kwa ngalawa, akasema, Wanaake na washushwe sasa, wakashushwa pamoja na mabahasha yao, wakakaribishwa nyumbani, hatta assubuhi tukaambiwa abiria wote washuke tukashuka pwani, wakataka watu wenyi wake wale walio nyumbani, wakaenda James na A. Amani, James akavulishwa kisibao chake cha kwapa; wakaangalia wakaona rupia thelitashara ndani, wakazitwaa, nazo ni zetu, saba za nauli yetu, na sita za chakula. Wakashikwa shikwa na kuwasukuma, wakisema watumwa wetu hao. Bassi James akashikwa na mtu anampeleka huko juu akasema, mtumwa wangu huyu, akaja mwingine akasema, mtumwa wetu wote huyu, watu wengi wakaja hapo, James akajaribu kusema nao, nao wakawapeleka majumbani. Sisi abiria tulikuwa pwani tumesimama, tukaambiwa tuende zetu tukashika njia ya juu, tukatoka hapo saa mbili assubuhi hatta athuuri kamili tukawasili Pangani. Alasiri akatokea James na mkewe na A. Amani, kufika

MSIMULIZI. 49

tu katika nyumba ya Mission, (kwani ndimo tulimokaa) tukawauliza, Jee! wangine wako wapi? wakasema, Hao wangine hawatoki illa ziende $25, tukawauliza, nyinyi jee mmepataje kutoka? wakatujibu hivi, Kwa sababu watu wa pale ni wengi sana Wabondei, bassi wamemjua James na mkewe wakawaachia, na A. Amani kwa sababu naona ni mwanamume, tukauliza, Jee hao wangine? wakasema, Hao wangine tukawajua nao ni Wabondei, nao wakasema, Maryamu ni mzalia, wakamwambia kama Mbondei wewe, ebu sema Kibondei, akisema, humcheka, Wasikia, ndiye mzalia, ndiye, siye hatta Mbondei. Bassi wamefungwa sio katika gereza illa wamezuiwa tu wasitoke mjini.

Bassi sisi tukamwambia Mafutaha anayengojea nyumba ya Mission, akatoka yeye na A. Amani kwenda kwa liwali kumwambia. Liwali akaandika barua yake akawapa akasema, mpeleke assubuhi, siku ya Juma a tano March 13, ikapelekwa barua ya Liwali kwa mikono ya James na A. Amani, barua ikasomwa, wote wakakubali kuwaachia na kulipa vitu walivyotwaa, illa Mwarabu aliyemtwaa Maryama akasema, Waacheni wenu, lakini huyu wangu simwachi labuda waje waniue, yakawa maneno mengi, hatta wakawaambia James na A. Amani, na nyinyi pia tutawafungeni pamoja. Wakaenda kuwaangalia wale wanaake wakawakuta wanapika, kiisha wakaenda zao pasipo kuwaaga, wasijue kama wanaenda Pangani.

Wakatoka usiku, Alhamisi wakafika Pangani, wakaenda kumwambia Litfali, akasema Kaeni nitampeleka askari. Nasi tukaandika barua iende Mkuzi na Magila kuwaambia habari hizi, na tena chakula hapana illa mimi nalikuwa na R 2,5 tukazitumia. Yule askari akafika Kipumbwi akawapa barua ile ya Liwali wakaitwa wakamfukuza wakamwambia, Sisi hatumjui Liwali, bassi rudi kwako wala sisi tusikuone tena, akaja kwa Liwali jioni wale baharia wakafanya uthia kwa nauli yao, tukawaambia hatuna fetha hatta moja ya

MSIMULIZI. 50

kuwalipeni, wakasema kopeni kwa watu ao kwa Wahindi, ao wekeni rahani kitu, James akataka kuweka rahani joho la reale tano, lakini Banyani hakulikubali, wakasema aongeze kitu kingine tena juu yake, lakini James akasema yafaa tuende kwa Liwali, tukaenda kwa Liwali pamoja na Mafutaha, yeye akasema na Liwali; Liwali akasema akawaambia baharia wale, kama ngojeni mpaka kesho wakirudi askari niliowapeleka Kipumbwi pamoja na hao wanaake. Tena Liwali akatuambia heri mpunguke kwani labuda yatakuwa matata mangine, usiku wa Alhamisi akatoka mke wa James na Salimini kijana anayekuja kujenga Pangani. Assubuhi Jumaa March, 15 saa mbili mimi na John Mdoe tukatoka, hatta karibu na Mgambo tukamkuta Mwalimu John wa Mkuzi kachukua bunduki yake, yeye na msimamizi wa Magila wanakwenda Pangani, tukaja hatta alasiri saa kenda tukawasili Mkuzi, hapana mtoto wa Mission hatta mmoja hatukumwona, mke wa Mwalimu mkubwa akatukaribisha. Juma apili tukatoka tukafika siku ile ile ya March 17, tukamkuta Rev. Mr. Woodward, akaniambia, kesho Juma a tatu twende zetu Misozwe, kwani Mwalimu Henry anakwenda leo Pangani, Juma a tatu tukatoka saa kumi, tukafika hapa usiku kama saa moja. Juma a nne, mimi Philip nikaanza kufundisha, na Jumaa Askofu alitia watu mikono, watu watano, wanaake wawili, Elizabeth na Kristina, na wanaume Daud Semfungo, na Robert Kapala, na James Mwaimu wa hapa.

Tena tumehadithiwa hivi na mwalimu John Swedi kama aliposikia hao wenzetu watatu wamo mikononi mwa watu huko Kipumbwi, akatumwa na Askofu yeye na Mhammedi msimamizi wa Magila hatta wakawasili Pangani hatta kwa Liwali wakampa khati ya kuwaacha, wallakini hao watu wakakataa kabisa kuwaacha, billa wapewe hizo reale hamsi u asharini, na sisi hapa Unguja tulipata barua ya Sayid Khalifa aliyomwandikia Liwali wa Pangani,

MSIMULIZI 51
kusema sharti waachwe, lakini Waarabu wa Kipumbwi hawakusikia; mwisho wakapatana nao kwa reale hamstashara tu, na aliyewakomboa ni John Swedi, Henry Nasibu na James Mwaimu, na watu waliokamatwa ni hawa, mkewe Henry Nasibu, na kitoto chake kidogo, mkewe Augustine Amani, na Maryamu mtoto wa mwalimu John wa Mkuzi. Na Mama mtoto alipopata habari alikuwa akilia kwa huzuni ya mwanawe. Lakini halafu wakarudishwa salama salimini. P.E.Y. na J.S.

HABARI ZA YERUSALEMI YA SASA.
(nussu ya pili)

Ndipo nikaenda kumtafuta Balyozi Mfransa, M. Le Doux, ndiye yule yule aliyekaa Unguja zamani mwenyi mtoto aliyejua Kiunguja tu, sikumpata wala bibiye, lakini Daktari aliyekaa Unguja sana nikampata nikakaa kidogo kwake, Dr Gregory, illa sasa huitwa Dr Arbela. Alasiri siku ile ile nikaingia mjini nikapenya hatta upande wa pili nikatazama moskiti mkubwa mzuri wa ajabu, usimamao mahali pa hekalu la zamani. Katikati yake uko mwamba mkubwa wa zamani, ndio mwamba wa mathbahu ya kafara ya hekaluni. Kwanza ulikuwako hapa mlima Moria, sasa kwa maanguko yote kama sakafu moja sawasawa, na juu yake miskiti miwili, wa kwanza wa Omar, umeviringana, wa pili E1 Aksa mkubwa sana, urefu kupita Kanisa la Mkunazini marra mbili tatu. Bassi hapa kwenyi lililokuwako kwanza Hekalu la Sulemani, nalo la Zerubbabel, na majengo yote ya Herode, sasa moskiti ya Kiislamu tu.

Halafu nikarudi nikaenda kutazama kanisa kubwa la Kimasihiya linakwitwa la Kaburi Takatifu kwani huko hutuonyesha mahali pa Kusulibiwa, na mahali pa Kaburi: Ni kama vyumba vingi vimekusanyika kufanya kanisa moja kubwa sana, vingine kama mapango yote yenyi taa na mathbahu. Halafu nikatoka nikapanda mlima wa upande

MSIMULIZI 52

wa pili wa mji ndio mlima Sayuni, nikatoka kwa mlango wa Daud kiisha nikapita kwa makaburi mengi sana nikafika kwa rafiki zangu.

Keshoye, masikini mimi, ikanya mvua nikaenda assubuhi kutazama zile sanamu za hekalu alizowafasiria Mr Woodward alipokuwako Mbweni mwaka jana. Baada ya athuuri tena nikaenda kuzunguka sana peke yangu. Nikapita katikati ya mji Mtakatifu nikaenda kutazama kwenyi hululiapo Wayahudi. Uko ukuta mmoja uliojengwa mawe makubwa sana, nao Wayahudi husema Ndiyo mawe ya hekalu la Sulemani, bassi huja killa Jumaa alasiri hulia huomboleza sana nyuso zao kwa hayo mawe, nikafika Jumaa alasiri nikaona mahali, lakini hapana waliao, nikaambiwa, wamekwenda zao labuda sababu ya mvua, nikaendelea nikatoka kwa mlango mdogo (Mlango wa simadi, Neh. II. 18.) nikashuka ndani ya boonde ya kijito Kidron, maji yake haba. Mbele yangu upande wa pili uko Mlima wa Zeituni hatta nussu ya kupanda kwake mizeituni, ndipo ilipokuwako zamani Gethsemane, nikatembea humo kwenyi alipoona juhudi ile ya ajabu Bwana wetu, nikachuma majani kidogo ya miti nikazidi kupanda. Njia niliyopandia ndiyo njia ile ya Daud, alipokimbia mbele ya Absalome, njia ndogo mbaya sana, nikafika upesi lakini juu ya mlima wa Zeituni uko sasa juu yake mnara wa kanisa mrefu sana, hupanda ndani madaraja 270. Nikapanda hatta juu kabisa inchi yote huonekana sana mvua tu imenizuia nisione Bahari ya Chumvi na Yardani, nikaona milima ya Moab ng'ambo yake, tena karibu chini iko njia ya Yeriko na Betania. Mnara huu huonyesha mahali wathaniapo Masiya alipaa mbinguni. Halafu nikazidi kwenda kwa miguu juu ya vilima mpaka Betania, huu sasa mji mdogo sana, kimasikini tena, unatazamia Yeriko, wapata kwa Yerusalemi kama Kiungani kwa Mbweni. Nikaona kaburi la Lazaro, tena hapa nalipata kuona mizeituni iliyokuwa matawi mageni. Nikarudi njia

MSIMULIZI. 53

ngine. Njia hii kubwa zayidi ndiyo aliyoendea Bwana Juma a pili ya Mitende. Humo nikamkuta mtu mmoja tu naye mwenyi kupanda punda. Njia hii kuzunguka miambani kwanza huonekana mlima wa Sayuni (mji mwenyewe usionekane) ndipo huanza kusema Hosanna. Halafu baada ya mayili nzima, huona moskiti zile kubwa karibu sana, zamani huona hapa Hekalu na uzuri wote, ndipo alipoanza Bwana kulia juu ya Hekalu la Muungu. Sasa njia hushuka boondeni tena, nikapita kwa makaburi mengi mengi sana. Killa upande hapana kitu illa makaburi tu. Tena hapa makubwa matatu. Kaburi la Zekariya la Yakobo, nayo nguzo ya Absalome. Nikaenda Gethsemane tena, nikashuka chini sana liko kanisa moja ndani ya inchi, kushuka kwa madaraja tu. Kiisha nikazidi kushika njia ile Bwana wetu alivyopanda katika daraja ya Kidrori hatta mjini, huingia mlango mmoja uliokwitwa wa Stefano Mt. ndipo alipopigiwa mawe, sikuingia nalizunguka nje, kupita kuta na maboma makubwa sana, halafu upande wa kaskazini nikapanda kilima kidogo karibu na ukuta, tena karibu na mlango wa Dameski, Gen: Gordon na wangine huona, hapa ndipo aliposulibiwa Bwana, nami nasadiki, umbo lake umefanana punde na kitwa cha mtu, nalitembea sana hapa, nikaendelea kwangu karibu na kuuzunguka nje mji pia. Ukubwa wake kama Unguja pasipo Ng'ambo ao Malindi, lakini pande zote boonde na milima, humo mwote tena makaburi, yenyi mawe juu yake. Ukiona kaburi moja Unguja, hapa utaona mia.

Siku yangu ya mwisho baridi sana na theluji, theluji tele chini, tena hushuka, naliogopa kupanda gari nikaenda kwa miguu tangu saa tatu assubuhi mpaka saa kwanza usiku kwenda kwenda tu baridi na mvua mno. Usiku nalifika Ramleh, nikalala kwa mapadre Wafransa, assubuhi mapema nikaendelea tena vile vile kwa miguu hatta Yaffa, nisione gari hatta moja la kunichukulia. Nilifika saa 'nne assubuhi.

MSIMULIZI. 54
nikachoka kidogo tu nikahubiri Kanisani alasiri, kwani Juma a pili. Hatta Juma a tatu nalipanda marikebuni, nikazunguka Beiruti, Tripoli, Larnaka, Alexandretta, Mersina (karibu na Turo) Smurna, Salonika, Atene, hatta Marseilles. Sasa nipo tena Ulaya nikampata Bibi na Jardi hawajambo kidogo. Muungu awe nanyi nyote. F. R. Hodgson.

HABARI ZA NYASSA.

Tumepata habari kwa ndugu zetu waliokwenda Nyassa, kwanza wamekaa sana Matope, kwani hawakuweza kuendelea mbele kwani maji ya mto Shire yamepunguka. Bassi William E. Kanyopolea na Denys Sayite wamekaa mji mmoja karibu na Matope, uitwao Patsapa, na Mfalme wa hapo jina lake Lionde amewapa ruhusa wajenge Chuo kikubwa kwa watoto wanaowafundisha; Aruffo na mkewe wanakaa Matope kufundisha watoto, na Augustine na mkewe kathalika. Katika mwezi wa Jannary, wametueleza kama mto sasa unaanza kujaa, bassi tutarajivyo wamefika Lukoma. Na Mr Johnson ametuarifu kama wote wanatenda vizuri kazi zao. So Songolo atarudi hapa Kiungani, na William na Denys watatwaa kazi yake kufundisha katika mji Mesanji, Aruffo atakuwa mpishi wa Lukoma, Augustine labda atakuwa akifundisha watoto wa Lukoma.

HABARI ZA MLOLELA AO CHITANGALI.

March 14, Tumepata habari kwa Mwalimu Cecil Majaliwa, ndizo hizi, Nafurahi mno kuona ile Chama cha Mtume Paolo Mt. ginsi kinavyoendelea na kifanikiwavyo, Muungu Mwenyiezi azidi kwa wingi wa rehema zake kuondokesha waalimu wa Afrika waingie katika shughuli yake ya kuvuna. Nathania haitaji kukuambia shughuli za hapa. Kwani siku hizi nina watu wengi watakao kufundishwa, nami ni

MSIMULIZI. 55

peke yangu, na Harry anisayidia sana. Juma a tatu assubui nina Darasa ya watoto wanaojifanya tayari kwa Ubatizo tangu saa nne unussu hatta saa tano. Alasiri yake tangu saa kenda hatta unussu, kuwafundisha waume na wake wote thelathini, na hawa pia natumaini Muungu atawachagua wangine wao kubatizwa siku kuu ya Pasaka. Juma a nne Assubui ni kama Juma a tatu, lakini alasiri yake nina watu wanaotaka kufanywa waanafunzi, nao huja saa kenda hatta unussu kwani wangine wanakaa mbali kidogo, watu 34 waume na wake.

Juma a tano saa nne hatta unussu watoto wawili walio Wamasihiya nao wanajifanya tayari kwa kutiwa mikono na Askofu akionekana upande huu, kwani uthia wa siku hizi haitaji nikuambie, hatta hapa Lindi pana watu wetu hupata uthia. Lakini alasiri ya Juma a tano nina nafasi ya mambo yangu. Alhamisi saa tatu assubui huja wakuu watatu kujifanya tayari kuwa waanafunzi, mmoja ndiye nduguye Nakaam, jina lake Marachila, naona siku hizi anajaribu sana, kwani zamani alikuwa mlevi na mkaidi, alhamisi hii tumefanya shauri kwa wake wake, kwani anao kumi na mbili, na huku sharti mke awe na mume, ao ni mashaka mno asipokuwa na mume, kwani ataka mume amsayidie wakati wa kulima, kujenga nyumba, na juu yote amsayidie wakati wa vita, kwani asipokuwa na mume husumbuka mno kama hana jamaa wa kumsayidia, kweli inchi hizi mbali na huko Unguja, na alasiri ya Alhamisi nina wale watoto wa Ubatizo, na wale wawili walio Wamasihiya, Ijumaa saa nne nawafundisha watoto watakaobatizwa, saa nne unussu hatta saa tano nawatwaa wale wawili watakaotiwa mikono, lakini alasiri sina shughuli isipokuwa kuzunguka katika vijiji wanamokaa, uthia wa watu wa inchi hii ni siku zote kugombana, na kupigana, na kukamatana, kweli mtu apata kufundishwa, akiwa na watu kama hawa, hali yao ilivyo na ujinga na usingizi, pasipo khofu

MSIMULIZI. 56
ya Muungu, upendo wake, na ukuu wake, juu yote shauko lake la kukombolewa kwao na wokovu wao. Lakini na hivyo hawajui, kweli mimi nafayidiwa mno kwa kukaa nao.

Tumepata tena habari kwa mletaji habari, kama Makwangwara walifika Chitangali kusudi kuupeleleza mji wapate kuupiga, bassi mzee Barnaba Nakaam, akawauliza mmetoka wapi? wakasema, Yao, lakini wakatambulikana sababu hawajui kusema Kiyao, nao ni usiku saa tatu, bassi wote wakakamatwa. Na tumemkamata kitoto chao jina lake Baraka, labda atakuja huko Kiungani kusoma, akiwa mwalimu aende kuwafundisha babu zake. Na kanisa letu limeisha kujengwa tena, na February 16 mtoto wa Harry Muubi amefariki, na mwalimu Harry anafundisha chuoni watoto asharini.

HABARI ZA KIUNGANI.

Feb. 19 Mr Jones-Bateman alifanywa Archdeacon wa Unguja, mahali pa Archdeacon Hodgson aliyekwenda Ulaya. Mwezi wa March tumewasafirisha waalimu wawili kwenda pande za Bonde, nao ni hawa Herbert M. Feruzi na Philip E. Yahom, na wote wawili hawakai pamoja, illa Herbert anakaa Magila mahali pa Manfred Manyula kwani amerudi hapa, na Philip anakaa Misozwe pamoja na mwalimu Henry Nasibu. Tena James Mwaimu, mwalimu wa Mkuzi, naye amerudi kwao Mkuzi pamoja na mkewe. Bassi katika mwezi wa February amesafiri Mzungu mmoja wa hapa kazi yake kupiga chapa, jina lake Mr Symonds, bassi alikuwa thaifu sana, na Daktari amemwambia aende kwao Ulaya.

HABARI ZA MASASI.

Feb. 15, Ndugu zetu, siku zile zilizotupitia tulikuwa na hatari za Waarabu kwa ndugu zetu wanaokwenda Lindi kuchukua mizigo ile inayotoka Unguja. Ilikuwa meli ya juzi, bassi Waarabu wakatwaa mizigo yote wakaifunga kati

MSIMULIZI. 57

ka nyumba ilikuwa ya Serafi, aliyoitwaa Dachi akaifanya ya kulala mwenyewe karibu na pwani; bassi wakaitia yote mle ndani, akafunga mlango. Wakanena wangine, tuwatwae hawa watumwa wao tuwaue, waje labda Wazungu wa barra tupigane nao, Ndipo akaondoka Selim rafiki wa Bwana Askofu, na Isa bin Sinnen, wakaenda mpaka Lindi wakawaarifu wenzao waliozuia mizigo; kunena kama wanaogombana nanyi sio hawa; tena hawa mliozuia mizigo yao ndio Waingreza na hao mnaogombana nao ndio Madachi. Tena kwa kuwa Selim na Isa, watu wakuu kuliko wao wakawapa mizigo. Watu wetu wakarudi wakatupa habari zilizowapata. Bassi Bwana T. L. Taylor akaandika barua ya Kiswahili ya harufi za Kiingreza akampelekea meli ya jana kumwarifu kama Wazungu wanaowataka kupigana nao ni Madachi. Tena Mapadre hao si kazi yao ya kupigana na watu wo wote. Na kuwafahamisha makusudi gani wamekuja hapa, ao nani aliwapeleka na kufanya nini hapa.

Bassi meli ya leo ilipowasili akaleta majibu Selim maneno si mengi machache tu, kunena kama yeye hataacha kuwasayidia kwa nguvu alizonazo hapa Lindi, kwa ajili ya urafiki wano wa zamani na Bwana Askofu; labda mimi Selim nife ndipo sina nguvu za kuwasayidia ninyi tena. Tena msije watu wa Masasi pamoja na watu wa Machemba kwani wana uthia mwingi mno, salamu.

Na katika Jan. 16, Bowani (Mbowani) na Majaha, ndio Makwangwara wanaotumwa siku zote killa pahali, bassi wamekuja na Walugaluga ndio Wanyamwezi waliokuja wengi wengi sana majeshi matatu wamefikia kwa Mhalule. Bassi wamekuja kununua baruti na bunduki kuwapa hawa Walugaluga wapate kuwasayidia vita. Tena Sonjela amepeleka fimbo yake kutaka urafiki kwa Machemba lakini hawa hawawezi kwenda pwani watu watawaua. P.K.

MSIMULIZI. 58

HABARI ZA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Baada ya salaam najaribu kukueleza habari mbili tatu. Siku hizi za Kwaresima kuna kazi moja, ndio kutoka na kuzungukazunguka kuwatafuta watu waliotoka katika shamba hili la Mbweni, nao wenyi kazi hii huenda wawiliwawili, siku hizi wanapatikana watu wa kuja Kanisani, zayidi wanaake wanakuja wengi. Ijumaa ya jana nilikwenda kuwatafuta watu, nikapita mahali pana nyumba nne nikawakuta wanaake watatu Waswahili na mwanamume mmoja, nikawaambia mje Kanisani jioni, wawili wakasema tutakuja, na mmoja akasema, sisi tunamwogopa bwana wetu ndiye Sayidi. Mwanamume huyo aliyekuwapo akasema huyo Sayidi labda unamwogopa wewe peke yako lakini sisi wenzako tunakwenda killa siku, siku ya Juma a pili. Bassi mwanamke yule akasema. Tutakuja kwa sababu tunaitiwa habari njema, na tena Mzungu ni kama shina na sisi matawi, tunapenda sana tujue habari za Muungu lakini tunaogopa kutiwa gerezani, labda tukizoea kuja Kanisani tutachongewa, nikamwambia ukitaka kujua habari za Muungu usiyafikiri yatakayokupata, halafu akasema, nataka sana nizijue habari zake aliyetutia roho, aliponena aliyetutia roho akainua macho juu. Ndio mwisho wa habari hizi.

Juma a nne March 18 ilikuwa "Retreat" ya Waalimu wa Mbweni walihamia kwa shamba la Miss Thackeray aliolinunua kwa Balyozi mkubwa hatta Juma a tano wakarudi.

March 25, 1889 Ilikuwa siku ya Chama cha Watakatifu.

Feb. 17, Watu kumi na tano waliotiwa mikono na Askofu watoto wa ndani edashara na wa shamba wanne, jumla kumi na tano. M.M.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Baada ya salaamu ninakuarifu mhabari mwingine kidogo ni huu, mkewe

MSIMULIZI. 59

Nicholas Faraji amepata mtoto mwanamume naye jina lake anaitwa William Nicholas.

Ninathani mtapenda kusikia habari ya jamaa wetu mmoja Mmasihiya. Kwanza alikuwa katika Mission ya Mombasa, lakini kule Mombasa alitoka akaja zake hapa Unguja, halisi makao yake yalikuwa Mkunazini, naye alioa mtoto wa Mbweni, bassi alikuwa hawezi siku nyingi hatta alihamishwa huku Mbweni kusudi atazamie baridi ya huku labda itamfaa. Lakini tujuavyo apendalo Muungu hapana mtu awezaye kulizuia, bassi Mwenyewe amemtwaa kiumbe chake; na jina lake Paolo Raha.

Ah siku hizi katika shamba la Mbweni limejaa waanawake wengi wajaani, pana nussu waume wao wamekufa, na nussu waume wao wametoroka.

Habari ya Chuoni ya shamba la Mbweni Mwalimu Cornelia ametoka, sasa Mwalimu wao watoto wa shamba ni Nicholas Faraji. Mbweni siku hizi mtu aliyetoka zamani hapa Unguja kama Muungu kumjalia kurudi salama salimini atakuja kuona Mbweni imebadilika kwani ataona sasa, kuna gari la farasi Bwana Mr Wallis amelinunua kwa Bwana Balyozi. G.K.

HABARI ZA NEWALA.

Bwana Porter alikwenda kwa Machemba akamkaribisha vema, na Feb, 17 mfalme mmoja wa Wamakua anakwitwa Nampepa amefanywa mwanafunzi leo, Mr Porter akamfanya kwa maneno ya Kiyao, tukaisha tena ikafanyika sala ya assubui, tukaondoka. Katika January, alikuja Mr Taylor toka Masasi, akakaa siku chache akaenda zake Masasi, tena akaja Bwana Cecil Majaliwatoka Chitangali, na yeye pia akakaa siku chache akaenda zake Chitangali. Na siku hizi toka January, Bwana Porter atakaa juu Makonde, huku mjini hushuka Juma a tano na Juma a mosi kwa kufanya Usharika Mtakatifu, tena Makonde karibu

MSIMULIZI. 60
itajengwa nyumba ya Mission.

Katika mwezi wa March tumefiwa na ndugu yetu Ruth Kabango alichukuliwa na maji ya mtoni, siku ile ile mtoto mwingine alitaka kwenda na maji kwani sasa wakati wa masika, lakini ameokoka na nguo yake imeenda na maji. Mwalimu Joseph Mtapakoma hajapata afya bado kwa ugonjwa wake. Katika March nyumba ya Mission imeanza kujengwa Makonde.

HABARI ZA MAGILA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Baada ya salamu nakuarifu kama katika mwezi wa March Mr Goodyear amefanywa Archdeacon wa Magila. Tena March 25 Bwana Askofu na mimi Hugh Mhina na John B. Mdoe na Francis Shame tulienda Umba, na March 26 tukashika njia ya kushukia Vanga, na mvua nyingi ilitupata. Tena tukafika Digo katika mji uitwao Mlalo tukapumzika hapo, na katika safari ya Bwana Askofu, alikuwapo Mr Key na Dr Ley wa Magila wanashuka Unguja. Tukaendelea mbele tukafika mji uitwao Karibuni tukalala hapo, hatta siku ya pili tukashika njia, na Askofu akashikika na homa ya nguvu, bassi hatuna buddi tukae tusiendelee mbele, na mahali penyewe panaitwa Bagamoyo. Na Wadigo wengi wenyi vidonda wakaja kutiwa dawa, tena tukaendelea siku ya pili tukafika mto uitwao Umba tukapumzika hapo, marra wakaja Waarabu wawili wakamuuliza, ninyi ni Madachi ama Waingreza? Askofu akasema, sisi ni Waingreza, Waarabu wakawaambia "sisi siyo taka Dachi, lakini Ingreza iko rafiki hapa Vanga" kiisha tukaendelea hatta tukafika Vanga. Na Vanga ni mji uliozungukwa na ukuta mrefu wa mawe, uko karibu na pwani na mzuri sana. Kiisha tukakaa siku moja, ya pili tukaingia katika Manuwari H.M.S. Mariner pamoja na Askofu tukawasili Unguja.

Barua ya Mletaji hatukupata safari hii. Mtg.

MSIMULIZI. 61

HABARI ZA MKUNAZINI.

Nawaarifu habari za huku kwetu, ya kuwa huku kwetu nyumba hii tunayokaa, Norman Namkachapo anasafiri anakwenda Magila, kufanya kazi miezi miwili na atakaporudi atakuja kuoa. Na sisi Juma a pili ile iliyokwisha March 31. twalikwenda katika H.M.S. Agamemnon twalienda saa ya saba tulipokwisha kula, watu watano jumla yetu tuliokwenda, tukatembea wakatuonyesha namna zote za vitu, selaha za vita hatta sisi tukachoka. Tukaambiwa sharti mngoje hatta saa kumi tukashuka. Na Balyozi Mkubwa amesafiri Ulaya, na Bibi mmoja wa Mkunazini Miss Smith. Hapa Mkunazini pamejengwa kitalu cha kukaa na kucheza sisi usiku tusipate kwenda kwingine. Kwenyi lilipokuwa zamani banda la sermala hatta birika la maji ya kanisani. G.D.

Watu wanaokaa barra peke yao wametuomba tupige chapa killa mwezi kilia mahali anapofundisha killa mwalimu mweusi, wasipate kusahauliwa, bassi shauri litafaa sana. Tunataka kuanza mwezi wa June.

Tukiisha piga chapa hii yote habari imemfikia Bwana Askofu kama Majumbe wote wa Pangani wanataka kupatana tena nasi, tupite njia ya Pangani siku zote, watatutendea urathi kama zamani.

Na Bushiri siku hizi anaanza kupiga shauri la amani na huyu Mdachi aliyekuja siku hizi. Bassi labda uthia utakwisha karibu sasa. Mtg.

April 14, Juma a pili ya Mitende, Granville Kachipumo na Martin Furahani walifanywa Wasomaji hapa Kiungani.

MSIMULIZI. June, 1889. V.
Imepigwa chapa Kiungani, Zanzibar,
katika "Universities' Mission to Central Africa."

VITA YA WADOICHA.

Siku hizi mkuu wa Wadoicha Captain Weismann amepigana na Bushiri karibu na Bagamoyo; Bushiri amejenga kituo na ngome hodari sana. Wadoicha walikuwa watu 920; ndio watu weusi Wasudani na Wazulu 600 na Wadoicha 320. Bushiri alikuwa na watu 600, karibu wote Waarabu. Walipigana kwa moyo sana, lakini mwisho Wasudani wakavunja ndani wakawafukuza Waarabu. Waliuawa wa Bushiri 80, na Wasudani 40 na Wadoicha wawili. Bushiri alijirudisha kwa kituo chake cha pili mwendo wa saa tatu akaanza kujenga ngome vile vile. Juzi, May 28, Wadoicha wamepiga mbiu kama wataanza kupigana June 1 na watu Wamrima walio kama kaskazi ya Bagamoyo, ndio katika Saadani, Pangani, Tanga, &c., bassi sasa vita inakaribia kwetu Bonde, nasi tunaomba sana isifike ndani, illa pwani tu.

Kwa kusini Lindi imekuwa uthia mtupu, hatta Bwana Askofu hakuweza kabisa kuchagua njia ile ya kufika Newala na Nyassa. Bassi akachukuliwa na H.M.S. "Mariner" hatta Tunghi kwa kusini kidogo. Ndio bandari waliogombania Wareno miaka miwili wakisema ni yao, Waingreza wanakataa, bassi kwanza Wareno walitaka kumzuia Bwana Askofu lakini amri ikatoka London kwa simu kumwambia Admeli apishwe ndani hatta kwa nguvu wakitaka kumzuia. Bassi wakampisha ndani na msafara wake kwa amani.

HABARI ZA NYASSA.

Leo hivi June 1 amefika Unguja Mr. Warner na Capt. Sheriff wakitoka Nyassa wagonjwa, wanasema kazi yote inaendelea sana, lakini barua za ndugu zetu zimesahauliwa na wakili wetu Kilimeni. Denys na William, wanafundisha Likoma, na waalimu wangine kama

walivyoandikwa humo pangine, illa na Aruffo anafundisha Patsapa ilipokwama steamer kwanza mtoni.

MSIMULIZI. 63

KUFA KWAKE REV. HERBERT GELDART.

Juzi juzi tulistushwa hapa na habari za huzuni kubwa sana, kwani barua zikafika katika Mkuzi kusema kama amekufa Mr. Geldart baada ya homa kali ya siku sita. Alianza kuugua Juma a pili ya pili baada ya Pasaka, akafa Juma a mosi iliyofuata. Alikuwa akianza kazi kubwa kule Mkuzi pamoja na Mr. Mercer na Rev. John Swedi, na Umba na Msaraka kumekuwa chini yake kwani Askofu haweki tena Mzungu kukaa Umba illa kwenda kule Juma a pili, na Granville anakwenda kukaa Msaraka kufundisha kule na kufanya chuo. Bassi tumefiwa naye ghafula, naye ameitwa aingie katika raha yake. Ametimiza miaka kumi tangu alikuja kwanza Afrika. Sasa Mr Sparks, aliye Kasisi ametoka Magila kwenda Mkuzi kumtwalia kazi yake.

HABARI ZA MBWENI.

May 29. Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Nakuarifu habari ya ndugu yetu mmoja aliyefiwa na mtoto wake May 26, naye Ursula aliyekuwa mke wa marehemu Gaiusborough Kimaramsele, Muungu amemtwaa. Tena nathani mtapenda kusikia habari za ndugu yetu Isaak Kambango aliyeunguliwa nyumba yake May 26 usiku saa saba killa mtu amelala.

Mtu akaja akaichoma nyumba yake, na watu walipotahamaki moto umeisha shika nyumba, na vilivyookoka ni kasha moja, na kitanda. T.M.

Safari hii hatukupata habari kwa Mletaji habari za Mbweni nyumbani. Mtg.

HABARI ZA MAGILA.

April 10, ilikuwa Siku ya faraga (retreat) kwa walimu wote, tukaanza Juma a nne jioni saa ya pili unussu baada ya saa ya pili sala ya jioni, tukashika faraga hiyo hatta siku ya Alhamisi assubuhi. Haya majina

ya waalimu waliokuwapo katika faraga hiyo: Rev. John Swedi, Ackworth Machaku,
MSIMULIZI. 64
Hugh P. Kayamba R., Samuel Sehoza, Leonard Pesa, Lawrence Kombo R., Henry Nasibu, Herbert Martin Feruzi, George Songolo.
April 19, Jumaa Kuu, watu wengi walikuja kwa sala ile kubwa ya saa sita hatta saa tissa. Archdeacon Goodyear akahubiri peke yake hubiri la kwanza la kueleza na Maneno yote Sabaa.

April 20, Ukawa Ubatizo katika sala ya jioni saa kumi na moja urobo, watu kumi na nne wakabatizwa. Katika hao waliobatizwa wawili wao walikuwa watoto wa nyumbani, majina yao Hiza, anaitwa Robert Lanton, mthamini wake ndiye Samuel Sehuza, wa pili Paolo Dezu mthamini wake Hugh Kavamba. Tena katika hao wawili palikuwa mtu na mkewe ndiye Gangana na mkewe Machambo, na baada ya ubatizo wakaenda mbele ya Mathbahu wakapiga magoti wakapewa Mbaraka kwa Arusi, kwani walioana tangu zamani sana mbele hawajabatizwa.

Tena wawili wao waliobatizwa walikuwa mwanamke na mwanawe, mama ni mzee na mtoto kijana umri labuda miaka 16 tu ao zayidi kidogo. Ndiye Mama Chaku na Mdoe, wanakaa katika mji mdogo karibu na hapa petu uitwao Kisiwani. Tena mwanamke mmoja aliyebatizwa akaitwa Monika, na mumewe alibatizwa zamani anaitwa Austini Singano.

April 22, Juma a tatu baada ya Pasaka, tulikwenda kushinda juu ya kilima kimoja palipo na nyumba iliyojengwa na Archdeacon Farler, tukashinda pale pamoja na Mr. Roberts, na Archdeacon Goodyear alifuata nyuma yetu akatukuta kule kilimani. Nasi tulichukua kuku wanne na mchele, tukaazima chungu katika mji ulioko karibu pale kilimani, lakini wenyewe hawakubali kutuazima burre, ikatupasa kutoa pesa kwa killa chungu tulichoazima na mitungi mitatu ya maji wakaleta, tukalipa pesa mbili mbili kwa mitungi miwili na mmoja mdogo tukalipa pesa moja.

MSIMULIZI. 65

Tukapika wali, na kuku wakachinjwa wakachomwa tukala, na baada ya kula tukacheza. Na pale kilimani tukaweza kuona mbali sana hatta tukaona vyombo baharini. Hatta saa kumi na moja unussu tukarudi kwetu.

April 25, Siku ya Marko Mwanjilisti, tukaenda kushinda mahali pangine kilimani paitwapo Seluka, penyi mawe mengi na makubwa na maji yashukayo kwa kassi na kuvuma sana kwani yanashuka juu ya miamba ile mikubwa. Tulifuatana na Mr. Roberts; lakini safari hii hatukuchukua chakula, illa tukapewa mapesa, wakubwa killa mtu pesa 4, wadogo pesa tatu, kwenda kutembeatembea kununua killa mtu chakula atakacho mwenyewe, ikiwa ndizi ao miwa, ao chochote apendacho.

Tukashinda kule na mvua ikanya wala hatuna kibanda, illa watoto wakajisetiri majumbani mwa watu. Hatta jioni tukarudi kwetu.

April 26, Walitazamiwa watoto kwa Maandiko Matakatifu tu sio katika mambo mangine ya chuoni. Siwezi kutaja sifa zake, kwani hatujaambiwa na Mtazamiaji bado. Na mtazamiaji ndiye Archdeacon Goodyear.

Watoto wanajaa furaha katika juma hii nzima zayidi kesho Juma a pili, wanatamani sana Juma a pili iishe upesi. Wanafurahi kwa sababu zamani ilikuwa desturi yao kwenda kwa mama zao marra ikiisha siku kuu, lakini katika Pasaka hii Archdeacon amefikiri akaona ni vema zayidi kuimaliza Pasaka kabisa, iwe Juma a pili kanisa lijae watu na kuimba nyimbo za Pasaka kwa furaha, na Juma a tatu ifuatayo kanisa liachwe tupu. Bassi mahali pa kwenda kwao katika Juma a tatu ya kwanza baada ya Pasaka ikabadilika ikawa kwenda zao Juma a tatu ya pili baada ya Pasaka: na kesho kutwa ndio siku ya kwenda zao bassi killa mtoto moyo wake umejaa furaha tu, twatazamia Juma a tatu ije upesi yawe matawanyiko muda wa Jumaa mbili nzima. Katika April 26, jana siku ya Jumaa tumepata

MSIMULIZI. 66
mtoto mwingineo aliyeingia Mission. Hugh P. Kayamba na N. Namkachapo wamefika salama, walifika hapa siku ya Juma a pili ya Mitende jioni kama saa ya kwanza unussu. S.S.

HERI NA SHARI.

April 28.
Tangu uthia wa Wadoicha hatta leo, Pangani haijawa rathi mno na Mission yetu, likitokea neno dogo tu la uwongo wa watu, Pangani hustuka, ya kwanza kwa habari za Bwana Askofu kupitia Vanga imewastusha mioyo, kwani wakaambiwa uwongo ya kwamba Mzungu amegeuza njia ya Vanga anapitisha selaha nyingi za bunduki apatane na Wabondei waipige Pangani. Tena wanunua vyakula vingi sana tayari kupigana, hatta majumbe yote ya Pangani wakaandika barua moja kwa shauri moja wakaileta hapa Magila kwa Archdeacon Goodyear kumwambia njia ya Vanga ile wasipite, wapite njia ya Pangani kama kwanza, wala hapana la kuwathuru kwani wakasema, wao hawana neno juu ya Mission tangu zamani sana. Naye Archdeacon akamwandikia liwali akamwuliza habari hizo za majumbe hawo wa Pangani amwarifu ginsi zao zote kama alijua shauri hilo ao halijui, kwani yee liwali ndiye mtu mmoja tu atusayidiaye Pangani na mashauri twasikiliza kwake yeye. Kujibu kwake liwali aliandika khati akaileta pamoja na majumbe mawili mmoja aitwa jumbe Mchuzi, wa pili jumbe Mwenjemwenje na huyu tangu zamani ni sahibu yangu sana, marra nyingi ameniita niende kwake walakini sijapata wasaa mwema kumwendea. Nao wamewasili hapa kwenyi April 14, Juma a pili ya Mitende saa ya nne unussu ya assubui tunasomesha darasa za Juma a pili. Hatta tulipokwisha, Archdeacon akawaita faraghani wakaitoa khati itokayo kwa Sulemani bin Nasor liwali, nikaisoma kwa Archdeacon kwani ni ya Kiarabu, na maneno hayakuwa mengi. Bassi ikasema, nimewaleta hawo majumbe mawili wakueleze wao wenyewe

MSIMULIZI. 67

habari walizonazo, na wakiisha kukueleza unipashe majibu waliokuja nayo huko Magila nami nijue. Baada ya kwisha kuisoma barua hiyo wakaulizwa habari zao, wakasema tumejia habari mbili, ya kwanza ukitaka kukaa hapa kaa walakini njia ya Vanga uiache upite Pangani, ya pili kama hutaki kuiacha njia hiyo uondoke uende zako Unguja. Naye akawajibu kwamba njia ya Vanga isingalivumbulikana illa kwa ajili ya uthia wao hapo Pangani, ya kwanza kwa kumzuia Bwana Askofu katika safari yake ya kuja Magila, ya pili wao wenyewe wakasema kama hawawezi kumpambanua Mwingereza na Mdachi kwani wote pia ni weupe, ndio kwa sababu hizi; na nyingine kama hizi za kuzuia mizigo yetu, ndio maana ikapitiwa njia ya Vanga kwani huko hapana uthia. Nao wakasema kama sasa amani ruhusa njia iwazi hapana neno wala jawabu lolote, wakasema na Mzungu aliye yote wa Mission akitoka Magila ao Unguja asipite njia nyingine illa Pangani, ndipo Archdeacon akawaambia ataandika barua kwa Bwana Askofu amwarifu habari hii yao, wakasema, Haya, andika, ukiisha tuchukue Pangani tuwaonyeshe majumbe wangine nao wajue kama kweli tumepatana tena. Bwana Goodyear akandika barua mbili, moja kwa liwali na ya pili kwa Bwana Askofu akawapa zote mbili wachukue; kiisha akaagana nao wakaenda zao kwao. Na leo April 28, tumepata barua mbili moja yatoka Unguja kwa Bwana Askofu, ina habari hizo hizo za Pangani, na ya pili yatoka kwa liwali, asema kama hakuyaamini sana maneno ya majumbe ya Pangani, ndipo akaandika barua kwa Sayid Khalifa amwulize mapatano haya ya majumbe na Wazungu wa Mission kama kweli ao akili za majumbe tu, naye asema kama amepata majibu mema lakini ginsi ya wema wake hatujui, kwani hakutueleza, na mwenyi kuleta hizo barua ni mtu wetu Maftaha alindaye nyumba yetu ya Pangani, naye ametupa habari njema, ya kwamba tangu kurudi kwa majumbe,

MSIMULIZI. 68

Pangani imetulizwa kwani wameambiwa kama habari zote wasikiazo ni za uwongo mtupu, kwani tena walisikia kama njia hii ya Vanga imepita Wadoicha mia kuja hapa, nao majumbe walikuja kupeleleza hayo pia wasione neno.

Pana ishara ya wema wao, zamani walipokamatwa ndugu zetu Kipumbwi ilitulazimu kuwakomboa kwa fetha, naye liwali akatoa rupia sitaashara kusayidia kuwakomboa, hatimaye akarudishiwa rupia asharini na tano pamoja na barua ya kumshukuru kwa hisani yake kwetu, na leo twaona barua yake pamoja na fetha aliyopelekewa kairudisha kwetu tena akisema kama hakuitoa kwa kutaka fathili tena, illa ametoa kwa hisani tu bass. A.M.

HABARI ZA CHITANGALI.

Mambo ya Siku kuu ya Pasaka ni hii. Assubuhi ilikuwa mvua kubwa sana hatukuweza kwenda kanisa kubwa, tukasali hapa nyumbani sala za assubuhi, hatta mchana wakaja watu wengi sana Wamasihiya na Waanafunzi na watu wanaojifunza kuwa halafu waanafunzi wakajaa kanisani, waume na wake. Tulipokwisha sala yote na kuhubiriwa pia, tulipotoka waanafunzi wakapokea nyama na killa mtu wakaenda zao wakifurahi sana mke kwa mume. Siku iliyo mbele ya Pasaka B. Nakam mfalme akatuchinjia mbuzi sisi watoto wote hapa nyumbani. Juma a tatu baada ya Pasaka akaja Mr. Porter na watoto wa Newala thenashara jumla. Juma a nne tukapokea Usharika Mtakatifu, hatta siku ya Juma a tano watoto kenda wakabatizwa saa tissa unussu, tulifurahi sana siku hii tulipopata jamaa hii imepata kuingia katika jamaa ya Kimasihiya, wamasihiya wote na waanafunzi walikusanyika pamoja siku hii, na baba na mama wa watoto hawa waliobatizwa walikuwapo kutazama. Siku hii tena tulipata mbuzi na tulifanyiwa karamu. Tumepata jambo moja la kusikitisha sana, April 24, aliingia mjini hapa mwivi, aliingia kanisani

MSIMULIZI. 69

akachukua nguo zote za kanisani nyeupe na nyeusi, tena akaja hapa nyumbani akaingia chumba cha Bwana wa hapa Chitangali, akazikuta nguo zimewekwa katika kamba akazichukua zote na nguo za watoto, na vichupa vya dawa, na msahafu mkubwa pia akachukua. Assubuhi tukaamka tukamtafuta hatukumpata hatta kidogo.

Kweli, kama nijuavyo kama mahali panapoanza Kimasihiya sharti pawe na uthia mwingi kwanza, ndipo tena watu wataanza kuongoka kidogo kidogo. Bassi sasa mniwie rathi msikie habari ya watu wetu, kwanza safari hii barua zetu zimechelewa sana, hatukuzipata upesi na tena watu wetu wanaokwenda kuchukua mizigo wamerudi mikono mitupu, tena wamekimbia, usiku wakarudi hatta hapa Chitangali, ginsi uthia ulivyozidi Lindi walitaka kuuawa watu waliokwenda kuchukua mizigo, hawakuleta kitu wala karatasi ginsi watu walivyo wakali kama simba. Na habari za hapa ni hizi, mwezi wa February wamekufa watu wawili mke na mume, tena April 6, wamekufa watu watatu mama na mtoto wake na mume mmoja, bassi watu wa inchi hii Wanasema si burre illa tangu alipokuja mwalimu inchi yetu kufa kumezidi, tena mbona watu wanakufa Juma a pili ndio anavyotukataza tusifanye kazi, na watu wanazidi kufa hatutaki kwenda kwa mafundisho tunakwisha. Watu wasemao maneno haya ndio wasiyoingia kabisa kanisani, huwashawishi walio waanafunzi kusudi wasizidi kwenda kufundishwa, lakini siku ya Juma anne ginsi watu wanavyokuja kwa mafundisho wengi sana, kweli shauri la waovu litakoma kwani wamemsahau Muungu Mumba wao, na akifa mtu husema si burre illa amelogwa; muungu wao watu hawa ni uchawi. Tena hapa yupo baba, na baba huyo ndiye aliyemzaa mfalme wa hapa yeye na nduguye, bassi alikuwa na mtoto mkubwa, zamani akawa mwanafunzi akafa; tena mtoto wake mdogo alikuwa akija kusoma amekufa pia. Bassi baba huyu amepiga marufuku watoto wake

MSIMULIZI. 70
waliosalia wasiende tena kwa Mzungu, wala yeye baba hajatembelea upande wetu, ana hofu ya kufa, anao watoto wawili nao wafalme wote, mmoja Mmasihiya na mmoja karibu atakuwa mwanafunzi, lakini wangine waliosalia amewahifathi wasife, tunatumaini kama baadaye macho yao yatafunuka, wengi sasa wanakuja wenyewe kutaka kujifunza maneno ya Muungu. M.H.

HABARI ZA MISOZWE.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Baada ya salamu nakuarifu habari za hapa petu Misozwe, katika April 27 miji ya hapa karibu na petu palikamatwa wanaake watatu na kijana mmoja wa kiume, nao ni waanafunzi wanaofundishwa hapa kwa Umasihiya. Watu wa hapa wakajaribu kuwatafuta pande zote walikoweza, ikapata siku saba walikuwa wakitafutwa. Mwisho wakapatikana wamekwisha uzwa, wamepelekwa Tanga, huko ndiko walikopatikana; wakaletwa hapa kwa furaha nyingi, kwa kuwa Padre wa hapa ndiye aliyetuma yule kijana mwanamume kwenda kumnunulia vitu vyake, na hawa wanaake ndio waliochukua mizigo iliyonunuliwa Gulio (gulio ni mahali wanapokusanyika watu kuuza vitu na kununua,) Padre wa hapa akaonyesha naye pia kama amefurahi sana kwa kuokoka kwao, na juu yote ni kwa sababu ni waanafunzi, akawachinjia ng'ombe kuwafanyia karamu. Na jumbe Makange aliye karibu naswi, aliposikia ngoma za vita akathani kama ni habari asikiazo marra kwa marra za Waarabu kuja kuwafukuza Wazungu wa huku Boonde, akaja marra na askari zake wamejifunga tayari kwa vita kupigana na Waarabu, akakaribishwa kama ilivyopasa. Tukamweleza habari ya ngoma alizozisikia usiku, alipojua kama ni habari ya kukamatwa watu kama ifanyikavyo marra kwa marra katika inchi hii na pande za huku; na akajua tena kama anayekamata watu jina lake aitwa

MSIMULIZI. 71

Bawa naye huyu alikuwa katika shauri hili kwa sababu watu wanatoka katika mji wake, bassi Makange akaamuru watu wawatafute wale wanyang'anyi wakionekana ao wasipoonekana wampe habari, akaenda zake. Lakini shauri lake lilikuwa kama akiwa ndiye Bawa wafanye shauri apigwe kama alivyopigwa mtu mmoja aitwaye Jengo aliyekuwa na desturi ile ya kukamata watu na kuwauza. Ikatukia habari kama wanyang'anyi wameonekana na mmoja wao ndiye huyu Bawa, na sasa watu wanafanya mashauri wakampige Bawa, kwa sababu watoto hawa wakaenda kutwaliwa katika mji wake Bawa naye ndiye aliyewarudisha tangu Tanga, alipojua kwa hofu kama anafanyiwa mashauri ya kupigwa, bassi hatujui mashauri yao yatakavyokuwa.

Juu yote sisi tumefurahi mno kwa kuokoka kwao katika utumwa kwani twataraja watakuwa Wamasihiya.

P.S. Na hivyo juzi hapa mtu huyu huyu Bawa amekamata watu wangine wanne. P.E.Y. pro. H.N.

Bassi wenyewe waliokamatwa wametuhadithia hivi,

Tumekamatwa tuliporudi sokoni, soko lenyewe linaitwa Bwembwera. Watu wenyewe tuliokamatwa tu wa'nne, majina yetu ni haya, mwanamume mmoja, jina lake Lugulu, na waanake watatu, wote tu watoto wa mtu mmoja, ndio Mamhando Mboza, Mamhando Mwaiko, na Manyelo Gumbo. Bassi tulipokamatwa tulifika karibu na mjini, tukataka kupiga ukelele, kusudi tuwaite watu, lakini wakasema msipige ukelele, mkizidi kupiga ukelele, tutawaueni, yule mwanamke Mamhando Mboza, akapigwa shime ya mkono. Hatta tulipoendelea mbele tukanyang'anywa mapesa yetu na vikuku vyetu, hatta tulipofika mbele kidogo, tukakuta kibanda tukaingia tukaona maji tukanywa, tukaenda usiku kucha, hatta tulipofika inchi ya Wadigo kunakucha, tukafanyiwa uji wa mpunga lakini hatukuunywa vema.

MSIMULIZI 72

Tukaambiwa tuapishwe, tukiisha watuvunjie chungu, kwani ndio viapo vya inchi ile yote tangu Bonde hatta Digo. Hatta tulipofika njiani mimi Manyelo Gumbo, na Mamhando Mwaiko, tukataka kutoroka, lakini wakasema, tukiwaoneni tutawakateni kwa shime.

Tukatoka kwenda Tanga kuuzwa, hatta tulipofika, tukafanyiwa ugali wa mtama, tukalala. Hatta assubui yule mwanamume Lugulu akauzwa, lakini bei ikavunjika kwani wakasema hatutaki kununua Wabondei, kwani watu wamesema Wabondei wasiuzwe. Tukawaambia wale watu, tupelekeni kwa Abdallah Gugu atukomboe kwani mtu huyu tunamjua sana, lakini tukamngoja wee hakuja, tukarudi tena nyumbani kulala, hatta assubui tukaambiwa twende, tukaenda tukafika njiani safari ikavunjika tukarudi tukaambiwa safari ni kesho. Hatta assubui tukatoka kwenda zetu, na njiani tukapewa madafu tukala, hatta mbele kidogo tukapewa samaki zetu zikanunuliwa, haya tukaenda tukafika Digo, tukanunua muhogo. Wenzetu tukawaacha nyuma, tukatangulia, tukafika njiani penyi kisima tukaoga, hatta wenzetu wakatufikia palepale, wakataka kupigwa kwa shime. Tukatoka pale tukafika karibu na mji zikapigwa bunduki mbili. Tukafika mjini, tukaambiwa tazameni baba zenu hawa, tukaingia katika nyumba, tukaambiwa, haya twende zetu kwetu, tukapewa nyama, tukashika njia ya kwetu. Haya tukaenda, tukafika mji mmoja unaitwa Mabungu, tukakutana na shemeji wetu mmoja anaitwa Kizuguto; tukaenda tukafikia mji ulio karibu na kwetu unaitwa Bagamoyo, watu wa kwetu wakaja kutulaki, tukaja hatta kwenyi mji wetu.

Baba zetu wakatuchinjia kuku juu juu kwa furaha kwani ndio desturi ya kwetu. Tukapewa chakula tukala. Tukaisha tukapewa zawadi, tukalala. Hatta assubui, tukachinjiwa ng'ombe na Mr. Woodward, na bunduki zikalia

sana, na karamu hiyo ilikuwa kwa sisi na watu waliosayidia kututafuta. Tena watu wa Bagamoyo karibu na petu wakaja kutuamkia. AAS.

HABARI ZA MKUNAZINI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu, huku kwetu Askofu amemtwaa Oswald Akusama afuatane naye kwenda Nyassa na kumfanyia kazi njiani kwa muda wa miezi mitatu. Siku kuu ya Pasaka, Juma a nne tulikwenda kisiwani katika mashua mbili, tulipofika kisiwani, marra wangine walienda kutafuta paa, lakini hawakupata; na Mzungu mmoja tulienda naye jina lake Mr Betham.

Siku ileile aliposafiri Askofu, na Herbert Selenge aliyetoka Magila akawasili hapa, na Prancis Shame siku hizi anakaa Mkunazini. G. D.

HABARI ZA KIUNGANI.

Siku kuu ya Pasaka hii tumefurahiwa mno, kwanza Juma a mosi jioni twalienda Mkunazini kwa sala ya jioni pamoja na Ubatizo; Walibatizwa watu sita wa asharini, watoto wa hapa kumi na kenda, ndio hawa: Charles Janson Mkumbukwa, Ammi Mvuma, Yohana Nibakali, Petro Sulemani, Petro Mlanzi, George C. Mshindo, Petro Kilekwa, Wilfred Zulangeti, Nikolao Mchege, Daudi Kahambwa, Oswald Mswakolo, Yohana Hamisi, Edgar Mwambala, Klaudio Mtindwa, Wilfred Dahire, Tomaso Kaponga, Greorge Kambwende, C. Ley Suudi, na Stefano Mgohay na watu wazima saba, kiisha tukarejea hapa Kiungani. Juma a pili iliyo siku ya Pasaka tulifanya ibada yetu papa hapa wala hatukwenda mjini kwani twalitaka kulilimbuka Kanisa letu. Katika Jumaa May 10, watoto wale waliobatizwa walitiwa mikono illa wawili tu, pamoja na Yohana Kimbilieni.

Tena May 12, Askofu amesafiri kwenda pande za Nyassa

pamoja naye Mr. Hainsworth, na Mr. Watson, na Yohana B. Abdallah, na Enoch Mtaiwa, na Peter Selenge na watoto wanne wa Newala. Katika mwezi huu wa May Mr. Matthews amewasili hapa naye ameshika kazi yake ya kutufundisha chuoni, pamoja naye amekuja na Mzungu mwingine "schoolmaster." Mr. Viney; na meli hii tumepata taa nzuri kwa kanisa letu. Tena siku kuu hii ilikuwa wakati wa mvua tu wala hatukupata nafuu ya kutembea po pote, lakini karibu Askofu kusafiri kwake, ilikuwa karamu Mbweni, na wote tukaenda tukafurahiwa sana. Na tena May 3 alikufa hapa mpishi wetu, Peter Gamachizi, aliyekuwa zamani mtoto wa hapa Kiungani.

Katika May 3 mwalimu So Songolo amefika hapa, naswi tumefurahi kumwona, naye anakaa hapa anazidi kujifunza kusoma; na pamoja naye amekuja na Mr. Allen anakaa Mbweni, anatujengea "studies" zetu hapa juu ya nyumba ya sermala. Tena mwezi wa May, Austini T. Mabruki na Arthur R. Mvenya wameingizwa kuwa waalimu mahali pa waalimu wawili waliosafiri Newala, nao ni hawa, Yohana B. Abdallah, na Enoch Mtaiwa. Mtg.

MAVUNO MENGI.

Tumeandikiwa habari nyingi za miji ya pwani ya Nyassa inapofanywa na itakapo kufanywa kazi ya kufundisha ndugu zetu wakaao gizani bado. Zimeandikwa habari hizi na So Songolo aliyefundisha huko Nyassa kwa miaka hii minne iliyopita.

William E. Kanyopolea, na Denys Sayite, hawa wawili wafundisha Likoma, mahali pa Murphy Makamla. Kwani Murphy Makamla yeye kaisha oa, kaoana na ndugu yake Eustice, akaaye kulekule Nyassa, naye ni mwalimu, hukaa mji wa Maendaenda pamoja na mwalimu Paul Mambo. Bassi huyu Murphy alipooa hakukaa tena Likoma alipelekwa marra Msumba, mji wa mkuu mmoja Wanyassa

MSIMULIZI 75

aitwaye Masanje, huyu Masanje anao mji mkubwa kuliko Wanyassa wangine hatta karibu miji yote ya Wanyassa kushika miguu kwa Wangoni ndio Makwangwara, isipokuwa yeye Masanje mji wake, kwani Wangoni wamejaribu marra nne hawakuweza kuuteka. Ndio mji akaao mwalimu Murphy na mwalimu Augustine Ambali na mkewe, ndipo nilipokuwa mimi So nikifundisha.

Na tuanze Likoma, twajua Likoma ni kisiwa, pana kisiwa kingine magharibi ya Likoma kiitwacho Chizumulo, kwani twaliacha wakianza kazi ya kufundisha huko Chizumulo. Mwalimu mmoja aitwaye Daudi Kasiya, aliyefundishwa humo humo Likoma akaoa, sasa amepata kuwa mwalimu, anaye babaye, lakini ni mzee kidogo aitwa Ambota, huyu mwalimu Kasiva aenda kuanza kazi Chizumulo pamoja na Mzungu Mr. Williams. Tena tukitoka Chizumulo tukienda Mashariki twaja Likoma mlichosikia marra nyingi habari zake. Tukitaka kwenda mashariki kwa ng'ambo twafika Kobwe, ndio kwa Chitedze ao Chitesi, huyu Chitesi ana jina lingine aitwa Chigoma sababu kakaa kaskazini ya mto ule Kobwe, naye akawashinda Wangoni marra moja tu, akaitwa Chigoma maana yake ngome ngumu. Tena yupo aliye chini upande ule ule alipojenga Chitesi aitwa Mwita ao Mkongojo, tena ukivuka Kobwe kwa kusini yake, utamfikia Mkusa ao Kapito ndio upande wa Mataka, huyo siye Mataka wa Kumwembe, ni wa palepale Pakabwe pwani ile ya ziwa la Nyassa. Nao katika kujenga kwao husonga pwani yake, na karibu sana kwa killa mji ungezungukwa na matete kwa mashariki, kwani hutunza sana matete yawe ngome Wangoni wajapo wakati wowote ijapokuwa usiku, na kwa magharibi yake bahari, na kwa kaskazini na kusini ni milango ya kutokea, iliyozibwa na miti mpaka majini, pangine kuwa karibu sana na maji, ukitokea kwa kaskazini pita mlango wake wa kaskazini, vivyo kwa kusini kwa mlango wake wa kusini. Mashariki hapana mlango sababu

MSIMULIZI. 76

ya matete na matope yaliyokwenda chini sana, ikiwa masika huwa maji tu.

Tusogee kusini kwa Mataka twafika Mbuzi ao pa Njafuo kijiji kidogo, mfalme wake aitwa Mbuzi, mashariki yake hakuna matete, wala maji hayapo wakati wa masika ni mchanga tu. Tena kusini kidogo ni pa Kango mfalme Mtaya, si kijiji kikubwa sana. Tena mbele yake kwa kusini kuna kijiji kingine chaitwa Utonga, Utonga ni kijito kiingiacho Nyassa, watu wamejenga kwa ng'ambo ya kusini ya mto, ng'ambo ya kaskazini katika kanwa la mto buo ni mashamba tu na mji wake umezungukwa na matete. Ukienda robo ya saa utafika rassi ya Marrha, penyi watu haba tu, nyumba zao wamejenga katika visiwa vya miamba, si watu wengi wakaapo pale Marrha wapata 30 tu, hukaa katika miamba hiyo kusudi Wangoni wasipate kuwafikia wakiwa usingizini. Tena ukienda mwendo wa saa unussu utafika kijiji kiitwacho Mbweka. Tena utapanda rassi kuu iitwayo Tumbi, Tumbi ni mlima mkubwa ulio karibu sawasawa juu yake lakini si sawasawa kabisa, tena hawakai watu kule Tumbi, watu huenda kuvua samaki tu na mitumbwi yao wakitoka Likoma ao Mbweka, ao Pangoo paitwapo tena Malila Ng'kandwe kusini kwa Tumbi, Ng'kandwe ndio mbwa wa mwitu, sauti yake ikasikiwa siku moja "Charles Janson" ilipolala pale Pangoo, kwani ghubba yake njema kwa jahazi, ndiyo bandari yake "Charles Janson" hapa Pangoo pana watu wachache tu, waliotoka katika kijiji kilicho karibu yake kwa kusini kiitwacho Chisanga. Chisanga ndio jina la mji na mfalme wake aitwa Manyika, ndipo akaapo Benjamin mwalimu aliyetoka Bandawe katika Mission ya Scotch; sasa kapewa msalaba, kapewa msalaba Juma a pili ya kwanza ya wakati wa Kwaresima. Waalimu wote wafanyao kazi ng'ambo ya pili walikuwapo, na waanafunzi wa Pachia na waalimu wao, na waalimu wa Msumba pia wakawapo pamoja siku hiyo.

MSIMULIZI 77

Isipokuwa waalimu wa Likoma William na Denys, ua mwalimu Daud aendaye Chizumulo pamoja na. Mr. Joseph Williams. Bassi Juma a pili ile ilikuwa siku kuu kubwa, hatta mfalme Masanje alikuwapo kwa hubiri lile alilohubiri Mr. Johnson karibu na nyumba ya mwalimu Augustine kwani yalikotendeka haya ni Msumba. Hatta Juma a tatu tukaagana waalimu wote waliotoka kazini mwao wakarudi kwao, Mr. Johnson akawafundisha wanaotaka kuwa waanafunzi Msumba na kuwafundisha watoto kwa mambo wanayofundishwa na waalimu wao kwa desturi yake, kwani ndivyo afanyavyo kwa killa afikapo bandari yenyi mwalimu. Tena twaingia kusini kwa Chisanga ndipo tufikapo alipozikwa Mr. Charles Janson, alipokaa kwanza akifundisha mwalimu. Augustine billa hajaja Unguja kuoa. Wallakini susa hukaa waalimu hawa wawili Paul W. Mambo na mke wake, na mwalimu yule Eustice Uledi naye na mke wake ha watoto wawili, Paul W. Mambo ana mtoto mmoja. Tushuke kwa kusini kwa Maendaenda twafika Msumba mji wa Masanje wakaapo waalimu wale wawili Murphy na Augustine tuliowataja zamani na wake wao, hawa waalimu hukaa kwa killa mtu na mke wake, mlango mbali kidogo, kama Paul W. Mambo na Eustice Uledi walivyokaa, Paul W. Mambo hukaa kaskazini ya mji ule, mwalimu Eustice hukaa kusini, nao hawafundishi nyumba moja, killa mtu na school yake na watoto wake, na nyumba zao za kulala karibu yao, illa siku ya Juma a pili tu, ndipo huwakusanya watu na watoto kwa mlango wa kaskazini kuwaeleza mambo ya Anjili na Agano la kale, pangine wakiwa na sanamu za kuwaonyesha husayidiwa sana mwalimu yule anayehubiri.

Nussu iliyosalia ya barua hii itatiwa katika Msimulizi ijayo. Mwezi huu hatuna nafasi.

MSIMULIZI. August, 1889. VI.

Imepigwa chapa Kiungani, Zanzibar,
katika "Universities' Mission to Central Africa."

VITA YA WADOICHA.

Vita hiyo inaendelea. Wadoicha waliupiga Pangani July 8, wakaupiga hivi. Kwanza manowari ya admeli ilipiga mizinga mikubwa, kwani walisikia watu wa mji wanavizia wengi, sio mjini mwenyewe, upande wa pili wa mto, upande wa kushoto ukiingia mtoni, katika miamba na rasi vyombo vipitapo karibu. Lakini watu hapana wengi, Wadoicha wakapeleka mashua za moshi wakashuka pale pale mjini, wakakuta watu hawako illa Wahindi tu, nao wameambiwa na Balozi wa Waingereza wakae ndani wasione hofu. Wangineo wote wamekimbia. Bassi Wadoicha waliposhuka Wahindi wakatokea tena. Tena Wadoicha wakateketeza nyumba za fito na za udongo na vibanda, nyumba za mawe hawakuzivunja, illa labuda moja mbili, wakaua watu si wengi. Na nyumba yetu ya Maftaa hatujui habari zake bado, kama nzima, kama imetekwa. Wadoicha wakajenga ngome zenyi mizinga na bunduki za midomo mingi, wakakaa. Hatta tumesikia Waarabu wengi wamerudia nyumba zao na mashamba, lakini Waswahili bado. Tena sisi tukataka kuwapelekea ndugu zetu Magila waraka, tukampa barozi wetu hapa Unguja, yeye akampelekea Captain Wissmann, Captain Wissmann akapata mtu kwa shidda Pangani, akamtuma Magila. Hatta marra mbili naona alituma watu, akatuletea sisi habari kusema, njia ya Magila wazi, hakuna hatari, ndivyo alivyosema.

Baadaye Wadoicha wakapiga Tanga vilevile. Hawakuvunja sana, wala kuua watu wengi, wataka wenyewe uthia huo utulie upesi, wapate kufanya biashara. Tena Bushiri amekimbia mbali. Hatta akafika Mpwapwa na watu kama mia, akakuta Wadoicha wawili wako, akawaendea usiku.

akamua mmoja palepale, wa pili akakimbia akafichwa na watu akaokoka pwani akaleta habari.

Hatta uthia pangine hufaa. Unafaa uthia huo kuwajulisha watu wengi Ulaya na kote kote habari za Upelekwa huu. Mimi nilipokuwako Ulaya, killa siku watu wote husoma habari ya Unguja na vita ya Wadoicha, na kusikia ndugu zetu walivyo hatarini, kwani siku hizi hatari mtu mweupe kusafiri katika barra, na zayidi Magila. Watu wakazidi kutaka habari ya Upelekwa, na kutuhurumia, na kutaka kutusayidia, wakisema 'kazi hii ya Muungu, isizuiliwe.' Hatta askofu mkuu wa Canterbury, ndiye mkubwa wa Kanisa lote la Kingereza, akaondoka akaenda kwa kanisa la London, ndio S. Paul's, akatoa maneno akihubiri kwa watu wengi katika siku kuu ya Upelekwa, hatari ya kazi yetu na tena tusichoke, na kututia moyo tusiache hatta mmoja wa kondoo, ndio waongofu wa barra. Bassi naona uthia huu wa Wadoicha utafaa tusayidiwe zayidi na Waingereza, kwa fetha, kwa sala, na kwa kuja waalimu na makasisi. Kwani wamezidi kujua mahitaji yetu.

SAFARI YA BWANA ASKOFU.

Tukatoka Unguja Juma a pili May 12, tukaingia katika H.M.S. "Mariner". Tulipongoa nanga tukaendelea mbele kidogo tukakuta manowari ya Madachi imetia nanga karibu ya Kwale inayokamata vyombo. Tukaendelea tukalala njiani, watu wote tulioingia katika merikebu tukalewa sana kwa mawimbi, na assubui tukapata nafuu wote. Lakini hatukuingia Kilwa tukapita bahari kwa bahari na tukalala njiani tena, na assubui saa 'nne tukafika Lindi, tukaikuta H.M.S. "Griffon," nasi tukatia nanga ikaja mashua yao kuamkiana na nakhotha. Tukang'oa tukafika mto Ruvuma unapoingia baharini, tukaingia ndani ya hori tukatia nanga tukalala ndio saa kumi; kwani nakhotha akasema tusiingie mjini usiku kwa sababu ya zile habari za

MSIMULIZI. 80

uthia wa Wareno, kwani hatta tulipokuwa tukitoka Unguja tukajua kama labuda itakwenda kuwa vita kati ya Wareno na sisi, na nakhotha akasema, wakifanya jeuri tutakwenda kupateketeza mahali pale. Tukaona ajabu kwa maji yale ya Ruvuma yanavyoingia baharini imekuwa kama boma, maji ya baridi na ya chumvi yanajitenga na hili boma limeinuka kama wimbi kubwa. Assubui tukatoka tukafika Tungi saa tatu na bandari yake nzuri sana, na tulipoingia tukaona huko bandarini manowari nne za Wareno zimetia nanga kwani wamepata habari na wao kama tunakuja, nasi tukaogopa sana, kwani zao 'nne na yetu ni moja nayo ni Mariner iliyo ndogo, tukaendelea kidogo kidogo, tulipotupa macho nyuma tukaona manowari ingine inakuja inatufuata kubwa sana, ikatupita ikaingia bandarini, tena tukatupa macho nyuma tukaiona ingine tena inakuja nayo ikatupita ikaingia, nasi wakati huo tumeshikwa na hofu, kwani manowari zao zikawa 6 na yetu ni moja wala hatukukaribia bandarini tukatia nanga mbali, tukaona mashua ya moshi inakuja akaingia nakhotha wao, akatuambia tuingie bandarini, tukaendelea ndani, tukatia nanga wakaja manahotha wawili tena wakaongea na nakhotha, wakashuka, nakhotha wetu akavalia akaingia mashuani pamoja na askofu wakamwendea liwali wa Mozambiki kutaka ruhusa ya kushuka, kwani hatta liwali akatoka Mozambiki kuja kwa shughuli hiyo tu ya kutuzuia, sio kwa maneno tu, siku hiyo ilikuwa tayari kwa mapigano. Askofu akarudi akasema amenikataza nisimwone leo, kwani akasema sitaki nimjie leo, njooni kesho. Tukalala, assubui akaenda askofu akaulizwa ginsi ya watu waliokuja naye na bunduki ngapi, askofu akasema, nimeleta watu 30 wala hawana bunduki, illa 2 tu, liwali akasema, nikathani wote wana bunduki, bassi nitakupeni ruhusa mtashuka leo alasiri. Liwali mwenyewe akaingia katika merikebu yetu ikapigwa mizinga 12 na katika manovari ya admeli wao. Alasiri tukashuka

MSIMULIZI. 81
na huko pwani nyumba moja ya mawe na askari wa Kireno wengi wanangojea, zamu kwa zamu, usiku asikari wa marikebu tatu na mchana asikari wa marikebu tatu, kwani zipo sita na Wamakua wengi wapo, na minazi na nyumba nyingi zimeharibika walipopapiga hawa Wareno. Mzungu tuliyemjua hatukumkuta, amekwenda Ibo, na nduguye amekwenda katika biashara yake, tukalala. Assubui tukatoka na njiani maji mengi mno, njiani tukalala siku mbili tukafika duka la mzungu yule katika mji wa Msaka, tukalala. Tukatoka hatta tukafika duka lake la pili tukalala. Tukatoka tukafika duka lake la tatu penyi ziwa Nangadi, tukatoka tukalala njiani, assubui tukafika ziwa Lidede tukalala, tukaenda tukafika Ruvuma saa tatu, tukangoja mashua hatta saa kumi tukavuka, nussu tukalala upande huu na nussu upande ule, kwani hatuwezi kuvuka usiku kwa sababu ya viboko, kwani wengi pale tulipovukia. Assubui tukavuka wote tukalala mji wa Wamakonde, assubui Juma a pili tukasali sala ya Usharika Mtakatifu, na baadaye Askofu akawaita Wamakonde akawahubiria na kuwaambia amri kumi na alasiri tukatoka tukalala pa Che Mlipa, na Juma a tatu saa pili tukafika Newala. Y.B.A.

HABARI ZA NEWALA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu. Baada ya salaamu siku hizi tumetoka Mission ya chini. Sasa tunakaa Makonde, nyumba ile imekwisha. Mwezi wa May, akaja Askofu pamoja na Mr. Watson, na Mr. Hainsworth, walifika hapa wote salama salimini, akakaa hatta siku ya Kupaa. Wakafanya mashindano kwa kukimbia na kutupa risasi na kuvutana, lakini Askofu alikuwa hawezi. Juma a pili ya Pentekote walikuwapo watu waliokuja kutiwa mikono, waana wake saba na watoto wa nyumbani kumi na nne, jumla yao watu asharini na moja. Baada ya siku si nyingi akafunga safari kwenda Chitangali, na Mr. Porter

amemsindikiza mpaka Masasi. Siku hizi watu wengi wamekuja kukaa huku kwa hofu ya maadui wale Makwangwara.

Mr. Porter amekwenda kwa Machemba kumweka huko Mwalimu Harry Mnubi afundishe watu wa mji ule killa siku.

Sasa nyumba tulipokaa kwa miaka mingi imeachwa; Mission sasa itakuwa juu ya Makonde tu katikati ya watu; Juma a pili tukafurahiwa kuona watu wengi sana wakakusanyika kuyasikia maneno ya Muungu katika Kiyao hatta nyumba haikutosha na wengi wakakaa nje kuzunguka nyumba. Watoto pia wanazidi kuja kusoma, watazidi tena kwa sababu sasa tumepata Waalimu wawili wema ndio Mr. Watson na Enoch Mtaiwa. Kwa siku nyingi tumeona shidda sana katika school tukikaa pasipo mwalimu, kwani Joseph Mtapakoma amekuwa mgonjwa tangu siku kuu ya Kuzaliwa na leo ugonjwa wake unazidi na mwisho wake hatujui vema, lakini Mr. Hainsworth anamtunza sana, hatujui labuda atapona, hatujui. C.M.

HABARI ZA MLOLELA AO CHITANGALI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Siku hizi tumepata furaha kubwa kwa Bwana Askofu ametufikia salama; tulipeleka watu Lindi kwenda kumlaki lakini tukapata habari kama amepita bahari kwa bahari hatta pwani ya Limenyene ndio Tungi. Alipofika hapa tukafurahi mno, alikuja pamoja na Mr. W. C. Porter na wapagazi wake nasi hapa tuliweka watu tayari kwa Ubatizo, na kwa kutiwa mikono. Akafika hapa Alhamisi June 6, tukaweka vitu vyote tayari hatta Juma a mosi saa kumi, watu wale waliowekwa tayari kwa Ubatizo Wakaanza kuvalia na kutangulia kanisani. Watu wengi wakaja, tukaanza sala hatta baada ya somo la pili tukaendelea hatta kwenyi mahali pa kubatizia, wakabatizwa, nao walikawa watu wazima na wangine na wake zao. Jumla yao ni watu 12, waume 7, na wake 5. Hii ni taratibu ya

MSIMULIZI. 86

majina yao, Isaak Sasu na Sarah Akumchindula mkewe, Habil Malita na Kate Akwitepeyo mkewe, Yonah Malekano na Deborah Achangalila mkewe, Mattayo Sulemani, Samwili Sulemani, Sila Kateyaga, Haruni Boli, Hannah Atugalaga, Salome Akuulinda. Keshoye Juma a pili ya Pentekote wakatiwa mikono wote wale waliobatizwa Juma a mosi na pamoja na watoto waliobatizwa, zamani, jumla yao waliotiwa mikono ni watu 22, na Bwana Askofu akatoa mahubiri kwa watu waliokuja, akawahubiria ginsi walivyo na bahati kupata Waalimu wa kuwafundisha, na akawaambia habari za kujenga kama imewapasa kujenga kanisa wenyewe; kwani hapa sasa tunahama kuwafuata walikojenga wao ng'ambo ya pili ya mto huu Chitangali. Baadaye tukatoka Kanisani na Bwana Askofu akaona vema kusema na watu habari hizo za kujenga kanisa. Harry Mnubi sasa ni Msomaji. Naona kama ndugu zetu watu wa chama watafurahi sana, na Juma a tatu Bwana Askofu akatoka hapa kwenda Masasi, na Mr. Porter akatoka kwenda kwa Machemba pamoja na Harry, kwani yeye atakaa huko kwa Machemba huyo Machemba akikubali.

June 10, watu wengi wamegawanyika, Bwana Askofu amekwenda Masasi pamoja na wapagazi wake, na Mr. Porter na Harry Mnubi wametoka wameenda kwa Machemba, wakaaga kama watarudi siku ya Alhamisi ao Ijumaa. Alhamisi tukatazamia, kumbe hawarudi, Ijumaa kathalika tukamtazamia asije, bassi tukasema labda wamelala njiani, kumbe alasiri tukamwona mtu anakuja akatuarifu kama Mr. Porter amekosa kwa Machemba, sababu amemkata ndevu Machemba. Marra tukamwona Mr. Porter anakuja tukafurahi sana, tukamulizia habari akatuelezea hivi. "Tumefika kwa Machemba hatta siku ya Alhamisi akaja Machemba hemani mwangu tukazungumza, tulipokwisha kuongea, mimi nalikuwa na kisu kidogo cha kukunja, ndani mwake mna visu vingi na mkasi mdogo umo ndani; Machemba akataka kutazama

MSIMULIZI. 84

nikatwaa mkasi nikakata ndevu kidogo za Machemba nikazifunga katika karatasi, nikakata zangu nikampa Machemba akapokea lakini si kwa mkono wake; nikathani kama desturi ya Kizungu ukimpenda mtu hufanya hivi. Baada ya haya Alhamisi ile ile alasiri yake akaja mtoto wa Machemba jina lake Kamtande pamoja na askari zake, naye amelewa akili zake zimempungukia, akaja hatta pahali nilipo, akasema kwa ukali, Hivyo wewe Mzungu, aliyekuambia ukate ndevu za babangu, ni nani? akatapika pale manono wee, hatta mimi nikazirudisha ndevu za babaye, na marra wakaja watu wakanisonga wakaniambia, wewe leo Mzungu kitwa chako halali yetu. Halafu akaja Machemba na watu wake, naye akasema, Umekosa wewe sababu umekata ndevu zangu, unaenda kunifanyia uchawi, mji wangu uvunjike. Kamtande akaja pale akajitapa na kurandaranda akisema, mimi mtanikuta popote mtakapokwenda. Mimi Mr. Porter nikamwuliza, je utakuja Newala kunitazama, akaniambia mimi sikujui kamwe umetokapi, wala mimi sikujui, nikasema, mimi ni rafiki wa Kamtande, naye akakana.

Ijumaa June 14, tukaenenda Chitangali kwa Nakaam kumaliza maneno. June 15 watu wa Chitangali wakakusanyika na wafalme wao na mzee Barnaba Nakaam ndiye mkubwa wao, na maneno yakatolewa mbele yao, na watu wote wakasema desturi hii si njema ya kukatana ndevu, bassi Barnaba Nakaam akasema atamlipia Mzungu.

Kwa Machemba bado hatujajenga mpaka uthia huu uishe. Siku hizi tunashughulika kujenga mji mpya walikohamia wenyeji, bassi tunajenga nyumba kubwa kwanza. Mambo haya ya Machemba Mr. Porter amelipa $ 35, kwani yakawa magumu sana ginsi watu wa Machemba walivyokasirika, kwani wakataka wamwue. M.H.

MAVUNO MENGI. (nussu ya pili.)

Zipo ng'ombe Msumba, si nyingi, kama zile zenyi zipo

MSIMULIZI. 85

kwa Chitesi na Likoma, zipo kwa kadri tu, lakini kwa siku hizi huzidi sana ng'ombe kuzaa kwani kwanza walikuwa nazo nyingi, lakini Wangoni wakaja wakateka, na vita hiyo wanaita nkondo ya Kaindi ndio watu walioteka ng'ombe zao Zamani.

Tena wakitaka kukata kuni sharti waende watu wengi kwa hofu ya Wangoni, kwani Wangoni hawapendi watu wa Msumba waende safari ao kutembeatembea inchi nyingine sababu wamekataa kushika miguu kwa Wangoni ndio maana. Wangoni hawapendi kuwaona watu wa Msumba, wakiwaona tu inakuwa kuuawa bassi, na sababu nyingine kama tulivyosema sababu Wangoni wameleta vita wameshindwa, bassi Wangoni hawa huona fetheha sana, hatta wakitaka kuwaonea watu wa vijiji vingine walivyoteka, watu huwajibu nendeni kawaoneeni watu wa Msumba, ao mkizidi kutuonea tutakimbilia Msumba, wakisikia jina la Msumba tu, marra moja hunyamaza kwa kuogopa, kwani watu wa Msumba wakali, nao watazidi kupata nguvu watu wa Msumba wakipata watu wengi sana kwao, hatutapata kuwafundisha vema. Tukiingia kusini kwa Msumba twafika Mtengula, pana kijiji kimeanzwa mwaka huu 1888, kwani mwaka ule 1886 Wangoni walikuja kuharibu, sasa watu wamerudia na kujenga kwa ruhusa ya Makwangwara, upo mto waitwa Lichomanje anapokaa mfalme Ghilombe.

Sasa twafika Kuchikole mji wa Wayao mfalme wake Chingomanje, bandari ya Nkota-kota ng'ambo akaako Jumbe. Tena ukipanda juu kwa mwendo wa saa wafika Ngolokolo, kijiji cha mfalme Manyamba, wapo tena watu wa Masanje hukaa na hawa Wayao nao wamepata mahali wanapaita Kumwela, ndipo wakaapo watu wa Masanje.

Ukishuka kusini kwa Magharibi, ukishukia pwani ya ile Nyassa wafika Mluluka, mji wa Wanyassa. Kusini kwake wafika Lusewa mji wa Wanyassa. Kusini kwake kwa mwendo wa saa saba wafika Mapanje mji wa Wayao, mfalme

MSIMULIZI. 86

wao aitwa Mdoka. Kijiji kingine kiko pwani ya Nyassa kando yake kijiji kingine milimani, kwani Mapanje ni jina la mlima, mwaka wa 1887 wakagombana huyu Mdoka wa Mapanje na Makanjila sababu ya Lusewa kwani Makanjila akatoka Kizunguro ao Kumpilipili ndio majina ya mji wake haya mawili, akapita nyuma ya Mapanje akafika hatta Lusewa akawapiga watu hatta akashinda, akachoma majumba akatwaa mateka, watu na mbuzi, na wangine wakauawa palepale Lusewa, wangine wakakimbilia Msumba kwani yeye mwenyewe Makanjila husema kama atawala tangu pake Kizunguro hatta Lusewa, walakini walipokuwa wakirudi, yule Mdoka wa Mapanje, akatwaa watu wake wengi wakashuka milimani, wakaenda kuwangojea watu wa Kumpilipili, walipokuwa wakipita wakapigana nao akawanyang'anya nussu ya mateka yao. Halafu yake yule Makanjila alipopata matata yale ya njiani, akasema "Ah! yupo mtu awezaye kunizuia kwa kitu nipendacho? Yupo mtu mbele yangu awezaye kupigana nami? Ah! ataona huyu Mdoka."

Akapeleka watu kwa Kalanje Unangu kulalika vita, akapeleka watu kwa Chingomanje, halafu wakapatana kumpiga Mdoka, wakaenda kwa vita hiyo wakampiga na mji wake wa chini ukachomwa moto, lakini wa juu hawakuchoma, wakarudi; halafu yule Mduka akataka kupatana, na Makanjila akasema, akitaka kupatana nami sharti waje kujenga karibu yangu hapa, Ghitepete na wewe Mdoka, wakakataa.

Halafu akaona wanakataa, akamwambia, vyombo vyako Mdoka lete huku iwe bandari hapa pangu, Makanjila akatwaa vyombo vya Mdoka, akasema sababu vyombo vyako na ng'ombe nimetwaa, haithuru kaa kwako huko huko, na Chitepete arudi kwake Lusewa wallakini sharti walete ng'ombe, sasa walakini hawajapatana halisi, kwani hawaaminiani sana huapa kama

MSIMULIZI. 87

atakuja kupinduka na kuja na vita tena, Chitepete akarudi Lusewa. Baada ya kuanza kujenga masakasa ya kujenga nyumba zao, wakaja Wangoni wakapigana nao, Wangoni wakakimbia, watu wakafa wanne na wangine wakajeruhi, na Maviti wakafa wawili wangine wamejeruhi kwani walikuja Wangoni wa vifamba tu, hawakuja haswa wapinga vita; ngao walizonyang'anya wakapeleka kwa Makanjila Kumpilipili, kunena tazama Bwana pale ulipotupa ruhusa walikuja Wangoni tumewafukuza.

Tena twende kwa huyu Makanjila kwani kwa Mapanje ndio hutawala yeye hatta mpaka wake kabisa na Mkata karibu na mlango wa Shire penyi milima iitwayo Mangochi, si mbali sana na ng'ambo ile alipojenga Mponda, penyi unaposhukia mto Shire ukishuka toka kwa Mponda wafika chini yake kwa Nyanja yaitwa Marombe, maji yake hayakwenda chini sana, bassi katika mji ule wa Mkata, hutaka mwalimu, kwani Makandaje ndio aliye pwani mkubwaye Makandaje Mkata akaa mlimani.

Chini yake ya Makandaje na Mponda ukipita chini kabisa ya Nyanja ya Malombe, ukiingia tena mto Shire utaona vijiji vidogo vidogo kando ya mto, anamoshuka Mr. Johnson na kufundisha watoto, na wakubwa wafanywe waanafunzi. Ushuke tena wafika kisiwa katikati ya mto Shire akaamo Lionde walipopewa ruhusa Charles Janson alipokwama wafundishe pale ya kisiwa cha Lionde, paitwa Patsapa, walipotoka wale waalimu Augustine, William na Denys walimwachia nyumba mtu mmoja wa Masasi, aliyetoka Mbweni aitwa John Padyera, hutunza nyumba yeye na mkewe, na sababu hawajui kusoma wamepata ruhusa ya kulima karibu na school ile, mpaka afikapo mwalimu atakayefundisha pale, wameachwa watoto waliojaribu sana kusoma, waliofundisha na waalimu wale wawili William na Denys walipofundisha hawakuanza kuendelea juu sababu ya kupungukiwa maji ya ule mto, walipopata maji wakaweza kupanda

MSIMULIZI. 88

juu wakaacha kazi ya pale wakaendea kazi ya Kunyanja. Bassi mabwana wa kule hutaraja sana kama marra watapeleka waalimu kwa miji ile iliyo gizani, haswa watakiwa upesi kwa miji hii mitatu sasa, kwa Lionde, Makandaje, na kwa Mdoka; kwani miji yao hawa ni Wayao wala hutaona Wanyassa wengi katika miji yao hii, kama kwa Masanje, Lusewa, Mluluka, Maendaenda, Chisanga, Pangoo, Mbweka, bassi Marrha, Utonga, Pakango ao huitwa Mbuzi, Mataka, Chitedze, Mapunda, Likotua, na Chizumulo. Mr. Johnson kwa killa mwezi hupita katika miji hii kwa kazi kubwa kuwafundisha wakuu kwa kuwaonyesha sanamu, hukaa vibandani wanapofanyia kazi zao hukaa chini nao na huanza kuwafundisha, na kuwaita majina yao waliopeleka majina waandikwe, ajapo awafundishe wapate kuwa waanafunzi, akifika kijiji cha mwalimu, kuwafundisha kwanza wakubwa bandani, ndipo wanapofanya mashauri yao na hukumu zao wakoseanapo waonyesha nani aliyekosa. Hawa wafalme watatu wameulizwa, wamesema wataka sana waalimu, wao wenyewe wanao waalimu wao wa Kiislamu hufundisha pale hatta wangine hujia sana kusoma Kiarabu kwani ndimo wanamofanya biashara zao kwa Makanjila, Makandanje, Mapanje, &c.

Na tujitahidi kwa kadri tulivyopewa talanta na Bwana tukafanye biashara nazo kwa wenzetu walio gizani ndani ya Afrika, haitaki akili tu, yafaa sana kuwa na akili lakini juu yote "Mwanga wetu waangaze vizuri mbele ya watu hatta waone vitendo vyetu vizuri wamtukuze Baba yetu aliye Mbinguni. (Mattayo v. 16.) kama tunavyoimba katika Nyimbo:-_-

"Bwana upeleke wengi walitoe neno, Wengi hawajasikia neno la Anjili." Bassi, tuwafikirie ndugu zetu walioko bara kama watu wema weupe walioko Ulaya, wanavyotufikiri na kutusayidia sisi kwa ndani na kwa nje. S.S.

MSIMULIZI. 89

MAGILA.

May 11, siku ya Juma a mosi tukapata habari nzito sana iliyotoka Mkuzi ya kufa kwake Mr. Geldart, kwa ugonjwa wa siku tatu, na Archdeacon Goodyear alikwenda Misozwe siku ya Jumaa, na kurudi kwa siku ya pili yake ndio Juma a mosi alipowasili hapa Magila marra alifikia habari hii, asipate hatta kituo akafuliza kwenda Mkuzi mazikoni, akaenda na jua kali sana, hatta kwa alasiri yakawa maziko. Tena kwa mwezi huu mmoja wa May baada ya kufariki Mr. Geldart Juma a mosi iliyofuata ndugu yetu mwingine akafariki ndio Annie Madeline Azama mkewe Lawrence Turi, akafa May 18 assubui, jioni tukamzika: Tena kwenyi May 29 siku ya Juma a tatu iliyo maandalio ya Siku ya Kupaa, kama kesho ndio kupaa, leo usiku ndio akafa mamaye Hugh Peter Kayamba, jina lake Elizabeti Makayamba, siku ya pili iliyo siku ya Kupaa tukamzika.

Na kwenyi June 18, ndio Juma a tatu baada ya Pentekote, yalikuwa machezo ya kushindana mbio, na mashindano ya kuchupachupa ndani ya magunia, na ya mbio za miguu mitatu, tena ikawa ya kuvutana kwa kamba waalimu na watu wa kazi, watu wa kazi wakashinda, na tena michezo mingine mingine. Siku ya Juma a nne baada ya Pentekote ukawa mshindano wa mpila wa mateke (football) kati ya Magila kwa miji miwili, Mkuzi na Misozwe pamoja, kwa killa upande watu edashara, na wakubwa wa killa upande ni hawa, upande wa Magila ni Leonard Pesa, na upande wa pili ni Philip Yahom.

Walakini ingawa watoto wa Mkuzi na Misozwe wameshindwa na wa Magila illa twawapa haki, na tena twawasifu kwani wamepigana kiume sana hatta wamepata kuingiza moja kwa kadri yao nao karibu wote waana wa Kibondei watupu isipokuwa mtu mmoja mwalimu wa Kiungani, mtaona

MSIMULIZI. 90

jina lake hapo mwanzo ndiye aliyekuwa msaada wao, illa upande wa Magila angawa wana wengi watoto wa Kiungani msaada wao, tena hawa wa hapa wamezoea siku zote kucheza kwa killa Juma a tano alasiri. Na kunako Juma a mosi June 15 tulikwenda Mkuzi kuweka jiwe la pembeni la Kanisa lianzalo kujengwa kwa siku hizi tu, Archdeacon Goodyear akasoma sala zote, tukaanza Usharika Mtakatifu, baadaye tukaenda kuweka hilo jiwe na Bwana Woodward akahubiri, kueleza maana ya nyumba hii ijengwayo na fayida yake, na matumizi yake. Na juu ya haya yote mtu hawezi kuzuia machozi kwa jambo lililotupata kwenyi June 24, la kufariki kwake Archdeacon Goodyear kwa ugonjwa wa siku tatu tu, ya nne akapumzika katika Bwana, tumevunjiwa sana hapa, twamwomba huyu Msimulizi awaambie wote wasikiao shauri lake mwingine.

Siku ya Juma a tatu July 8, assubui saa ya pili tukasikia kitu kama mizinga ao ngurumo, hatukutambua mojapo ni lipi, wangine wakasema hili wangine hili, hatta jioni ndipo tukapata hakika kama ni Wadoicha wameipiga Pangani wameitwaa, na manuari ziliopiga ni tatu, lakini hatuna hakika ya watu waliouawa, twasikia ati ati tu bassi, na twaona hatuna hatari kwa Waarabu na watu wa Mrima kuja huku kwetu kama kujilipa kisasi, kwani wao wenyewe waandika barua kwetu, wanaomba tuwakaribishe hatta uthia huu uishe, walakini twawaambia hatuwezi kuwakaribisha, kwani na sisi tu wageni inchi hii, tumekaribishwa, na shughuli yetu inchi hii ni ibada, wala hatuna ugomvi na mtu awaye yote si Mwarabu wala si mshenzi, tumewaambia wakipenda wafanye mashauri na majumbe wa inchi, wapate kuwakaribisha wakae, lakini twaona majumbe hawatakubali kwani inchi hii hawawataki Waarabu wakae nao, kwa hofu ya kufanywa watumwa, bassi hatujui hatima yao mahali gani watakaposakini haswa. Na tena

MSIMULIZI. 91

nakuarifu ya kwamba hesabu ya Msimulizi zijazo huku zipungue, zije kama arobaini tu, kwani safari hizi mbili nyingi zimebaki na hasara sijui kama itanilazimu mimi ao siyo. Tena ongeza majina haya ya waalimu hawa, Lawrence Kingodi asomesha katika mji wake mwenyewe ndio Kiole, na hapa petu George Songolo na mwanamke mmoja Sybil Mambo. A.M.

HABARI ZA MKUZI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Habari za Mkuzi siku hizi tangu safari ya mwalimu Granville na watoto wa mwalimu mkubwa ndio J. Swedi, walikuta mshindano wa wila (ndio mchezo wa Kibondei) Kidungwe na mtu mmoja Msambara anakwitwa Bushiri, ilikuwa mwezi huu wote wa May mchezo tu. Ulipokwisha mwalimu mkubwa naye akafanya shelehe ndio furaha kwa watoto wake na zayidi kwa Maryamu aliyekamatwa Kipumbwi kwa uthia wa Madachi; ngoma ya siku mbili, kiyao. wila, dandaro.

Kwa siku kuu ya Pentekote watoto walikwenda Magila kwa mashindano ya mpila, wamerudi Jumaanne jioni. Kanisa la Mkuzi amekwenda twaliwa Archdeacon Goodyear kuja kutia msingi, ilikuwa June 15, walikuwapo waalimu wote, Archdeacon Goodyear, Mr. Woodward, Mr. Sparks ndio makasisi, na shemasi wawili mwalimu John Swedi na Mr. Mercer, na Ackworth Machaku msomaji, Mr. Woodward ndio aliyehututubu Kibondei siku hiyo, na watu wote wa mtaa wa Mkuzi wakafurahiwa kuona mwanzo wa kanisa lao.

HABARI ZA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu. Baada ya salaamu ninakuarifu kama Juma a nne July 2, lilikuwa kusanyiko la Chama cha Watakatifu, Archdeacon Bateman ndiye aliyekuja kuwafanyia sala, wakati wa kuenda kanisani walipita wakiimba njiani.

MSIMULIZI. 92

July 3, Mr. na Mrs. Wallis wakafika hapa kutoka Buki, kwani walikwenda huko kubadili hewa, wamesema ni mahali pa zuri sana. Hatta assubui yake siku ya Alhamisi July 4, Mr. Key akaenda zake Ulaya. July 16, Ilikuwa siku ya Chama ya Mchungaji Mwema. July 25, tulikwenda shambani la mama yetu Miss Thackeray, tukashinda kuko huko, jioni tukarudi, tena tulipokea shanga kuko huko inayotoka kwa Mr. Musworthy. M.M.

HABARI ZA SHAMBA LA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu, mtu mmoja wa huku jina lake Charles Nyama amefiwa na mkewe June 21. Tena June 23, mwanamke mmoja akitwanga, akaja mwanamme mmoja kwa jeuri akamtia jeraha kwa kisu kiisha akakimbia asipatikane hatta leo. Mtapenda sana kusikia habari za watoto wawili wa hapa waliopotea, lakini sasa wameonekana, majina yao Hamisi, na Kalumpa. July 8, Jioni walienda pwani na kule pwani kuua wachuuzi samaki, wakawaita wawasayidie kupaa samaki, kiisha wale watu wakafanya shauri la kuwaiba, bassi mmoja akamwambia mwenzake, mimi nitaenda kule, nawe uwatwae uwaambie twendeni kokoni mkatwae samaki. Bassi wakafanya kama walivyosema, wale watoto kufika tu kokoni walikamatwa watiwe utumwani, naswi jioni tukawatafuta hatukuwaona, tukaenda Kiinua Miguu wala hawako, July 9 tukawatazamia wasije. Kumbe watoto usiku ule wakachukuliwa kuuzwa mbali kupita Mwera, kunakwitwa Pango Nguruwe. Mtu aliyewanunua kule anao watumwa wengi, na wale watoto wakakaa siku nne kule kwa bwana yule. Wale watoto wawili walitoroshwa na mtoto mmoja naye mtoto yule aliibwa pia zamani kidogo katika Mission ya Wafransa, July 12 hatta 13 wakafika Mwera kwa mtu mmoja jina lake Buheri wadi Ambali akawauliza mmetokapi? Wakamwambia, tumeibiwa Mbweni

MSIMULIZI. 93

na sasa tunatoroka, yule mtu akawapa chakula, kiisha akawaleta hapa Mbweni July 14, na mtu aliyewanunua aitwa Sayidi. Bassi wazee wa wale watoto Wakafurahiwa sana kuwaona watoto wao, nao wamekuja na yule mtoto aliyewatorosha. Majina yao waliowauza wale watoto, Wadi Juma, na Heri, nao wamekamatwa wamefungwa kifungoni, na yule mtoto amerudishwa kwao Mission ya Wafransa.

HABARI ZA KIUNGANI.

Juma a tatu baada ya Pentekote June 10, hapa Kiungani palikuwa mashindano ya mpila wa vibao "cricket," tangu saa pili unussu ya assubui hatta saa tano, na mshindano wenyewe ulikuwa pwani ndogo ya Kiungani.

June 13, tulienda kushinda Bawe watoto wote wa chuoni, pamoja na Archdeacon Jones-Bateman, Mr. Matthews, na Mr. Allen, mashua sita tukaenda nazo, na tulijaribu kutafuta paa wallakini hawakamatiki sababu ya miiba mingi, na jioni tukarudi. Siku mbili tatu zikiisha Archdeacon akatuarifu kama tutafanya mchezo majira ya usiku, bassi akatueleza habari za mchezo wenyewe ginsi utakavyokuwa. June 25, tukaanza kucheza majira ya saa kwanza ya usiku, na mchezo wenyewe unaitwa Evano.

July 1, meli ya Ulaya imekuja pamoja na Mr. Madan, na Mr. Smith Padre aliyekuja Unguja zamani kidogo, na Mr. Dale naye ni Padre pia wallakini ni awali kufika Unguja; naswi tumefurahi huwaona, na Mr. Madan anakaa hapa mahali pake pa zamani, na Mr. Smith amesafiri Newala, na Mr. Dale anakaa hapa Kiinua Miguu. Peter Limo msomaji July 4 amesafiri kwenda Ulaya. Tena mchezo ule wa Evano twaliucheza marra ya pili July 10, nao ulistawi kuliko marra ya kwanza.

July 15, ugonjwa ukamwanza Archdeacon Jones

MSIMULIZI. 94

Batemah, naswi tunahuzunika, wallakini tufanyeje, illa yote haya yawezekana kwa Muungu, bassi siku hizi zote ameugua hapa, wallakini July 26 amepelekwa Mkunazini ajaribie hewa ya kule. Naye anaenda Moris meli hii ya mwezi wa August. July 18, palikuwa kutazamiwa darasa nne 'Examination' na mwenyi kutazamia ni Mr. Madan, muda wa siku tatu.

Nao walioshinda darasa ya kwanza ni 1. John B. Mdoe, 2. Hugh S. Mtoka, 3 Martin Furahani, na katika darasa ya pili 1. Coastantine Mgoma, 2. Archie A. Semmanyi, 3. Nicholas Kusi. Na darasa ya tatu 1. Julius Mkwaya, 2. Alban Njengune, 3. Charles J. Mkumbukwa, darasa ya nne 1. Rikardo Sulemani, 2. Petro Sulemani, 3. Henry Msopola.

Tumesikia ya kuwa marra ilipoenea katika Ingereza habari ya Archdeacon Goodyear alivyofariki, Bwana Ellis-Viner akapata ruhusa kwa daktari kufanya safari kuturudia, Bassi sasa yuko njiani kuzunguka Kepi, atafika labuda mwisho wa September. Tena akiwapo naye doktari mwingine mahali pa Dr. Ley, watafurahiwa sana Magila, na sisi pia.

Na habari ya Archdeacon Goodyear alipofariki ndio hii? Alikuwa na kazi nyingi, akazidi kuwa kama baba wa Waboondei kuwatunza kuwaongoza kuwachunga. Kazi yake ya mwisho alikwenda Mkuzi akafanya dini kubwa ya kuweka msingi wa kanisa jipya la mawe litakalojengwa pale pale, akarudi Magila akaanza kuugua, asitake kulala, mpaka Alhamisi hana buddi kulala, homa ikazidi siku tatu.

Juma apili ndio June 23, Wazungu wa Mkuzi na Misozwe wakaenda kwitwa wakaja Juma tatu, siku kuu ya Yohana Mbatizaji, wakamkuta amezimia roho, wakakaa hatta Jioni wakimwombea, saa tano ya usiku akatoa roho akastarehe

katika kazi zote. Jambo hilo kubwa na lenyi huzuni, kufiwa na watu wawili hao marra moja Bwana Geldart na Bwana Goodyear walio hodari na kupendwa na kutuzoelea sana. Kazi itaendeleaje? "Si kwa nguvu wala kwa uwezo, illa kwa Roho yangu, asema Bwana wa Majeshi." Tumshukuru Yeye.

Hatta huku Kiungani tunapo huzuni yetu. Kwani siku hizi Archdeacon Jones-Bateman ameugua homa sana kama zamani, baada ya siku akachukuliwa Mkunazini akapata hajambo kidogo. Hatta Aug. 4, ameingia meli ya Kifransa amekwenda zake Moris kubadili hewa na apate afya na Miss Townshend amekwenda kumwuguza njiani. Twatumaini atapata kuturudia baada ya mwezi.

Kinanda kipya cha Kanisa! chetu cha Kiungani kinajengwa na Mr. Allen, kikubwa na kizuri.

Constantine Mgoma, na Archibald A. Semanyi, na Nicholas Kusi wamekuwa Waalimu, nao wa darasa la kwanza sasa.

Tumesikia habari ya Magila kidogo tu, kwani barua zapotea kwa uthia wa pwani. Lakini hawajambo. Na Bwana Woodward ameingia kuwa baba mahali pa Bwana Goodyear.

HABARI ZA NYASSA.

(Barua hii ya W. E. Kanyopolea, hatukupata nafasi ya kuiingiza katika 'Msimulizi', lakini tumeipiga chapa tukakuletea, upate kufurahiwa nayo.)

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu, Baada ya salamu nakuarifu, ya kuwa sisi ndugu zenu tumewaasili salama huku Nyassa halisi, kwani pale nilipokuandikia zamani jina lake Ntsapa ni mahali tu tulipokwama ao iliposakama merikebu yetu. Bassi hapo tumekaa wee hatta tukataka kwenda kutazama mbele. Hatta panapo mwezi wa February Bwana akatupa neema akatuletea mvua, bassi nahotha akasema, afathali tujaribu kupita; bassi tukajipakia sisi na vitu vyetu, hatta kufumba na kufumbua siku ya pili yake tuko Ziwa la Malombe, marra tukaingia Nyassa halisi tukaenda wee hatta panapo siku ya Alhamisi tukakaribia mji wa Msumba, hapo akaapo zamani So. Bassi

Mr. Johnson akasema, naona yafaa mimi William na Benys tukae hapo, kwani So anakwenda zake Unguja. Bassi sisi pasipo tofauti tukakubali, tukafika hapo mahali tukashuka vitu vyetu na sisi wenyewe, Augustine na mkewe wakaenda zao Likoma. Aruffo hayupo pamoja naswi kwani tumemwacha Matope. Bassi wasikia sana tukakaa hapo hatta merikebu ilipokuja kutoka Likoma marra akaja Mr. Johnson akasema, twendeni Likoma, mwahitajiwa huko na Archdeacon, hapo Msumba akamleta Augustine Ambali yeye na Murphy kukaa hapo badala yetu sisi. Bassi aliposema vile Mr. Johnson tukalala papo hapo siku ile, kwani akasema kesho ndio siku ya kwenda, bassi usiku uleule wakaja wevi wakaiba mablanketi mawili ya So na kasha moja la Denys lile la mti, na kanzu yangu na msako wake pamoja. Bassi assubui tutazame twaona vitu vimekwenda, tufanyeje hatuna neno. Bassi tukajipakia merikebuni na tukamwagiza Augustine ajaribu kumshurutisha mfalme wa hapo atume watu wake kutafuta wevi hao. Na sisi tukaja zetu Likoma, na wakati tulipokuwa tunakuja Likoma tukapita miji mingine walimokaa ndugu zetu, kama Paul Mambo na mkewe na Eustace na mkewe, na wangineo, wote hao walikuwa hawajambo, illa mke wa Paul naona hawezi. Bassi tukaenda zetu moja kwa moja hatta tukafika Likoma siku ya Juma a mosi February 29,1889, ndio tukafika Likoma. Hapa tukakuta wote hawajambo, na mabibi wale waliotuacha nyuma wote hawajambo kwa kadri yao, na Archdeacon Maples yupo salama salimini. Tukafurahi kwa kadri kama tuwezavyo, wallakini Mr. Warner yule aliyekuja na Archdeacon Jones-Bateman, yeye tumemkuta hawezi sana yupo kitandani. Tukakaa wee siku ya Juma a nne March 2, mpenzi Murphy Makamla akaoa, na mchumba mwenyewe jina lake Sarah Poyaga, akaoa kama huko Mbweni wallakini haipiti huko, kwani hapana ghasia ya watu kama huko. Wallakini wakafurahi kama wawezavyo: baada ya haya, wakataka sasa kwenda kwao Msumba ndiko wakaako, lakini merikebu ikawa na shughuli ya kumpeleka Mr. Warner kwa Bandawe, ndio upande wa pili wa ziwa, (kwani kama nilivyosema hawezi) bassi akaenda huko kwa mganga, bassi merikebu ikarudi. Siku ya Alhamisi March 4, ikawachukua akina Murphy na mkewe na mke wa Augustino wakapelekwa Msumba, na baada ya kuwapeleka hapo, ikaenda zake

pande za chini ya ziwa hatta sasa mwezi wa April haijarudi, hatufahamu kwa sababu gani, illa twatazamia tu. Bassi habari za nyuma huko baada ya merikebu kwenda huko chini, na kuwapeleka ndugu zetu So na Mr. Allen wajao huko Unguja ni hizi. Archdeacon amefikiri kama yafaa katika kisiwa kingine karibu na hapa Likoma, kujenga nyumba na kukaa huko mtu wa kuhubiri Anjili ya Bwana, na jina la kisiwa hicho Chizumulo, na zinajengwa huko nyumba kama tano ao sita; na siku moja nalikwenda huko kwa mashua, bassi nilipofika huko, tukatafuta nafuu tukala na baadaye tukafanya kama kutembea. Bassi mimi nikamtwaa mtoto mmoja kutembea naye jina lake Ngoma nikijaribu kumuliza kitu hanisikii, illa kwa neno moja moja tu, bassi ilikuwa kazi yetu kusema kwa mikono na ishara zingine na mimi nikawa kama mjinga tu kwani hatusikiani hatta kidogo, mimi nikafikiri hadithi ya "Mohammadi Mtepetevu" pale alipoangukia baharini akaokotwa na wavuvi, walipokuwa wakisema naye hawasikilizani. Bassi sisi twalikuwa hatusikilizani illa kwa neno moja moja tu, kwani watu wa kisiwa kile hunena Kinkamanga, na mimi nilipo ndio kwanza najifunza Kinyassa, bassi havipatani. Archdeacon Maples siku moja alienda Bandawe ndiko aliko Mr. Warner kumtazama kama hajambo ao bado, (kwani nimesema kama alikuwa hawezi sana), bassi akaenda Bandawe kwa daktari. Bassi akakaa huko kama siku moja hatta siku ya Juma a mosi jioni, akarudi, kwani alitoka hapa siku ya Juma a tano, Bassi akatuarifu habari za huko yakuwa "Mission" hiyo inaendelea sana toka wadogo hatta wakubwa, wanahitaji sana kusoma elimu ya chuoni, Jumaa pili Archdeacon alihubiria watu maneno hayo, na kuwaambia kama twataka watu wa Likoma nao pia wasikie maneno ya Anjili na kuleta waana wao kwa chuoni kupata elimu, na tena akasema labda baadaye ndipo itapata kufanikiwa na kusitawi kama huko Bandawe.

Juma a tatu tukasikia habari ya kuwa mfalme Kitedzi amepokea bandera ya Wareno, na wafalme wangine pia, bassi panapo Juma a mosi Archdeacon na watoto wangine na Denys wakaenda huko upande wa Chitedzi kumtazama na kuuliza habari ya bandera. Bassi marra alipofika tu, marra watu wakamtwekea bandera ya salaamu, ile ile ya Wareno, kwani huyo Mreno aliyewapa aliwaambia, kama killa afikapo Mzungu yeyote watweke, nao wakafanya. Na akamwagiza

mfalme Chitedzi ya kuwa Juma a nne aje wafanye mkutano na kusema vizuri maneno hayo. Wakaja zao wakafika hapa Likoma usiku, sisi tuko kanisani.

Wakakusanyika watu wa humu? Likoma na watu wake aliokuja nao, wakasema maneno yao hatta wakaisha, siwezi kukuambia yote, kwani sisi tulikuwa chuoni tunasoma, yaliyo haba ni haya. Sasa mfalme ataka kurudisha kwa Wareno wenyewe, na aliporudi kwake baada ya siku mbili tatu tukasikia safari ya kwenda Kuchiwambo ndio Quilimane, ndio neno la huku, tangu chini ya mto Shire na Zambesi wote hujua Kuchiwambo tu. Bassi safari ikatoka, lakini baada ya kwenda siku mbili tatu wakatumwa wajumbe kuirudisha, kwani wasema vita ya Makwangwara inakuja, na sasa wamerudi wapo pao, na wamepelekwa wajumbe wanne kwenda kwa Makwangwara kuuliza kama vita inakuja kweli, ao ni ulimi wa watu tu. Ndiyo niliyoyasikia kwa masikio yangu.

Huku nyuma nimesema kama Charles Johnson merikebu haijaja iko huko chini, bassi siku ya April 8 "Delta boat" ndio mashua ya chuma ya matanga, ikaenda zake Bandawe kumtwaa Mr. Warner (kwani nalisema kama yuko huko), bassi panapo siku ya Juma a nne ikatokea Charles Janson na tukafurahi sana, kwani hatta barua za huko tutapata. Tumepata, walakini mbona kidogo barua zenu? Naswi tumefurahi na tumeshukuru. Bassi panapo siku ya Alhamisi Charles Janson ikatoka kwenda Bandawe kupeleka mizigo na barua za huko ilizotwaa Matope, baharini akakutana na mashua ile, lakini wao wakaenda, na hawa wakaja pamoja na Mr. Warner, naye hajambo wallakini naona anakwenda zake Ulaya, kwani homa imemshinda. Bassi Charles Janson imerudi siku ya Ijumaa jioni, hatta ya siku Juma a mosi ikatoka imekwenda zake chini, kuwaangalia waalimu, naona atakuja nao kwa siku ya Juma kuu, ao siku kuu ya Pasaka, hizi ndizo habari. Na Wazungu, mabibi kwa dakika hii wote hawajambo. Waalimu wamekuja lakini ni haba sana kwani ni Murphy na Benjamin tu (huyu na mwalimu wa kukuhuku). Bassi wangine wako kwao, na sababu zao ni hizi:-_-Augustine na mkewe hawawezi wote wawili vifua na ugonjwa mwingine. Paul W. Mambo, na Eustace, sababu vita mjini pao, bassi wanajaribu kuwakalisha watu mjini pao. Aruffo yupo Ntsapa chini kabisa, karibu na Matope, hawezi kuja huku, kwani

merikebu haifiki huko. Na hawa wawili walitoka zao hapa marra ilipokwisha tu Juma kuu, siku ya Juma a mosi, April 20. Na habari za Pasaka njema sana, tumecheza na tumefurahiwa, sana kwa Juma nzima. W.E.K.

MSIMULIZI. October, 1889. VII.
Imepigwa chapa Kiungani, Zanzibar,
katika "Universities' Mission to Central Africa."

HABARI NJEMA KWA AFRIKA PIA.

Jambo kubwa mno ajabu limefanyika mwezi huu September, 1889. Barozi Mwingereza na Barozi Mdachi wamefanya shauri na Seyidi Khalifa, naye Seyidi amekubali maneno yao. Bassi siku hizi ametoa khati kubwa kutangaza habari, kama tangu siku ya kwanza ya November hii ijayo mtu ye yote aingiaye katika inchi iliyo haswa milki yake Seyidi, huyo amekwisha kupata uhuru ametoka mtumwani. Maana yake, tangu Nov. 1, hakuna watumwa tena katika Unguja na Pemba na Mafya na pangine illa wale waliokwisha kuwapo zamani. Hakuna zayidi. Bassi baada ya miaka si mingi, utumwa utakoma pia katika pande hizi. Habari hii njema ikaenda Ulaya upesi kwa simu, Mfalme wa Ingereza akampelekea Seyidi jibu marra moja la furaha na kumsifu, kwani ndiyo bora, watu wasiuze wala kununua watu wenzao.

VITA YA PWANI.

Hakuna uthia sana wala kupigana siku hizi, lakini bado kwisha wote. Wadachi wa Pangani waliuthika na watu wa Madanga, mji katika njia ya kwenda Magila, wakawafukuza, nao wamepotea mbali mbali katika Boondei, hawana shauri, njaa tu na kuomba. Tena Mdachi mkuu wa Tanga amekwenda Magila kumwamkia Mr. Woodward, akaleta wenziwe kenda na asikari wa Misri arobaini. Wakakaa kidogo wakala wakalala wakatoa maneno mazuri, wakatenda kwa adabu, wakataka tupite siku zote njia ya Tanga, na kupata vibarua wa mshahara kutenda kazi kwao Tanga. Wakaenda zao illa wawili walikuwa hawawezi. Wakakaa kidogo, wakaenda nao pia.

MSIMULIZI. 97

Mambo ya Magila thaifu sana siku hizi. Huko Kasisi mmoja tu peke yake katika Boondei, ndio Bwana Woodward. Tena Bwana Mercer yuko Mkuzi, Kasisi hapana. Na Henry Nasibu peke yake Misozwe, na Granville Msaraka. Hatta Bwana Wride amekuja zake Unguja kupata afya. Tena Mdachi mkuu, Capt. Wissmann, amefunga safari kubwa ya watu wengi wenyi bunduki kutoka Bagamoyo kwenda Mpwapwa na Mamboya, atazunguka hatta kurudi Pangani. Alipokwisha kuendelea mbele katika barra, alipeleka habari Pangani kusema hajambo. Akapeleka hivi. Njiwa aliyefugika sana na kuzoezwa kurudi kwake marra moja alitwaliwa, naye akafungiwa khati ndogo chini ya bawa lake, akaachwa pale barra, marra akaruka juu, akaenda Bagamoyo moja kwa moja akaleta khati salama salimini. Njiwa hutumika sana hivyo Ulaya. Lakini tumesikia yule Bughiri amezunguka kuja nyuma yake Capt. Wissmann amepinga njia ya kurudi. Itakuwaje baadaye, hatujui.

Tena manowari za Wazungu zinakwenda zao halafu, zisivizie sana baharini, illa labuda bunduki na baruti tu zisichukulike vyomboni wala watumwa.

KUFA KWAKE REV. C. J. SPARKS.

Huzuni kubwa sana tena, kwani ndugu yetu marehemu Clement John Sparks, Kasisi ya Mkuzi ameitwa na Muungu kuingia katika Raha yake. Alianza kuugua Umba akaletwa Tanga, akapakiwa katika manowari ya Wadoicha akaja Unguja, lakini baada ya siku tano akafia Mkunazini Sept. 22, Kweli inchi ya Boonde ina Kasisi mmoja tu bass sasa; na Makasisi watatu, watu weupe, wamewafia Wabondei katika miezi mitatu. Imekuwa kama sauti ya Muungu kwa Wamasihiya wa Bonde ikiwaita watafute kuwatwalia

MSIMULIZI. 98

Wazungu kazi hii ya kuchunga roho za ndugu zao katika Ungoje wa Kanisa, kwani wao wataiweza vema tabia ya inchi ile, Wazungu hawaiwezi vema. Wamepewa namna nzuri, bassi wazifuate.

HABARI ZA NYASSA.

Barua ya Mletaji hatukupokea mwezi huu, lakini twasikia kwa furaha kama Bwana Askofu akafika salama, na anataka kurudi kwa njia ya Zambesi. Na tena watu 40 wamebatizwa Aug. 3, katika Likoma, 25 watu wazima, 15 watoto. Furaha sana hii. Na watu wote hawajambo. Na chuoni ya Likoma inaendelea sana.

MASASI.

Salamu sana kwa Mtengenezaji. Baada ya salamu nitakuarifu habari zilizotupata kwa wapagazi wetu waliokwenda huko Lindi kwanza; penyi meli ile ulipokuja Msimulizi. Ndugu zetu Edwin Ramathani na Stefano Kajembe wakaenda Lindi wakachukua barua za juzi, wakaenda kwanza pamoja na wapagazi watano illa wangine wakaogopa sana. Bassi hawo watano wakaenda pamoja, na Edwin na Stefano wakaenda nussu siku wakarudi kwa hofu ya maneno ya watu waliowadanganya, waliposikia kama kule pwani watu wa Mzungu wanaviziwa sana kwa ajili ya B. Nakamo.

Bassi hawa wawili tu wakaenda pwani, watano wale wakarejea pale pale Mambaka, Edwin na Stefano wakafika Chitangali wakalala, watu wa pale wakajaribu kuwatia woga lakini wasikubali kurejea nyuma. Tusipokuwa na barua mkononi, wakanena, tungerudi, lakini tumechukua barua tukirudi tutakuwa kama tumedanganya kwani tumewapa tumaini hatta huku sasa tukija huku tumefunga moyo wetu kama tukifa bassi; Bassi wakaenda wakaenda wakafika kwake Edwin Ramathani ndio Newelewele

MSIMULIZI 99

wakakaa siku, akachukua watu wake watano. Wakatoka wakafika Mlawela, akaacha pale kusudi ikitokea hatari warudi wakapashe habari mjini, wenyewe wakafika Lindi. Wakatwaa barua wakampa Banyani ndiye Damdali wakamwambia barua hii kampe Rashidi wa Chapapa; Banyani akanena hasha, heri tukamwite aje huku tumpe barua hii, kwani hapa mjini uthia mwingi sana kwani sisi hatuna hatta ruksa ya kuenda zetu wanatufanya sisi ndio mtego wao: kwani wakanena, tukiondoka, Wazungu watapiga Lindi marra moja; kwani sisi tu watumwa wa Wazungu, wote sababu tuko chini ya rayia za Kiingreza. Bassi akatoka akamwita Rashidi akaja peke yake, wakamwamkia wakatoa barua mbili wakampa, moja Kizungu moja Kiarabu ya kiswahili, Edwin akasoma, akanena Rashidi, Zote hizi zangu? Wakanena ndio! Akanena, mbili kwaje? Akajibiwa lakini maneno ni mamoja kama ya humo. Bassi mwenyewe akanena, Bassi heri tuchukue moja hii mlioandika Kizungu tuende nayo mpaka kwa Sheikh Kazomari mkamsomee mbele yake, kwani akisikia kama mimi nimepata barua mbili ataona uwivu, tena mimi ni mkubwa peke yangu hapa Lindi. Akatoka. Rashidi na Edwin na Stefano na Banyani wakaenda wakafika watu wengi wakakusanyika na Waarabu pia, Edwin akatoa barua akamsomea ikaisha. Wakaondoka wakaenda faragha wakasemana wakaisha wakarudi, wakanena sisi haifai tumkasiri huyo, kwani ametuheshimu hivi hatta akatuletea barua hizi;
Bassi wakawapa mizigo wakanena, Angalieni mizigo mmepewa illa msitoke kwa wazi vijana wasiwaone, itakuwa ghasia burre. Wakawapa ruhusa wakatoka. Tulipowaona tena tukafurahi sana kwa ajili yao.

Safari ya Bwana Askofu bassi tukasikia kwanza katika barua yake, kama atashuka Lindi, tukapeleka safari kubwa kupita kiasi chake cha killa siku, wakaenda wakafika Lindi,

MSIMULIZI 100

illi meli ikija wafuatane nayo. Lakini Rashidi kama tusikiavyo na wenziwe wakamwotea akija wamtie mnazaani wamhasidi. Kwani wakanena, Yeye anakuja makusudi apate kuwa jemadari wao wapapige Lindi. Hatta safari yenyewe wakawaambia msikae hapa mjini kwani hii si safari ni vita tu, toka kukaa Wazungu Masasi hatujaona safari kuma hii. Bassi Stefano akaenda kwa Shilimu kumpasha habari kuma kule Lindi wanatufukuza tusimngoje Bwana Askofu, bassi akatuma mwanawe kuenda kuwatuliza, lakini hawakukubali, naye Stefano hakukubali kuondoka akatoka kidogo tu kama pwani ndogo akajenga na safari yako, mwisho wakaona meli wakinena Bwana Askofu hakuingia ameingia katika Manowali wakapata mizigo wakarudi. Bwana Askofu akaenda akashukia Mineng'ene (Tunghi) akaja Newala, tuliposikia tukafurahi sana kama amefika salama. Akakaa kule kama juma moja akaja Chitaugali, mwisho akaja kwetu Masasi tukaona furaha nyingi mno kuonana naye tena, kwani ndugu zetu waliowekwa kwa Ubatizo wakamtazamia mno na sisi pia, akafika June 11. Bassi Alhamisi ukawa Ubatizo, hatta Juma ya pili ya Utatu wakatiwa mikono watu 28, wan je 20, wa nyumbani 8, tukafanya siku ile siku kubwa akachinjwa mbuzi wakakaribishwa Wamasihiya wale pamoja tukafurahi mno kwa ajili yao wenzetu walioingizwa katika Ujamaa Wa Kimasihiya. Naona mngependa kusikia katika hawa watoto wa nyumbani majina kwani wawili walikuja hukohuko, ndio: Yustino Mkandu, mthamini wako mimi, tena Isaya Kusungulu Nanaguje, mthamini wake Peter Selenge, tena Krusostomo Kaungani nduguye Isaya, mthamini wake Yohana Chimbonaga. Bassi hatta Juma a tatu June 17, akatoka akashika safari ya kwenda zake Nyassa akanena hatapita kwa Makanjila

MSIMULIZI. 101

illa atapita kwa Mponda mpaka Nyassa; akanena, Nikijaliwa kunako October natumaini kuonana tena. Kwaherini sana waanangu.

Safari ya Mineng'ene. Bwana Wathen akataka kwenda zake Ulaya lakini hakuweza akanena kwani alipofika kule MinengÂ ene hakuona watu kwani mji mzima kama hapana watu wamekimbia vita. Bassi yeye akarejea, naswi tukapeleka watu kwenda kumlaki Bwana Smith kwani tumesikia kama anakuja lakini walipowasili Newala Bwana Wathen akawaeleza kama kule pwani hakuna watu, mimi pia nimerudi siwezi kwenda zangu. Bassi waina nanyi heri mrejee mkamwambie Bwana kama watu hapana. Bassi wao wakarudi, tunaona sasa tunatumaini labuda Bwana Smith atashuka Lindi naye Bwana Taylor atajaribu kuongeza watu wapate kumlaki akija, na kama watu wa Lindi wakimpa ruksa ya kushuka pale Lindi pasipo uthia tunatumaini labuda hapana, uthia kama watu wa Mission hawawezi kufanya vita. Wasalama.

Naona mngependa kusikia kama ndugu yetu Harry Muubi na mkewe waliokwenda kwa Machemba alimkataa kukaa kwake. Bassi sasa wanakaa huku Masasi kwani Bwana Askofu aliona heri aje akae huku akajengewe nyumba Chilonji kwa Mkuti. Lakini sasa wanakaa mlima huuhuu wa Mtandi tunaokaa sisi, lakini sisi tunakaa chini ya mlima yeye anakaa mlimani. Lakini siku 22 July saa kama saa sita ao zayidi, nyumba yake ilianguka lakini sasa anajenga kibanda cha kujishikishia kwa kitambo kidogo. Akija Bwana Smith atajengewa nyumba kwa Mkuti. P.K.

HABARI ZA NEWALA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu. Ulipopata barua ya mwisho yenyi habari za Newala ulisoma kama

MSIMULIZI. 102

ndugu yetu mwalimu Joseph Mtapokoma alikuwa hawezi sana. Bassi siku chache baadaye Muungu akamwita aingie katika raha yake Aug. 6, Nathani wote waliomjua wamemhuzunikia sana kufa kwake, na haswa walio ndugu zake za Chama cha Paolo Mtakatifu, kwani naye alikuwamo Chamani akitazamia sana halafu kuwatumikia watu weusi katika kazi takatifu ya Ungoje wa Kanisa. Lakini ameitwa na Muungu apate thawabu yake upesi.

Siku kuu ya Yakobo Mtume, tulikwenda mimi na Bernado Mpunga, Cypriani H. Chitenje, na Arthur Kasembe na wangine, kuwinda kanga, nasi tuliwaua kanga wanne.

Na siku kuu ya Bartolomayo, tulikwenda kuwinda pamoja na Mr. J. Hainsworth na Mr. H. Watson na wangine. Bassi siku ya kwanza tulitoka tukafika Mchauru, Mchauru ni mto unaoingia Rovuma, tukapika nayo ilikuwa aththuuri. Tukatoka tukaja Mkoo, tulipofika, Bernado na Luka, na Archur walikwenda kutafuta maji. Bassi wakamwona mbunju, mbunju ndiye ng'ombe mwitu, tena mkubwa hatta farasi ni mdogo. Bass kumwona yule mbunju, Bernado alikuwa tayari kumpiga, alikuwa akibadili marisawa kutia risasi na Arthur alikuwa akimfukuza akampigia kelele akakimbia na Bernado hakumpiga. Tukalala hatta assubui tulitoka Mkoo tukaja Kingurunguru tukapika na tukatoka pale tukaja Mwiti; Mwiti ni mto nao pia waingia katika Rovuma, katika Mwiti uko mti, ukitiwa motoni nyote mtakuwa wagonjwa. Bassi pale tukaenda kuwinda, na wangine wakaenda kuvua makambale, na makambale ya Mwiti mizuri sana, tukalala pale. Assubui yake tukaenda Mieesi, na Mieesi ni mto nao waingia pia katika Rovuma, mua makambale pia, na tulipokwenda huko wapagazi wakasema, tukitoka saa ya kwanza assubui tutafika saa saba lakini tukatoka assubui saa ya kwanza tukafika Mieesi saa nne unusu. Tukatoka Mieesi tukafika Mbangala, na Mbangala

ni mto nao waingia katika Rovuma. Lakini tukaenda kulala Rovuma upande wa kuume wa Mbangala na chini yake Rovuma. Na Mr. Hainsworth akamwona ndogolo mkubwa sana, akampelekea marisasi akampiga, hatta assubui akamwendea akampiga asimpate hatta kidogo na hii ilikuwa Aug. 28, Siku ya Juma a mosi walikwenda Adamu Nandole na Mattayo Tambala, Petro Mbika, walikwenda kuwinda, Adamu Nandole akampiga mbunju mdogo, na Juma a pili hatukupiga bunduki tulikuwa tukichezea maji ya Rovuma tu, tukauvuka, na upande wa pili ukatushinda kuvuka, illa mimi Enoch Mtaiwa nikaogelea hatta kati ya mto kiisha nikarudi.

Bassi tukafika hapa petu Newala Alhamisi usiku, ndizo habari za siku kuu ya Bartolomayo.

Na jamaa zetu wanasafiri leo Sep. 8, pamoja na Mr. Taylor, wanarudi Kiungani, ndio Arthur Kasembe, Barnaba Mtaula, Sipriani Chitenji, na Yustino Mkandu. E.M.

WAIGAJI WA KIUNGANI.

June 25 ulikuwa mchezo, na mchezo wenyewe ulikuwa mchezo wa "Evano." Na mchezo huu ni juu ya hadithi moja ya wakati wa Warumi walipokuwa wakifanya vita na Wakaledonio (Scotland) na Waingereza. Na mchezo huu umegawanyika sehemu nane, sehemu 'nne za kwanza tukacheza uani, ni za mwisho chuoni. Tukaanza kucheza hivi;-_-Sehemu 1. - Evano, alikuwa Hugh Mtoka. Bassi akaingia Evano mwenyi mfuagwa nyuma yake akimhimiza. Na mfungwa alikuwa Arch: J. Bateman. Evano akamkata kamba mfungwa, na mfungwa akamwuliza sababu ya kumfungua asimwambie. Naye Evano akamchukua akamwonya njia ya siri aende zake. Na mfungwa akataka kumpa pete Evano ipate kumsayidia siku ya hatari, akakataa. Illa akamwacha aende kwa jamaa zake.

MSIMULIZI. 104

Sehemu II. - Madruidi. Na Madruidi ndio wakuu wa dini wa Wakeledonio zamani zile. Na hawa mkubwa wao Martin hawa, nao wote wamevaa ndevu nyeupe. Wakaja wote kwa Furahani, na walio chini yake wanne. Bassi wakaingia shangwi nyingi, wakiishangalia sanamu yao, kwani walifanya sanamu kubwa ya pipa. Nao walipofika wakataka yule mfungwa achomwe. Nao walipoona mfungwa hayuko wakakasirika sana, wakaenda kumwita mfalme, wakamwuliza juu yake asijue habari za mfungwa. Lakini Evano akaungama kama ndiye aliyemtorosha. Bassi wakamtwaa wakamfunga wakamtia ndani ya sanamu, (kwani sanamu ile ilikuwa ya enzerani tupu). Walipokaribia kumchoma, Druidi mkuu akaona vita ya Warumi inakuja, akapiga kelele, Warumi!! Wakakimbia watu wote wakaenda zao. Mfalme alikuwa P. Limo.

Sehemu III. - Marra mfalme alipoona vita kali akamtuma mtoto wake Evano kwenda kwa Lujidi ndugu yake mfalme kutaka msaada. Na alipokuwa akienda alipita njia ya hatari sana. Nayo ilikuwa juu ya dari la nyumba ya kupiga chapa, na pale palijengwa paango la Madruidi. Bassi Evano alipopita pale, Madruidi wakamkamata wakataka kumchoma lakini wakaja askari Warumi wakaona Madruidi ndani ya paango pamoja na kijana. Wakawatwaa Madruidi wakawaua, na yule kijana wakamwuza.

Sehemu IV. - Soko la watumwa (sasa hadithi yetu tumetoka Kaledonia, tupo Uingereza katika Dorchester). Na mwuzaji watumwa alikuwa Martin Furahani. Na katika kuuza watumwa mmoja wapo alikuwa "Evano," naye pia alikuwa mtumwa. Na huyu Evano akanunuliwa na tajiri mmoja wa mji ule jina lake Terentio. Na huyu tajiri alikuwa mimi Samwil Chiponde nikamnunua $300. Nami nikamwuzia mtu mgine kwa $95. Na huyu mtu niliyemwuzia ni Manfred Manyula, jina lake alikuwa Lutatio.

MSIMULIZI. 105

Sehemu V. - (Chuoni). Na katika sehemu hii ni katika nyumba ya yule Lutatio anafanya mashauri na Pompiano. Pompiano alikuwa C. Lizani. Bassi hawa walikuwa wakifanya mashauri ya kumwua Konstantino Kaisari (yule mfungwa alikawa huyu). Bassi hawa wakafanya mashauri ya kumwua Kaisari, wakapatana Evano ndiye atakayemwua Kaisari wakimpa kisu kikali. Pompiano akaenda zake.

Sehemu VI. - Evano anafichwa chumbani mwa Konstantino pate usiku amue, na aliyemficha ni Stefano, alikuwa Reginald Songolo. Lakini usiku ule zilionekana barua mbili zikamwonya Kaisari kama pana hatari. Na barua moja ilikuwa ya Kaisari mwenyewe. Na moja ya Mlinzi wa mfalme jina lake Lukilio. Lakini barua zote zilikuwa za kumwonya Kaisari. Lakini Evano usiku ule hakutenda jambo lolote, kwani usiku ule ule nyumbani mle alisikia sauti ya mamaye. Na mamaye alikuwa Miss Mills. Bassi Evano akatoka akaungama kama anataka kumwua rafiki yake aliyemfungua zamani. Bassi akakimbia akaenda zake.

Sehemu VII. - Katika sehemu hii yumo askofu katika chumba cha huko Rumi anasoma. Na askofu alikuwa P. Limo, na zamani za mafukuzo hizi. Na Askofu alipokuwa akisoma akaja kasisi jina lake Agathos, na huyu kasisi alikuwa Clement, naye anatoka Uingereza. Askofu akamwuliza habari zote za Ulaya akamwambia njema, naye akasema amemkuta kijana mmoja Mkaledonio akamwambia mlete hapa, kasisi akamleta Evano, askofu akamuliza habari zote alizo nazo naye akamweleza zote. Kabla hawajaisha kunena askari Warumi wakavunja ndani wasiwakute watu, kwani wameisha kimbia kwa njia za chini, wameenda zao.

Sehemu VIII. - Mama yake Konstantino, alikuwa Miss Bennett, alikaa kitako na mama yake Evano. Bassi

MSIMULIZI. 106
walikuwa hawa wawili wanaongea. Akaja askari kuwaambia Konstantino anakuja. Naye Konstantino akaja akitoka vitani. Akamsumulia mamaye habari zote za vita yake na tena kama pana kijana jina lake Evano alipigana sana kwa ushujaa. Hatta halafu Kaisari akatuma askari kwenda kumwita Evano, akaja mwenyi mavazi ya vita. Akakutana na mamaye, wakakumbatiana. S.C. Ndio Mwisho.

HABARI ZA MKUZI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu. Nakuarifu kama Mkuzi siku hizi panajengwa kanisa jipya kuta zake hazijaenda juu sana kwani mafundi haba tu. Na Mzungu ni mmoja mwalimu na msimamizi papo, mwalimu ni mmoja tu, James sasa hafundishi. Na Kasisi wa hapa akawa hawezi sana akapelekwa kwa njia ya Tanga kwenda Unguja. Na Sept. 15, ndio siku tuliyofanya siku kuu yetu ya Bartolomayo, twalikawia hivi kwa sababu ya kutafuta ng'ombe wa siku kuu na alipopatikana akachinjwa siku hii na Wamasihiya wote wakagawiwa nyama mbichi haikupikwa karamu, na Mr. Woodward alifanya Usharika Mtakatifu siku hiyo kwani alimpeleka Mr. Sparks mpaka Umba tena akarudi kwa Mkuzi. Na siku ya pili yake watoto wa Mission wakaenda kwao kutembea kwa juma unussu tangu Juma a nne, hatta Juma a mosi ya pili kurudi. Kwani ndio desturi ya Mission za Bonde killa siku kuu kubwa watoto waende kwao kupumzika kidogo kwani watoto wengi wa mbali mbali huja kusoma. Nilipotoka Mkuzi kurudi Kiungani Sept. 19, nalipita kwa njia ya Pangani, majumba mengi yameungua moto. Na Madachi wanajenga ukuta kuzunguka, nyumba zao, na forotha ipo penyi nyumba ya Liwali wa kwanza, lakini nyumba ya Mission ipo lakini vitu vyote vyalichukuliwa. Lakini mngoja nyumba sasa amerudi

MSIMULIZI. 107

anangojea. vilevile kama kwanza. Tukaingia chomboni Ijumaa assubui hatta Juma a mosi athuuri tukaingia Mwanda tukashuka, tukaenda kwa miguu hatta mjini, jioni tukafika tukalala Mkunazini. Juma a pili tukaenda Kiungani. G.J.S.

HABARI ZA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Aug. 26 tulikwenda alasiri kushinda pwani ya Wadi Kapecha, sisi watoto wa Mbweni na watoto waanaake wa shamba wajao kusoma. Na sisi tuliokwisha kutiwa mikono wote, tulipata chayi pamoja nao Mabibi na Bwana, na jioni tukarudi nyumbani. Siku hizi hatuna buddi kupata huzuni marra kwa marra kwao Wapelekwa wetu wa pande zingine, juu yote wa Magila, kwani juzi juzi hapa alishuka Mr. Knowles kutoka Magila kusudi lake kuja kupata hewa Unguja, akakaa hapa Mbweni; alionekana thaifu lakini hakukosa kuja saa za ibada ao mezani; lakini alipokwenda mjini kutaka habari zake kwa mganga siku ya kurudi Magila tena, saa za kurudi tena Mbweni homa ikamzidi; tangu siku hii asiweze kuondoka kitandani, Jumaa usiku September 14 akafariki. Huyu ndiye Mzungu wa kwanza kufia hapa Mbweni na kwa kuzikwa pia, Juma a mosi alasiri akazikwa. R.M.

HABARI ZA KIUNGANI.

Panapo Aug. 14 Philip E. Yahom mwalimu amewasili hapa kutoka Magila.

Aug. 17 ndio mwaka wa Kiislamu, mji mzima ulikuwa wenyi uthia mtupu, lakini uthia huu haukudiriki, kwani General Mathews, mkuu wa askari, aliwatawanya askari zake killa pahali, hatta hapa walikuja askari kukaa kwa zamu mchana na usiku muda wa siku mbili, ndipo uthia ulipotulia. Aug. 24, Siku kuu ya Bartolomayo Juma a mosi ulikuwa mkutano hapa, wageni wengi wakaja wa Mkunazini na Mbweni. Kwanza ulikuwa Usharika Mtakatifu

MSIMULIZI. 108

saa ya kwanza unussu, tena saa nne unussu wageni wote walipokwisha kuwasili hapa, tukaingia kanisani wote kwa Sala kubwa ya Assubui, na Mr. Wallis ndiye aliyekhutubu, kiisha tukatoka. Aththuuri tukapokea chakula chetu, kiisha wangine walicheza tinge, na wangine ni kuzungumza tu na rafiki zao, hatta jioni killa mtu akajirudia katika masikani yake. Aug. 25 ilikuwa Juma a pili, killa mtu alistarehe. Aug. 26 Juma a tatu alasiri palikuwa mashindano tu bass, wangine kwenyi mpirani, killa upande watu edashara wala hapana walioshindwa, na wangine walishindana pwani ndogo ya Kiungani, kupiga mbio, kutupa mbali mpila, kuruka, na kuogelea.

August 28 Siku kuu ya Augustino Askofu mweusi wa Hippo mtu wa Afrika, tulicheza tangu assubui hatta jua chumvini. Sept. 2 Archdeacon Jones-Bateman amerudi (Unguja pamoja na Miss Townshend kutoka Moris. Aug. 5, Tumempata mtoto mmoja jina lake Chapamba ametoka katika H.M.S. Agamemnon, tena tunafurahi kama tumepata viti vizuri vya kanisa letu vitokavyo Poona, vimefanyizwa na Wahindi Wamasihiya. Tena tunafurahiwa sisi watu wa Chama cha Paolo Mtakatifu kama Archibald Semmanyi ameingia chama.

Hapa mwezi huu wa September, kumejengwa sakafu nzuri ya kuchezea mpila wa vibao (Tennis.) Tena chini ya Studies hizi mpya zijengwazo, kumekuwa nyumba ya sermala. August 20 Ijumaa imekuja meli ya kusini pamoja na Mr. Taylor, na Sipriani Chitenje, Arthur Kaisembe, Barnaba Mtaula na Yustino Mkandu. Tena H.M.S. Reindeer imekamata watumwa 124, na penyi August 21 tumechagua watoto watano katika hao 124, majina yao, Yanikore, Sauli, Kamanaa, Kibandera na Kaluma. Mikael Yusufu amekwenda kukaa Mkunazini kuwa mwanafunzi wa mpishi, na Marko Njala pia amekwenda

MSIMULIZI. 109
kuwa mshona viatu vya kizungu kwa Mgoa Souza. Mtg.

HABARI ZA MBWENI SHAMBA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Nathania mtapenda kusikia kama Basil Kamna na mkewe wamepata mtoto mwanaume amezaliwa Sept. 10, amebatizwa Sept. 22, jina lake Samuel Frank. Filipo Mpande na mkewe wamepata mtoto mwanamke amebatizwa August 24 jina lake Alexandra, Henry Abdallah amepata mtoto mwanaume jina lake Yohana. Siku kuu va Mattayo Sept. 21 Mr. Wallis alifanya siku kuu ya waimbaji (Choir), walikwenda kushinda kisiwani Chumbe pamoja na watoto wa chuoni wa shamba. Tuliingia katika dau Bwana wawili na Bibi wawili, na watu weusi 36, ilikuwa karamu kubwa sana kwetu, lakini hatukucheza kwani maji yamejaa sana, ilikuwa kutembea kisiwani. Hatta saa kumi unussu tukaingia dauni, tangu Chumbe tulipata baridi nzuri, kupita Chukwani baridi hapana, marra tukaona mashua ya moshi mbele yetu, Mr. Wallis akawaambia watufungashe, wakatufungasha, nayo ni mashua ya H. M. S. Boadicea ikatupeleka hatta Mbweni, saa thenashara na robo tukafika Mbweni. Watu waliosafiri na Bwana Askofu, katika kurudi kwao wamefika hapa Sept. 20 nayo ilikuwa furaha sana kuimba na vigelegele bunduki zikapigwa. T.M.

HABARI ZA MSARAKA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu. Baada ya salaamu naona mtapenda kusikia khabari za huku za siku hizi, bassi naanza kuwaarifu khabari yenyewe. June 15 palitokea uwongo mkubwa sana, nao ndio huu, Siku moja, mtu mmoja alikuwa amelala usingizi usiku, bassi na katika usingizi wake aliota amejiwa na mtu aliyekufa zamani sana; bassi yule mfu akaulizwa khabari na yule mtu wa uhayi, mfu alimwambia maneno haya, Ebu nitazame sana,

MSIMULIZI. 110

bassi alimtazama saana, mfu alimwuliza tena, umepata kuniona siku hizi zote zilizopita? Alijibiwa sijapata kukuona, bassi akasema. Nimerudi Ahera kusudi kuwaletea ninyi habari zitakazowapatia uzima wa milele.

Akanena huko ninakotoka wazimu wana ghathabu sana juu yenu. Akaulizwa kwa maana gani wana ghathabu? Akanena kwa sababu mmepanda mtama mwaka huu, akamwambia waonaje tukitaka kuwapa rathi huo wazimu tufanyeje? Akanena sharti mtama mwache shambani ukae wala mtu hatta mmoja asijaribu kufukuzia ndege, ndipo mtapata kuwa wahayi, illa mtu akiitharau ni nathari yake, kwani hana buddi kuko huko shambani atapigwa makofi na wazimu. Lakini maneno hayo yanaaminiwa na washenzi walio katika upumbafu waliourithi kwa baba zao. Juma a mosi kama mjuavyo ndio siku yangu ya kutelemkia Umba, bassi nilimwona mtu mmoja katika shamba lake, naye aitwa Chapwata, bassi nilimtega, kwa sababu yeye alikuwa akifukuzia ndege mtama wake. Bassi nilimwambia kwa sababu gani unafukuzia ndege mtama wako? Marra hivyo alinijibu, Ah, hivyo kumbe mwalimu hunitaki? Nami hamwuliza kwani? Akaniambia unaonaje taabu tuliopata zamani mfalme Sayidi alipopigana na Mbaruku, kama tungalikuwa hatuna Wazungu wote sisi Wabondei tungalikuwa watumwa, bassi jambo hilo ndilo linaloniogofya kuacha mtama kuliwa na ndege, nami hamwaambia una akili. Lakini msithanie maneno haya Wabondei wote wameyaamini, illa watu wanaoitwa wabahau (ndio wasio na fikiri) nao wamepata hasara tupu, kwani mashamba yao hayana mtama, wote umeliwa na ndege.

Na khabari nyingine ni hii. July 18 ndiyo siku nilipoanza kuwashawishi watu wa miji yangu mitatu, 1 Msaraka, 2 Mkumbi, 3 Jaila, habari ya misalaba. Nao nilipowaambia waliona furaha sana, nami ninajaribu kuwafundisha

MSIMULIZI. 111

Alhamisi hatta Alhamisi panapo saa 10 unussu. Lakini siku moja Mr. Sparks alimtuma Mbondei mmoja kutelemka hatta Pangani kasidi kuwaletea Wadachi barua wazilete huku Unguja, bassi alifika salama nazo, lakini wakati wa kurejea Bonde alipofika Mgambo, alikamatwa na watwana wakamfunga mikono nyuma, naye alikuwa na rupia zake tatu akawapa kusudi kutetea roho yake, nao walimwacha. Bassi alipofika mjini akawapa watu habari iliyompata. Bassi ikaenezwa ya kuwa yule hangalikamatwa, iliyomwacha hatta akakamatwa ni msalaba, bassi watu wale waliokuwa wakifurahi kwa khabari ya misalaba wakapungukiwa moyo. Marra nilisikia watu wangine wakisema maneno haya;- kumbe sisi tulikuwa tukitumainia kwamba misalaba ndiyo itakayo kutusayidia, kumbe ni hatari kwa Wangwana; bassi fayida yake nini kuwa na misalaba, nami hatta sasa ningali nao kujaribu kuwaambia khabari hii ya misalaba, nami ninatumaini kama Mwenyiezi Muungu atanisayidia kuwavuta katika kuwa Waanafunzi tupate kuwa kundi moja, na Mchunga mmoja.

Na hapa ninawaarifuni khabari ya chuoni yangu July 29 ndipo tumepatana na mtu kutengeneza chuoni yetu. Kwani siku chache iliachwa tupu watoto walikuwa wakisomea nyumbani, lakini sasa nimeona afathali itengenezwe kwa maana nyumba sasa imekuwa haina nafasi kwa sana, kwani pana siku hupata watoto 47, 44, 39, watoto wa nje tu hawa, watoto wanaume wanakuja illa si kwa mno, kwa maana kazi hujitahidi sana kuwinda paa killa siku, kwani kwenda msituni ndio kama kuvua samaki kwao, msitu ndio bahari yao, lakini watoto wa kike ndiyo wajao wengi sana. Nami ninatumaini hatta hawa wanaume watazidi. G.K.

Kesho Okt. 1. Wanakwenda Mr. Wallis na mkewe Mkuzi, na Miss Townshend na Dr. Castle kukaa Magila. Wanaingia merikebu ya Wadachi kushuka Tanga.

MSIMULIZI. December, 1889. VIII.
Imepigwa chapa Kiungani, Zanzibar,
katika "Universities' Mission to Central Africa."

MIMI HAPA MSIMULIZI!

Ee Bwana wee, u hali gani? nimekujia tena kwa maongezi safari hii; na habari zangu mwenyewe nionavyo njema sana, kwani nafikiri kama sasa nimepata umri wa mwaka mmoja tangu kuzaliwa kwangu, na kweli tangu kuwa mchanga tu kazi yangu kusafiri na kusimulia tu. Nimefika marra kwa marra kwa killa mji wa Upelekwa wetu nimezungumza na watu sana, wamefurahi kupata habari za ndugu zao pangine pote, kwani ndizo niwapazo sana, hatta huniona sasa kuwa kama rafiki wa kutazamiwa sana. Hatta nilipo huku Unguja kwani mimi mzalia, ati, wa kisiwa cha Unguja. Waletaji habari hawakosi kuniletea habari za kwao, hawanisahau, illa labda mmoja wawili wamepitiwa mahali.

Sijajua, somo, kukawia kutoka huku mwezi wangu ukiwadia, nafunga safari nakuja zangu usipungukiwe habari, kwani, somo, mimi mpesi bado, sijawa mzee, ati, kwani mwenyi umri wa mwaka mmoja tu. Wala sijapata kuzuiwa sana hatta kwa vita hii ya Wadachi, labda vita hii ya Wareno itanizuia safari hii nisifike Likoma upesi, lakini nitashuka zangu Kilimeni, nitajitahidi kupenya hatta Nyassa.

Na Mtengenezaji wangu ninaye yuleyule, nimemzoea sana, tunapatana kweli; ananitengeneza na kunisahihisha na kunifungashia safari vema siku zote.

Lakini, somo, nina neno moja, uwe rathi, usikasirike. Nataka sana mwaka huu ujao unikaribishe vilevile, nije nikakusimulie vilevile habari za ndugu zako; labda utanijibu, kwani sikukaribishi? Ah, bwana, mambo ya Bin Adamu, mengi; sisemi mimi Bin Adamu halisi, kwani nina

MSIMULIZI. 113

kinwa cha kusema tu na masikio ya kusikia tu, hatta watu huniita kitabu tu, lakini uwe rathi, kuna gharama kidogo katika kufunga safari yangu, hatta sina buddi nikuombe unilipie pesa sita kwa mwaka huu ujao kwa Mletaji habari wa kwenu apate kuzileta Unguja, kwani, somo, bin Adamu asafiripo hana buddi kula. Bassi usikatae, lakini uniambie nije sikuzote kwako, nami nitakuja.

Bassi somo, maneno hayo, ni yangu; nami nashughulika sana, kwani sharti niwafikie watu kama 350 killa safari hatta Ulaya nafika kwa watu wapata 20. Bass uwe rathi, bwana, mimi hapa Msimulizi wako.

VITA YA PWANI.

Hatuna hakika ya mambo mengi miezi miwili hii. Captain Wissmann alikuwa amefunga safari kwenda Mpwapwa. Bassi alipokwenda zake, Bushiri akaja pwani akaleta Maviti wengi, yeye na Bwana Heri wakafanya vita kubwa pwani juu ya Wadachi pande za Saadani akapigwa, Bushiri akakimbia. Tena Captain Wissmnn akarudi njia ile ile aliyokwenda, ameacha Wadachi watatu Mpwapwa na asikari mia, makusudi watulize watu wa pande zile, na kuilinda njia ya kwenda Unyanyembe, Ujiji, na pangine. Halafu atakwenda kupiga Kilwa.

Katika Pangani na Tanga hapana vita. Illa watu wa Pangani waliofukuzwa wamefanya uthia kidogo, kwani waliwakimbilia Waboondei, wakawashawishi watu wa Sega, wawasayidie. Bassi wakaja Wadachi wakavunja mlango wa boma la Sega, wakawastusha watu hatta hawakuweza kuwapigia bunduki moja. Wadachi wakaenda zao, ikawa uthia vilevile Sega.

Siku hizi manowari nyingi zimekwenda zao, na Maadimeli wote wawili, wa Waingereza na wa Wadachi, wamekwenda zao. Hakuna kuvizia sana baharini kama kwanza. Tena

MSIMULIZI. 114

barozi mkubwa Mr. Portal amekwenda Ulaya, kwani Col. Euan Smith, yule yule aliyekuwapo kwanza, sasa anarudi tena. Bassi huyo Mr. Portal tumkumbuke sana na kwa heshima, kwani amepatana sana na Seyidi Khalifa, hatta Seyidi amekubali kutangaza sheria ile, tuliyoinena katika "Msimulizi" wa Oktober. Bassi Mr. Portal amewapatia watu wengi kuwa huru, tangu Nov. 1 na baadaye, hatta wasimjue wenyewe wala kumshukuru kwa kazi yake njema ndio watumwa wale wazikimbiliao inchi za Seyidi Khalifa na miji yake na visiwa vyake.

UGANDA.

Barua ya ndugu yetu Henry Wright Duta imetuwasilia siku hizi, ikatoka Usambilo upande wa kusini wa ziwa Nyanza mwezi July, ikafika hapa November. Na habari zake za ajabu na mashaka pia. Kwani amesema yule Mwanga, mfalme wa Waganda aliyekubali Askofu Hannington auawe, akawaonea watu wake akataka kuwaua Wamasihiya wote, hatta akafukuzwa mwenyewe na Waarabu, yule yule Mwanga alikimbia Usambilo kwa Mwarabu mmoja akafungwa akaokoka tena, akawakimbilia mapadre Wafransa kule kule. Na Wamasihiya wengi wa Uganda, wapata elfu tano sita, nao pia wakakimbilia Usambilo, wakasikia habari kama Mwanga yuko kwenyi Wafransa afundishwa nao, amekuwa Mwanafunzi, labuda atabatizwa baadaye. Wakasema, kama kweli Mwanga ametulia ametubia matendo yake mabaya aliyowatendea ndugu zetu zamani, bassi tumsamehe. Hatta wakamkubali Mwanga kuwa mkubwa wao, wakaingia mitumbwini wakaenda kwa kisiwa kimoja kikubwa, Sese, karibu na Uganda, Mwanga na Waganda walio Wamasihiya, na Waingereza wawili walio wapelekwa, Mr. Gordon na Mr. Walker, na Wafransa wangine, na Mr. Stokes pia alikwenda. Halafu wakashuka pwani Uganda wakapigana na Waarabu na

MSIMULIZI 115

Waganda waliowafuata, wakapigwa, wengi kama mia sita wakafa, wakarudi kisiwani Sese. Hatta mitumbwi yote ya pande zile ikaletwa Sese, Waarabu wasiweze kuvuka wengi kufika Sese, kwani mitumbwi hapana. Bassi ndio hali yao, thaifu na yenyi mashaka, kwani wanaviziwa na adui wala hawana nguvu ya kuwashinda. Bassi wamemletea balyozi hapa Unguja barua wakisema, tuma watu kuja kutusayidia. Lakini hataweza, kwani mbali sana. Tena Henry Duta amekuwako Sese, ataka tuwaombee ndugu zetu Wamasihiya wa Uganda, kwani wamepata mazito mengi, tena wako hatarini, wapate kuokoka. Hatta Mwanga akipata nguvu kuingia katika enzi yake tena, labuda ataweza kuueneza sana ufalme wa Bwana wetu katika Uganda.

Tena siku hizi habari kubwa imekuja, kusema Stanley anakuja Unguja, naye karibu, labuda atadiriki kufika "Msimulizi" asijepigwa chapa bado. Na huyo Stanley ajabu sana, kwa nguvu zake na safari zake, ginsi alivyosafiri sana kupita watu wote katika barra, zamani na siku hizi pia. Kwani yapata miaka miwili unusu akaingia merikebu "Madura" papa hapa Unguja, pamoja na Waunguja wengi, na wangine wengi wapagazi, akazunguka Kepi, akafika Kongo. Tena akaingia mashuani, yeye na watu wake, wote wakaenda mbali sana kwa mto Kongo, na mto mdogo wake Aruwimi. Alipofika pale, akafanya kituo kikubwa na mwenzake mmoja kuwa mkubwa wake, akasafiri tena kwa miguu kwenda kwa Ziwa "Albert Nyanza" kwani ndio kusudi lake, kufika alipo Mzungu mmoja, jina lake Emim Pasha, amekaa siku nyingi peke yake, amezungukwa na adui, asikubali kushindwa nao. Bassi Stanley ataka kumletea msaada. Akamletea, lakini kwa shidda kwani safari ya hatari sana, njaa, mapoli, adui, marathi. Hatta

MSIMULIZI. 116

akafika penyi Emim Pasha, akarudi kwa kituo kile kutwaa mizigo, akakuta kimeharibika na mwenzake ameuawa. Haithuru. Alifunga safari tena kurudi pale pale Emim Pasha, akapotea siku nyingi sana, watu wa Ulaya wote wakasema, Stanley amekwisha kabisa. Kumbe ikaja barua kusema, yu hayi bado, atenda kazi yake, atarudi. Ndivyo alivyo. Anakuja, hatta sasa yupo karibu. Ulaya wote utastushwa sana na kushangilia na kufurahi, watamkaribisha kwa vigelegele ya mizinga na heshima kubwa, kwani amezindua mlango wa kuingia katika Afrika, ameingia mwenyewe, ataingiza na wengi baadaye. Hatta Wamasihiya watafurahi wakiona ule mlango wa Livingstone umezidi kuwa wazi, mlango wa kuingilia Bwana wetu na anjili yake. Haya, twende.

HABARI ZA MLOLELA [AO CHITANGALI.]

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Na sasa mmesikia kama Mwalimu Cecil ametoka hapa akaenda zake Unguja kwa kazi yake ya Ungoje. Na Mr. J. Hainsworth yupo hapa pamoja nami. Naye ameanza kujenga school, kwani mlisikia kama tumehama mahali pale pa kwanza, sasa tunakaa ng'ambo ya pili. Na kanisa limekwisha jengwa nalo limejengwa kwa sadaka za watu wenyewe wa hapa.

Na tena habari za mtu mmoja anayedanganya watu wa hapa, anaitwa Chikale ao Chimpada naye ni Mnyassa, anafanya dawa nyingi za kuwadanganya watu, na mwenyewe husema kama dawa zake hakuonyeshwa na mtu, illa alikufa na baada ya kufa akazikwa na baada ya siku tatu akafufuka, bassi dawa hiyo amefunuliwa na Muungu. Na siku za kwanza watu wengi sana wakamwendea wakimletea kuku kwa hizo dawa zake, na huwaambia kama

MSIMULIZI. 117

"Kesho mtapona," na kesho ile yule mgonjwa kama amezidishwa ugonjwa wake; wala hana dalili ya kupona, bassi watu wakaanza kumwia kwa zile kuku walizompa na akawarudishia wenyewe tena, na tangu siku zile hatta leo watu wamekoma kwenda kwake.

Na Barnaba Nakaam sasa kaisha patana na watu wale waliofanya uthia wa Lindi, naye kaenda Masasi tembea. Siku hizi watu wengi waliokuwa hawaji kusikiliza maneno ya Muungu wanaanza kuja wengi mno. Mahali hapa tulipojenga safari hii pote pamezungukwa na msitu na nyumba zote kati, haswa mji wake mwenyewe B. Nakaam unaoitwa Msokosela, uko kati ya msitu na boma la miti. Watoto wa hapa huja kwa kusoma killa siku pamoja na watoto wa kike, nao watoto wa kike hawana mwalimu sasa, kwani Lucy kenda Unguja. Y.B.A.

Na Bwana Cecil Majaliwa, aliopo bapa Unguja akija kufanywa Kasisi, anatuletea habari hizi za kazi yake na safari yake.

Mbele ya kutoka kwanza Chitangali Siku kuu ya Mikael wamefanywa Waanafunzi 27, watu waliokuja siku zote kujifundisha, mmoja wao ndiye mzee Maruchila ndugu wa Barnaba Nakaam mkuu wa Chitangali. Twaomba Muungu azidi kuondokesha Wamasihiya, Muungu ameibariki sana kazi yetu, sasa Chitangali jumla Wamasihiya 32 Waanafunzi 44, wasikia hawana hakika killa siku waingia.

Oct. 9, Nikatoka Chitangali mapema kusudi nipate kwenda sana, kama saa ya pili unussu tukafika Chitangali ya Mangochi ziwani, tukafika saa tano, tukatoka mimi na Bwana Barnaba Nakaam, Daud na Isaak, na Wamasihiya wa Chitangali walionisindikiza hatta karibu ya kufika Mpumbe wakarudi, sisi tukalala siku ile Naikula.

Oct. 10, Alhamisi assubui mapema baada ya sala tukatoka,

MSIMULIZI. 118

kama saa tatu tukafika kwa Machemba nikajaribu sana kumtafuta lakini sikumwona, tukatoka, karibu na mwisho wa mji wake tukawakuta Paolo Mputeni na watu wake. Tukamwona Daud na nduguye na wenziwe wanatoka Unguja wakatupa habari kama Mr. Sparks na Mr. Knowles wamefariki, hatukwenda sana siku hiyo, tukalala kwa mtu jina lake Ndomondo katika watu wa Machemba.

Oct. 11, Tukatoka assubui tukafika Kunleje, tukalalia kwa Kaliwanje Mwera.

Oct. 12, Tukatoka Kaliwanje hatta Mloweka kwa Mahilinga mkuu wa Kimwera, akatuheshimia sana, akatupa nyumba.

Oct. 13, Tukashinda Mloweka kwani Juma a pili, hatta alasiri tukatoka mpaka kwa Sellim, na pia akatufanya wageni wake, jioni akatupakia mashuani kwenda Lindi, tukafika Lindi kama saa sita usiku.

Oct. 14, Tukaweka killa kitu tayari kuingia katika meli, tukatengeneza madafu 44 kwa Bwana Askofu.

Qct. 15, Nikaenda kumtazama Kathi Omari, na Rashid Oui Papa, Kathi Omari mtu wa akili na mzuri sana. Oct. 16, Ndiyo siku iliokuwa siku ya meli lakini meli haikuja. Watu wengi Lindi wakauliza mambo ya Bwana wetu Isa Masiya, wangine kwa kweli na wangine kwa thiaka, na habari za ndoa na talaka.

Oct. 17, 18, 19, Tukakata tamaa ya meli, Oct. 20, Juma a pili, tukawa Lindi vilevile mahali pasipo kanisa, lakini tukasali chumbani mwetu jumla Wamasihiya watatu.

Oct. 21-24, Twatazamia chombo, kwani tumesikia kinakuja kutoka Unguja, Oct. 25, chombo kikaja. Oct. 26, Kikaenda Mikindani kupeleka bithaa iliotoka Unguja. Oct. 27, Juma a pili tena hali ya huzuni, alasiri chombo kikaja kutoka Mikindani. Oct. 28, Wakapakia, mwajua kupakia kwa chombo

MSIMULIZI. 119
kanda moja moja.

Oct. 29, Jioni ya Juma a nne tukaingia chomboni.

Oct. 30, Juma a tano wakatweka, tukasumbuka sana na tharuba kutwa na kucha hatta Alhamisi Oct. 31, tukaingia bandari ya Sangarungu jioni. Nov. 1, Ijuma wakatweka mapema, tukapata safari nzuri sana, hatta jioni tukafika Ukuza tukalala, chombo nilichotaka kuingia kutoka Lindi, kilichochukua barua, nimesikia kama kimevunjika.

Nov. 2, Wakatweka kutoka Ukuza lakini hatukwenda sana kwani shwari, jioni wakatia nanga kisiwa Mofya.

Nov. 3, Watu wa chomboni wakashuka kuteka maji, mlikuwa na Mabanyani wakapata kwenda kupika. Vyombo kama kumi vilikuja kuteka maji, Juma a pili wote tukashinda kisiwa Mofya.

Nov. 4, Wakatweka, kutwa, tukalala Kwale, Nov. 5, wakatweka, kutwa, mbisho hatta jioni wakatia nanga Pemba Mnazi, Nov. 6, wakatweka tukapata upepo mzuri lakini hatukuweza kuingia mjini tukalala nyuma ya Chukwani.

Nov. 7, Tukaingia Unguja rafiki zetu wakatufurahia mno. Tukathani Bwana Askofu amekwisha fika, lakini hatta wao hawana habari zake.

HABARI ZA NEWALA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada va salamu siku hizi hapa katika Mission ameuawa chui alikufa Oct. 13, kwanza akategwa na bunduki ya kubandua ya Mission.

Oct. 15 akaja akakwarua-kwarua bunduki, lakini haifyatuki ilikuwa ngumu, bassi asubuhi yake tulipoona hivi tukabadili tukaweka bunduki ya Nokoa T. Chiputula, bassi tukatega akaja akataka kutwaa kuku bunduki

MSIMULIZI. 120

ikapigwa kama saa tatu unussu, tukatoka watoto wote kwenda kutazama lakini tukaona kuku tu amepigwa kucha, na chui akasimama ukutani, tena akaruka ukuta karibu hakuenda sana akaanguka akafa wala hakutoa ngurumo, kwani risasi ilimpiga haoni; na marisao pia. Na assubui tukaenda watoto wachache kutazama kama saa kumi na mbili tukataka kupanda ukuta, mtoto mmoja akasema nimemwona chui amekufa, bassi watoto wote wakapiga makelele, chui amekufa! amekufa!! Watu wengi wakaja kutazama. Bassi Mfalme wetu mzee Matola akatoa zawadi, kwa kumlipia ndio dasturi yao siku zote tangu zamani zao mtu akiua kitu cha hatari kama simba humpa zawadi, na ngozi yake ni nzuri sana ina madoadoa mengi sana na mazuri. Na katika siku kuu ya Luka, Mwalimu Enoch alikwenda Chitangali, pamoja na watoto wawili wa Chitangali, Yohana G. Mpalila na Danieli Usufu, wakarudi Juma a tatu, walikwenda Jumaa. C.M.

HABARI ZA MBWENI SHAMBA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Mtu mmoja jina lake John Gilbert Mabruki amefiwa na mwanawe. Tena Oct. 19 Florence mkewe Titus Mataula amezaa mtoto mwanamke, Oct. 20, mtu mmoja jina lake Bahati mke wa Kainna amezaa mtoto mwanamume, Oct. 29, Bridget mkewe Timdthy Matitu amezaa mtoto mwanamke. Tena mtapenda kusikia kama ndugu yetu mmoja aliofariki, alikuwa hawezi kwa siku nyingi hatta akahamishwa Mkunazini, huko tena Muungu amemtwaa Nov. 13 na jina lake Daniel Majaliwa, naye amezikwa ziwani. T.M.

HABARI ZA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu. Na baada ya salamu nakuarifu habari hizi siku ya 4 Oct. ilikuwa Chama ya Waalimu wa Mbweni, na mtu mmoja akaingia

MSIMULIZI. 121
ndiye Blandina Mwamkwama.

Siku kuu ya Siman na Yuda, 28 Oct., tuliyakinia kwenda kushinda Chukwani lakini hatukwenda, tukashinda nyumba ya kazi, sababu ilikuwa mvua nyingi. Tukafanya furaha yetu hapa.

Tena siku ya 12 Nov. watu chache kama kumi na tatu, watoto wa Chuoni walikwenda Mkunazini kwa mchezo kidogo, siku nzima wakashinda wakatembea dukani, hatta alasili saa kumi wakarudi zao Mbweni.

Siku ya 29 Nov. tunamtazamia bibi mgeni atakayekuja kufanya kazi hapa Mbweni jina lake Miss Margaret Berkeley. R.M.

HABARI ZA MKUNAZINI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Na baada ya salamu nakuarifu habari kidogo, Oct. 18 akabatizwa mtoto mmoja wa Miss Mills jina lake Stefano Alfaeato. Nov. 3 akabatizwa mtoto mwanamke wa Litala na Agnes Sudi jina lake Elizabeth. Oct. 20 watu watatu wametiwa katika Uwanafunzi, majina yao Habeba, Maua, na mwingine. Oct. 22 Giles Dodoma alimwoa Alexandra mtoto wa Mbweni, na Peter Salimu alimwoa Emma Dunford. Oct. 23 walikuja kukaa hapa Alban Sekehola na Philemon Juma. Oct. 29 Miss Shaw amefika Unguja, Nov. 4 Kathbert mtoto wa Miss Mills alifariki akazikwa ziwani. Norman Namkachapo akarudi tena Unguja baada ya taabu nyingi, Marko Njala akaja mjini kushona viatu mahali pa Luke Mabruki, kwani siku hizi Luke anafanya kazi katika H.M.S. "Cossack." Na siku hizi Mkunazini kuna chama cha watu waliopatana kwa ahadi kama hawatakunywa kileo cho chote kwa muda. Siku kilipoanzishwa chama Archdeacon Jones-Bateman akaja kuwahubiria na Mr Clarke pia, kisha wakatazamishwa sanamu ya ukutani na Mr Madan hapa petu. Watu kumi

MSIMULIZI. 122

na mbili wametoa ahadi kwa muda wa miezi sita. Na Nov. 16 watu wa chama pamoja na rafiki zao walijikusanya kutazama mchezo wa "Bluebeard", mwalimu Cecil akasoma hadithi yake, watoto wa Mbweni pamoja na Miss Bennett wakafanya sanamu nzuri sana, watoto wa Miss Mills wakaimba, tulipotoka wote tukaimba "God save the Queen". Na Bwana Mr. Clarke akaenda Pemba katika H.M.S. "Mariner" akarudi Juma a mosi Nov. 23, akaenda zake siku hiyo hiyo, akaenda Ulaya kwa mwaka mmoja. Salaamu. S.U.

HABARI ZA MKUZI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu kama Wadachi walipokwisha piga Pangani ukaja uthia kwa Wabondei, majumbe ya Pangani wakaja na mali wapate kuwapa watu wawafiche, watu wangine wakapokea mali na wangine wakakataa. Tena ilipokwisha, watu wa mji mmoja katika Mkuzi ndio Sega, pakaondokea mkubwa mmoja jina lake Semwaiko akataka kuleta vita kwa Mdachi, naye pia alikuwamo katika wale watu waliochukua mali kwa majumbe. Hatta watu wa Mkuzi wakaogopa kwa sababu marra kwa marra watu wanakuja kusema uwongo kama Mdachi yuko njiani analeta vita, bassi wanaake usiku wanahama, wangine hulala mashambani na wangine wanasema, sisi Mdachi akija kweli tutamchukua hatta kwao hao waliokula mali za majumbe, wangine hujisifu wakisema, na aje sisi tunamngoja tupigane, nyie mnaogopa, nasi hatuogopi. Tena siku moja tukataka kwenda kushinda Kakindu siku ya sikukuu ya Watakatifu wote pamoja na Mr. Wallis na mkewe, na mwalimu John Swedi pamoja na watoto wote wa Mkuzi, na mwalimu wa Umba ndiye Granville Kachipumo na watoto wake wote na mkewe wakaja Mkuzi. Tukakaa tukaona watu wengi wa Mkolola wapita wamejifunga selaha killa mtu kwa selaha

MSIMULIZI. 123

yake, wakaulizwa, mnakwenda wapi? wakasema, tunakwenda kumwamkia Seyidi Pangani, kumbe wanakwenda kuchukua wenzao wapeleke vita kwa Madachi. Bwana Wallis akasema, ni heri tusiende kwani labuda watu hawa wanakwenda kupigana na Madachi, watakapofukuzwa na wakija wakituona njiani labuda watakamata mtoto watamua kwa uchungu, bassi itakuwa uthia mwingi. Tukakaa tukacheza palepale Mkuzi hatta jioni ikapigwa kengele tukaenda kanisani, tukatoka tukaenda mezani tukala halafu tukatoka tukacheza halafu tukaenda kulala. Assubui tukaagana na watoto wa Umba na mwalimu wao, tukakaa, marra tukaona watu wa Sega wakakusanyika pamoja na watu wangine, hatta na mtoto wa Sehiza jumbe wa Mkuzi akaenda, jina lake Kichenje, na katika hao wote mkubwa wao ni Semwaiko, mzee Sehiza akajaribu kuwarudisha asiweze, wakakataa, wakaenda hatta Mgambo wakasema, na aje tunamngoja wakakaa hatta Juma a pili. Captain Wissmann alisafiri, aliporudi akaambiwa vita iko Mgambo nao wanaoleta ni Wabondei, akaandika barua akasema, waambieni wailete leo; wasipoleta, kesho waningoje, walipoiona barua wakaitwaa wakaipasulia mbali wakakaa hatta assubui Juma atatu wakajifunga selaha zao, hatta walipoisha wakaingia katika ngome wakakaa, marra wakaona majumbe waliowapeleka kwenda kungoja Boza wanafukuzwa marra wakaona asikari za Dachi wanakuja na Captain Wissman amepanda juu ya frasi na upanga wake, Kichenje akamwambia Semwaiko, vita ileee inakuja, akauliza iko, wapi? akamwambia ile, akamwambia, kweli; Kichenje akasema, nipishe mimi nipige kwanza, Semwaiko akamwambia, acha nipige mimi kwanza, akamwambia, vema. Aliposimama apige bunduki, kumbe wale adui walikuwa tayari kupiga zao, marra aliposimama Semwaiko apige, adui wamekwisha piga zao, wakampiga risasi za

MSIMULIZI. 124
kifua zikatokea mgongoni akaanguka chini amekwisha kufa. Kichenje alipomshika ameisha, wenzie wakamwambia, mwache ameisha kufa, akamwacha, wakapigana sana. Na upande wa Mdachi palikuwa na mtu mbaya sana wenzake wanapopigana yeye huchukua msumeno anakwenda kukata mlango wa mji wakimkosa risasi hakubali kushindwa anarudi. Mtu mmoja jina lake Bota akapigwa risasi za mgongoni zisiingie illa zikaenda kukata sikio, akakimbia, na Kichenje akakoswa risasi, lakini baruti tu ilimwumiza mgongoni lakini asikubali akapigana sana kusudi wampate mwenzao Semwaiko aliyeuawa, hatta wakampata mfu wakamzika. Wakapigana nguvu zao zikawa haba, wakanyang'anywa ngome, Mdachi akaitwaa ngome, na watu wakufukuzwa wakuingia mwituni. Wadachi wakaingia, wakachoma mji, halafu Captain Wissmann akawaita asikari akisema, njooni ninavunja kasha mchukue viasi wakaenda, na Wabondei walipowaona walithani askari za Mdachi wanaitwa kwenda zao, bassi haya sisi tutoke msituni tuwapige, marra askari walipokwisha kupewa viasi wakawafukuza tena Wabondei, nao Wabondei wakaingia mwituni vilevile hatta vita ikaisha Wabondei wakarudi kwao na Mdachi akarudi kwake.

HABARI ZA KIUNGANI.

October 4, Waalimu wawili Daudi Machina na Samwil Chiponde nduguye, wametoka hapa kwenda Newala kuwatazama jamaa zao na kurudi tena. Mtoto mmoja Nikolao Mchege alikuwa akienda Kanisani majira ya usiku, marra akaumwa na kinyoka kidogo, lakini hakumthuru, illa mguu wake ulivimba tu kwa juma mbili, sasa amepona. Tena John B. Mdoe, Hugh Mhina na Wilfred Madudu walienda Magila kutazama jamaa zao nao wamerudi Oct. l6. Tena siku, ya Juma a mosi, alikuja hapa balyozi Lieut.

MSIMULIZI. 125

Smith akasema kama amemwona mtoto wa kiume ametupwa na wajoli wake sababu hawezi kidonda kikubwa mguuni na bwana wake amekufa, na Archdeacon Jones-Bateman akaamuru kuchukua kitanda kumleta hapa, bassi akaenda letwa mtoto, akaoshwa, akapewa nguo nzuri, kiisha akatiwa dawa naye yupo hapa hajambo kidogo siku hizi, naye amewekwa huru na anafurahi sana. Oct. 29, waalimu walitazamiwa akili (Examination) muda wa siku tatu.

Mwalimu Clement Kathibeni alitoka hapa kwenda kutembea Magila mwezi wa October, hatta Nov. 1 kwenyi siku kuu ya Watakatifu wote aliwasili hapa tena pamoja na Alfred Juma. Tena tunafurahiwa sisi watu wa Chama cha Paolo Mtakatifu kama Alfred Juma ameingia Chama Nov. 3, Nov. 7, Bwana Cecil Majaliwa ametufikia, naswi tumefurahi mno kumwona, naye amekuja kusudi aipokee kazi ya Ukasisi. Nov. 9, waalimu tulifanyiwa karamu pamoja na Bwana Cecil, tena Nov. 12 palikuwa na karamu ya watu wa Chama cha Paolo Mtakatifu. Tumeletewa Mathbahu nzuri ya Marmara tupu kwa Kanisa letu, na kwenyi Nov. 17 ndipo Mathbahu yetu imezinguliwa. Tena viti vya Kanisa letu vimeletwa, na tumeanza kuvitumia Nov. 21, navyo vimetoka Poona mji mmoja ulioko Hindi; Jana Nov. 26 Mwalimu Paul Kasese amewasili Unguja akitoka Masasi kuja kuoa, na leo yupo hapa Kiungani. Mtg.

HABARI ZA MSARAKA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nimeona heri niandike habari ninazozisikia na zinazotendeka hapa. Siku hizi kuna uthia mwingi sana; wa kwanza ndio huu. Juma a tatu nalienda kwenyi mji mmoja, na mkubwa wa mji huu ndiye Manyamoto. Lakini mbele ya kwenda huko nalimwambia Mbwewe anipe vijana wawili, na Maduda anipe vijana wawili.

MSIMULIZI. 126

Kwani hawa wawili Mbwewe na Maduda ndio waliokuwa wakimkaribisha huyu mtu ninayemwendea kwa Manyamoto ndipo nitajua ya kuwa nyie wawili hammo katika shauri hili la Semboja, ndiye mwivi wenyewe aliyeiba watoto. Hawa wawili Maduda na Mbwewe wakanipa hawa vijana. Nikafuatana nao hatta kwa Manyamoto, kwani ndiko aliko huyu mwivi, mbele ya kuingia mjini naliwaambia vijana wawili, waingie kwenda kupeleleza kama yupo, nami na wale vijana wawili waliosalia tukajificha mwituni. Bassi wale vijana wawili walipoenda wakamkuta huyu mwivi Semboja anasaga tumbako, wakarudi wakanipasha habari. Bassi mimi nikafikiri ya kuwa haifai kumfunga kwanza, kwani tukimfunga itakuwa uthia na kishindo na ikiwa uthia na kishindo hivi, Manyamoto atasema kwa nini hamkuja kwangu nikawapa maarifa ya kumkamata? Bassi tukamtafuta Manyamoto hatukumwona, tukaambiwa amekwenda mji wa pili. Tulipokwenda tukamkuta anafanya mashauri hayahaya ya kumkamata huyu mwivi wetu, tukafurahi sana. Bassi Manyamoto akasema, haya twende nikakupeni mmtakaye. Tulipokuwa tukienda kumbe naye Semboja anakuja, ana mkubwa wake, aliponiona mimi akajua ya kuwa naja kukamatwa, bassi alitupa kisogo akaenda zake, tukamwandama hatta saa a nne za usiku tusimpate. Bassi nikamwambia Manyamoto sharti amtafute sana, asipompata mji wake utatiwa moto na Madachi. Oct. 9 Watu wa Ngome waliniita wakasema njoo tukuulize, kwa kisa gani twatakiwa tupigwe na Madachi. Bassi nikaenda mimi na Clement Kathibeni, tukawaona watu tayari kupigana na Madachi, wangine upanga, wangine mkuki, wangine upinde, wangine bunduki. Tukaingia ndani ya mji tukasemezana tukaisha, halafu wakasema hatuwi rathi mpaka tuone barua ya Bwana wa Magila. Bassi assubui akaenda Clement na mtu

MSIMULIZI. 127

mmoja kutwaa barua iendayo Tanga kwa Madachi. Na katika siku zilizopita nimepatikana na mashaka, kwa maana nalifunga nyumba yangu pasipo kumwachilia mtu. Bassi nikaenda Magila. Siku ya pili yake niliporudi nikaona mlango uwazi. Bassi nikasema labuda nitamkuta mtu ndani. Nilipoingia mlango wa kwanza nikaona tena wa pili umefunguliwa, na nilipotupa jicho kwa mlango wa tatu, pia nikaona umefunguliwa. Bassi nilipoenda kwa huo mlango wa tatu, nikaona makasha yamevunjwa, na nguo zangu zote zimetwaliwa, na fetha kathawakatha zimekwenda. Bassi nikafanya bidii nimpate mtu huyu, lakini hakupatikana hatta leo. G.K.

HABARI ZA BWANA ASKOFU.

Mwezi uliokwisha, November, tulimtazamia afike hapa, kumbe twalisikia kwa simu katika Msumbiji kama amejaribu kupita Zambezi kufika Kilimeni, lakini ameendewa na Wamagololo wanaopigana na Wareno, akakimbizwa hatta Nyassa. Sasa tunamwonea mashaka njia gani atatokea pwani, wala habari zake zayidi hatunazo. Wala barua za Nyassa hazikupata kutufikia mwezi huu.